# Nipashe

Alhamisi Septemba 29, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581083

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




**NIFFER AKATAA KUTOKA NA KIBA**

UKURASA 27


SUPA JACKPOT

TZS. 1,034,905,195

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Aieleza** korti mauaji ya ofisa usalama aliyebeba mil. 400/-

UKURASA 5

# Uchaguzi wa CCM wabeba mageuzi

- **Vigogo** mikoa mikubwa wafyekwa... *Endelea ukurasa 2*
- **Orodha** kamili walioteuliwa... *Endelea ukurasa 9, 10 & 25*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### RIPOTI CAG YASIMAMISHA VIGOGO 5 HALMASHAURI

WATUMISHI watano wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu wamesimamishwa...

UKURASA WA 4

### WAITWA KUTOA MAONI SHERIA YA NDOA

WIZARA ya Katiba na Sheria imeanza kukusanya maoni ya wadau na...

UKURASA WA 5

### ATINGA KORTINI KUZUIA HARUSI, ATAKA MIL. 50/-

MFANYABIASHARA maarufu, Wilfred Mushi (57), amefungua kesi kwa hati...




Machifu wa Mkoa wa Mbeya, wakitembea kwenye barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM), wakati wakienda kufanya tambiko la kuzuia ajali kwenye mteremko wa Mlima Mbalizi mkoani humo juzi. **Habari zaidi Uk. 21**.
**PICHA: NEBART MSOKWA**

## Milioni moja wa Elimu Bure rasmi kidato I

UKURASA 3



## Waziri Ummy atoa hadhari hodi ebola

UKURASA 2

**MICHEZO** **DEJAN NDIYO KAMA MLIVYOSIKIA SIMBA** UK.32 **KABWELA** UK.7



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, akiwataka wananchi kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa ebola. Kulia ni Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichwale na Mkurugenzi wa Kinga wa wizara hiyo, Beatrice Mutayoba. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uchaguzi CCM wabeba mageuzi

**Na Waandishi Wetu**

NI mageuzi. Ndivyo hali halisi inavyoonekana ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) baada ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) kupitisha panga kali katika uteuzi wa wagombea nafasi za uenyekiti wa wilaya.

Uteuzi huo wa wagombea wa nafasi hizo muhimu katika ustawi wa chama, umeibua mshangao na maumivu kwa baadhi ya wilaya baada ya waliokuwa wakishikilia nafasi hizo kuenguliwa.

Mabadiliko hayo, ni dhahiri yamefanywa kwa vitendo kutokana na matamko na maono yaliyokuwa yakitolewa na viongozi wakuu wa chama hicho wakiwamo makamu Mwenyekiti Bara, Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, Katibu Mkuu Daniel Chongolo na Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka.

Viongozi hao katika ziara za kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na uhai wa chama, kwa nyakati tofauti walikuwa wakitamka wazi kwamba katika kuteua wagombea, chama hakitaangalia umaarufu wa watu bali weledi na uaminifu pamoja na maadili.

Aidha, walionya kuwa wanachama na makada watakaokiuka maadili ikiwamo kujihusisha na rushwa au kupanga safu ndani ya chama hatawavumiliwa, hivyo majina yao yatakatwa.

Kutokana na kauli hizo na yaliyofanyika katika uteuzi huo, ni dhahiri kwamba CCM imejibu kwa vitendo yale viongozi wake waliyokuwa wakiyakemea na kuonya kuwa hatua zitachukuliwa.

Uteuzi huo umeleta taswira mpya ndani ya chama kwa baadhi ya mikoa huku kiuhalisia ikionyesha kuwa CCM inajizatiti kwa kutengeneza safu imara kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani wa mwaka 2025 ambao dhamira kuu ni kushika dola ili kuendelea kutawala.

**DAR ARUDI MMOJA**

Katika uteuzi huo, waliokuwa wenyeviti katika kipindi kilichopita, aliyerejeshwa kugombea tena ni mmoja tu, Lucas Mgonjwa kutoka Wilaya ya Ubungo. Wengine, Ubaya Chuma (Ilala), Harold Maruma (Kinondoni), Henry Chaula (Kigamboni) na Almishi Hazali (Temeke) majina yao hayakurudi kwa ajili ya kuingia kwenye kinyang'anyiro.

Kadhalika, katika baadhi ya wilaya ambazo zimekuwa na vuguvugu la kisiasa, waliokuwa wakishika nafasi hizo pia wameenguliwa katika uteuzi mpya.

Mkoani Arusha, kwa mfano, aliyekuwa Mwenyekiti wa Wilaya ya Arusha, Joseph Massawe, jina lake halijarudi sambamba na Mwenyekiti wa Iringa Mjini, Abeid Kiponza.

Pia katika Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza, Wilson Mesha jina lake halijarejeshwa. Wengine ambao hawajarejeshwa katika Mkoa wa Arusha ni Farahani Mungure (Meru) na Ndirango Laizer wa Ngorongoro.

Wenyeviti wa zamani katika mkoa huo waliorejeshwa kugombea tena na wilaya zao katika mabano ni Lucian Akoonay (Karatu), Simon Saning'o (Arumeru) Joseph Sadra (Longido) na Wilson Kurambe (Monduli).

Katika Mkoa wa Dodoma, Shabani Kilalo (Dodoma Mjini), Stewart Masima (Bahi), Mussa Matari (Kongwa) na Meja Mstaafu Johnick Salingo wamerejeshwa kutetea nafasi zao wakati Francis Gambo (Chamwino) na George Chibwiye (Mpwapwa) wakienguliwa.

Killian Myenze aliyekuwa Mwenyekiti wa Wilaya ya Kilolo na Constantino Kihwele (Iringa Vijijini) wamerejeshwa kuwania nafasi hizo huku Daudi Yassin kama ilivyo kwa Kiponza (Iringa Mjini) akienguliwa.

**KILIMANJARO, SINGIDA WAPETA**

Mkoani Kilimanjaro, waliokuwa wenyeviti katika wilaya zote, Alhaj Omar Shamba (Moshi Mjini), Wilfred Mossi (Siha), Siril Mushi (Moshi Vijijini), Wang'uba Maganda (Hai), Jaffar Kandege (Mwanga) na Anthony Tesdha (Rombo) wote wamerejeshwa. Hata hivyo, aliyekuwa mwenyekiti katika wilaya ya Mwanga, Isaya Mungulu (Same) hakugombea tena, hivyo wagombea wapya watachuana.

Aidha, katika mkoa wa Singida, wenyeviti wote waliomaliza muda wao, wamerejeshwa kuwania tena nafasi hizo. Viongozi hao ni Lucia Mwiru (Singida Mjini), William Nyallandu (Singida Vijijini), Jumanne Makhanda (Manyoni), Mika Likapakapa (Ikungi), Samwel Joel (Iramba) na Lameck Itungi (Mkalama).

Katika Mkoa wa Mbeya, waliokuwa wanashikilia nafasi hizo wamerejeshwa isipokuwa Hashim Mwalyawa (Mbalari) pekee. Waliorejeshwa ni Akimu Mwalupindi (Mbeya Vijijini), Sam Mwakapala (Rungwe), Noel Chiwanga (Chunjya), Afrey Nsomba (Mbeya Mjini) na Patrick Mwampeta (Kyela).

Kwa upande wa Songwe, Hebron Kibona (Ileje) na Twist Mohamed (Momba) wameenguliwa ilhali Hamad Juma (Songwe) na Simon Mboya (Mbozi) wamerejeshwa.

Mkoa wa Njombe, Ona Nkwama (Makete), Stanley Kolimba (Ludewa), Mgaya (Njombe) wamerejeshwa kuwania nafasi hizo wakati Stephano Kinyangasi (Wanging'ombe) ameenguliwa.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mkuranga, Ally Makisano, ndiye pekee aliyeenguliwa katika mkoa wa Pwani huku Maulid Bundala (Kibaha Mjini), Abdul Marombwa (Kibiti), Khalfan Sika (Kisarawe), Rajabu Mbonde (Rufiji), Hassan Pango (Mafia) na Zahoro Abdul (Bagamoyo) wakirejeshwa kuwania nafasi hizo.

Katika Mkoa wa Rukwa, aliyekuwa mbunge machachari wa Nkasi Kusini, Ally Keisy, ameenguliwa kugombea nafasi hiyo wakati Alfred Mwanga (Kalambo), Engelbert Mwanisawa (Sumbawanga Vijijini) na Chami Chasuka (Sumbawanga Mjini) majina yao yamepitishwa tena kuwania nafasi hizo.

**TANGA MOTO**

Mkoa wa Tanga nao umekumbwa na mageuzi baada ya waliokuwa wenyeviti wa Pangani (Rajab Abdulrahman), Mohamed Kingalangala (Kilindi), Othman Malunda (Handeni) na Emmanuel Challe (Korogwe Mjini) kutorejeshwa kuwania nafasi zao.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa vigogo hao, Nassoro Nassoro (Korogwe Vijijini), Laick Gugu (Muheza), Ismail Kasomo (Mkinga na Hamis Mkoba (Tanga), wameteuliwa tena kugombea.

*** Imeandaliwa na Beatrice Shayo (DAR), Augusta Njoji (DODOMA), Lulu George na Steven William (TANGA), Godfrey Mushi (ARUSHA), Richard Makore (MWANZA), Ashton Balaigwa (MOROGORO), Nebart Msokwa (MBEYA) na Thobias Mwanakatwe (SINGIDA).**

# Waziri Ummy atoa hadhari hodi ebola

**Elizabeth Zaya na Golden Kisapile (TURDACo)**

SERIKALI imesema Tanzania iko kwenye tishio kubwa la kukumbwa na ugonjwa wa Ebola huku akiitaja mikoa ya Kagera, Mwanza, Geita, Mara na Kigoma kuwa kwenye hatari zaidi.

Vilevile, ameitaja mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Songwe, Mbeya na Dodoma kuwa katika hatari ya kati kutokana na mwingiliano wa viwanja vya ndege na vituo vya mabasi yanayotoka nchi jirani.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema ugonjwa huo haujaingia nchini lakini kuna hatari kubwa kupata kutokana na ukaribu wa eneo lililoathirika zaidi na ugonjwa huo wilayani Mubende, Uganda na mpaka wa Mutukula nchini.

"Tunasema Tanzania iko kwenye tishio kubwa la kukumbwa na ugonjwa huu kwa sababu Wilaya ya Mubende, Uganda iko umbali wa kilomita 130 kutoka makao makuu ya nchi hiyo, Kampala.

"Kutoka Kampala hadi Mutukula mkoani Kagera nchini ni umbali wa kilomita 220 na kutoka Mubende kwenda Mutukula kupitia Masaka ni umbali wa kilomita 230. Kwa hiyo, mnaweza kuona hatari iliyopo.

"Kuwapo kwa ugonjwa huu katika nchi jirani kunaweka nchi yetu katika hatari kubwa kutokana na mwingiliano wa shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia mipaka rasmi na isiyo rasmi," alisema.

Waziri Ummy alisema ili kukabiliana na tishio la ugonjwa huo nchini, tayari wamepeleka timu ya wataalamu ya kukabiliana na magonjwa ya milipuko katika mikoa iliyo kwenye hatari zaidi na maeneo yote ya mipakani.

Ummy alitoa maagizo kwa wakuu wa mikoa yote nchini na viongozi wa halmashauri kuandaa mpango wa kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo, kuimarisha ufuatiliaji na kutoa taarifa ya wahisiwa wenye dalili za Ebola katika maeneo yao kupitia mfumo wa magonjwa ya mlipuko na yanayopewa kipaumbele (IDSR).

"Ninawataka wakuu wa mikoa yote wasipuuze tetesi za wahisiwa wa ugonjwa huo, tunawaomba na wananchi nao watoe taarifa wanapohisi kuna mtu ana dalili hizo, ninasisitiza kwamba hatutapuuza tetesi zozote. Na ninaomba wakikutana na wagonjwa wenye homa kali wasiwapuuze, wawachunguze zaidi," aliagiza.

Maagizo mengine ni waganga wakuu wa mikoa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati kwa mganga mkuu wa serikali kuhusu tetesi za wahisiwa na mwenendo wa ufuatiliaji wa ugonjwa huo.

Pia kufuatilia ukaguzi wa afya za wasafiri wanaoingia nchini hususani kutoka nchi zilizoathirika na kuimarisha timu za haraka za kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ndani ya mikoa yao.

Waziri Ummy pia aliagiza kutolewa elimu kwa wananchi kuhusu ugonjwa huo na namna ya kujikinga, kuandaa na kuimarisha vituo vya matibabu ya wagonjwa wa kila halmashauri, kuhakikisha kuna dawa, vifaa tiba na kinga kwa ajili ya wagonjwa na watumishi wa afya katika maeneo yote muhimu.

Aliwataka kuandaa maeneo maalum kwa wanaohisiwa, mapumziko, miundombinu ya kunawa mikono ya maji tiririka katika ngazi ya kaya, taasisi, sehemu za biashara, stendi za mabasi, shuleni, nyumba za ibada na maeneo ya mikusanyiko.

Baadhi ya mikakati mingine aliyosema imechukuliwa katika kukabiliana na tishio hilo ni kuimarisha timu za haraka za uratibu ngazi zote, ikiwamo kuzungumza na wataalamu, kuimarisha uchunguzi wa wasafiri katika maeneo ya mipaka husuan yenye mwingiliano mkubwa na nchi ya Uganda.

Mingine ni kuimarisha huduma za upimaji Mkoa wa Kagera na kuweka huduma za maabara tembezi, kuhakikisha kuwapo vituo vya kuwahudumia wagonjwa watakaothibitika, kuimarisha mfumo wa usafirishaji wa sampuli kuhakikisha unafika katika Maabara ya Taifa ya Jamii Dar es Salaam.

**DALILI, MAAMBUKIZI**

Waziri Ummy alitaja dalili kuwa ni homa kali, kuchoka mwili, kuumwa viungo vya mwili, vidonda katika koo, kuhara, kutokwa damu katika matundu ya mwili ikiwamo puani, mdomoni, masikioni, machoni, na njia za haja kubwa na ndogo.

Alisema ugonjwa huo unaambukizwa kutoka mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa njia ya kugusa majimaji ya mwili ya mgonjwa hususan mate, machozi, damu, matapishi, haja ndogo na kubwa.

Ummy alisema pamoja na tishio la ugonjwa huo nchini, hawatafunga mipaka isipokuwa watawekeza zaidi katika kudhibiti kupitia mbinu mbalimbali walizozoweka.

Alitoa wito kwa wananchi kuepuka kutembelea maeneo yenye ugonjwa huo, kula nyama ambayo haijapikwa vizuri, mbichi au mizoga na kugusa mnyama mgonjwa.

# Milioni moja elimu bure rasmi sekondari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ZAIDI ya wanafunzi milioni moja walioanza elimu ya msingi wakati mpango wa elimu bure unaanzishwa, wanatarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza Januari, mwakani katika mikoa yote nchini.

Kutokana na idadi hiyo, serikali imetoa Sh. bilioni 160 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa mapya 8,000 kwenye shule za sekondari 2,439 ili kukabiliana na upungufu wa madarasa utakaotokana na ziada ya wanafunzi kidato cha kwanza mwaka 2023.

Kwa mwaka 2023, takribani wanafunzi 1,148,512 wanatarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza ambao ni zao la kwanza la elimu msingi bila ada.

Kutokana na ujenzi huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa ametoa maagizo mbalimbali ikiwamo ujenzi kukamilika ndani ya miezi miwili na nusu na halmashauri itakayoshindwa hatua zitachukuliwa kwa viongozi husika.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Waziri Bashungwa alisema hatua hiyo inatokana na nafasi zilizopo kwa sasa zinatosheleza kwa wanafunzi 454,902 tu kulingana na wanaohitimu kidato cha nne mwaka huu.

"Idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2022 ilikuwa 907,802 ikilinganishwa na wanafunzi 422,403 waliohitimu kidato cha nne, hivyo ilihitajika kuongeza miundombinu ya madarasa na vyoo, yenye kutosheleza nyongeza ya wanafunzi 485,399 wa ziada,"alisema.

Bashungwa alisema shule hizo zinatarajiwa kuanza muhula wa masomo Januari, mwakani na tayari Wizara imeshatuma fedha kwa mamlaka za serikali za mitaa nchini ili kuhakikisha ujenzi unafanyika kwa wakati.

Aliwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha wanafuatilia hatua zote za ujenzi wa vyumba vya madarasa katika maeneo yao na kuhakikisha ujenzi unakamilika ndani ya miezi miwili na nusu kuanzia jana.

"Viongozi hawa wanapaswa kuwasimamia wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kufanya matumizi sahihi ya fedha zilizotolewa na wakumbushwe kufuata miongozo inayotolewa juu ya fedha hizo, ili kupata thamani halisi ya fedha kwa miradi inayotekelezwa," alisema.

Pia aliwaagiza kufuatilia kwa ukaribu ukamilishaji wa ujenzi wa shule mpya kupitia mradi wa SEQUIP ili kusajiliwa na kupokea wanafunzi Januari, 2023.

"Miradi yote inayoendelea kwenye maeneo yenu inapaswa kukamilika kabla au ifikapo Oktoba 31, mwaka huu, kama nilivyoelekeza hapo awali," alisema.

Waziri aliagiza kila mkoa uandae na kuwasilisha Ofisi ya Rais-TAMISEMI mkakati wake wa kukabiliana na tatizo la miundombinu kwa wanafunzi wapya wanaoandikishwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Alimwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI kuwaelekeza makatibu tawala wa mikoa wote nchini kuhakikisha wanafuatilia kwa karibu hatua zote za ujenzi na kuwasimamia wakurugenzi kukamilisha ujenzi.

"Naagiza hatua stahiki kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa mtendaji yeyote atakayekwamisha juhudi za serikali za kuhakikisha wanafunzi wote watakaochaguliwa wanaanza masomo Januari mwaka 2023," alisisitiza.

# Kampuni 20 za Marekani zamulika fursa uwekezaji

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI 20 kutoka Marekani zimewasili nchini katika ziara ya kuangazia biashara za kilimo, nishati, huduma za afya na viwanda vya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe na Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright, walizindua ziara hiyo juzi jijini Dar es Salaam, yenye lengo la kujionea fursa za kiuchumi kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Naibu Waziri Kigahe alisema: "Marekani na Tanzania zimekuwa na uhusiano mzuri wa kirafiki tangu mwaka 1961, uhusiano uliojengeka kwenye kuheshimiana, maadili na matazamio ya pamoja ya kuwa na mustakabali wenye amani na ustawi zaidi.

"Marekani ni ya tatu miongoni mwa wawekezaji wakubwa zaidi wa kigeni Tanzania na imekuwa ikitoa msaada wa maendeleo na msaada mwingine katika kujenga uwezo wa kushughulikia masuala ya afya na elimu, kuchochea ukuaji mpana wa uchumi na kuimarisha usalama wa kikanda na wa uchumi nchini ili kudumisha maendeleo."

Balozi Wright alizipongeza kampuni hizo kwa uamuzi wao wa kuiangalia Tanzania kama mahali pa kuwekeza katika sekta muhimu za uchumi na kupanua biashara zao.

"Tunakaribisha ushiriki zaidi wa Wamarekani katika uchumi wa Tanzania, kwa hakika hili ni mojawapo ya malengo ya msingi kabisa ya ubalozi wetu.

"Kampuni za Kimarekani huja na ubunifu, ujuzi na mtaji lakini pia nia ya kuwafundisha Watanzania jinsi ya kusimamia na kuendesha biashara zao. Nafasi za ajira wanazozizalisha nchini sio zile za kada za chini tu, bali pia zile zinazohitaji stadi za juu za kiteknolojia na kiutawala," alisema Balozi Wright.

Jana ujumbe wa wafanyabiashara hao ulikwenda Zanzibar ambako utapokea maelezo kutoka kwa wawakilishi wa serikali na kufanya majadiliano na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar na kuhudhuria mkutano utakaohutubiwa na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman.


HBS Hannah Bennie Schools

**OPEN JOB VACANCIES - WE ARE HIRING**

- UPPER PRIMARY SCHOOL TEACHERS (5)
- LOWER PRIMARY SCHOOL TEACHERS (4)
- NURSERY/ DAY CARE TEACHERS (4)
- MANAGER HUMAN RESOURCES (1)
- MANAGER FINANCE & ADMINISTRATION (1)
- SENIOR SOFTWARE DEVELOPERS (4)
- PROPERTIES & PREMISES OFFICER (2)

For detail job descriptions, qualifications and mode of application, **visit www.hbs.ac.tz**

We DO NOT provide details related to Job applications/ vacancies over the phone, KINDLY DO NOT CALL , FOLLOW INSTRUCTIONS ON HOW TO APPLY FROM OUR WEBSITE **www.hbs.ac.tz** or email your enquiries

**Send Application before 30th october 2022**




217064902

# Wananchi waitwa kutoa maoni sheria ya ndoa

**Na Beatrice Shayo**

WIZARA ya Katiba na Sheria imeanza kukusanya maoni ya wadau na wananchi, ili kuwa na uelewa wa pamoja wa vifungu vinavyohitaji kufanyiwa marekebisho katika Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Taarifa hiyo iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, ilibainisha kuwa wizara inaendelea kupokea maoni ya wananchi kuhusu mapendekezo ya sheria kupitia dodoso lililoandaliwa ili kuwa na uelewa wa pamoja.

"Kwa sasa wizara inaendelea na ukusanyaji wa maoni ambapo imeendelea kukutana na wadau na makundi mbalimbali ikiwamo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, wabunge, viongozi wa dini, viongozi wa kimila, waendesha bodaboda na wengine," wizara hiyo ilisema katika taarifa yake.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kwa sasa timu ya wataalamu iko mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Lindi ikiendelea kukusanya maoni.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa wizara inauomba umma kuwa na utulivu kwa suala hilo linaloendelea la kukusanya na kuchambua maoni likikamilika litawasilisha bungeni, mapendekezo ya marekebisho ya sheria husika kwa ajili ya kuijadili na kupitishwa.

Mwaka 2016, Mahakama Kuu ya Tanzania katika kesi ya Rebecca Gyumi dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika maombi Na. 5 ya Mwaka 2016, ilitolewa uamuzi suala la umri wa kuolewa ama kuoa.

Mahakama Kuu ya Tanzania iliamua Sheria ya Ndoa ipitiwe upya ili kuondoa ubaguzi na kukosekana kwa usawa kati ya umri wa chini wa ndoa kwa ajili ya wavulana na wasichana.

Katika uamuzi uliotolewa na Jaji A. Munisi kwa niaba ya majaji wengine wawili, mahakama ilisema kuwa kifungu cha 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ni kinyume cha ibara ya 12, 13 na 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inatoa haki sawa kwa wote mbele ya sheria.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kabla ya uamuzi huo, serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kutunga sheria mpya na kurekebisha sheria zinazohusiana na upingaji wa ukatili wa jinsia na umri wa mtoto.

Alieleza jitihada zilizochukuliwa ni kutoa tafsiri ya mtoto katika sheria ya mikataba, sura ya 345 kwa kueleza umri ambao mtu anaweza kuingia katika mkataba kuwa ni yule ambaye amefikisha umri wa mtu mzima.

Ilieleza kuwa licha ya kutungwa kwa sheria ya mtoto ya mwaka 2009, suala la mtoto hususani mtoto wa kike katika sheria ya ndoa imeendelea kuwa tatizo katika jamii.

"Msingi wa changamoto hizo ni kukosekana kwa tafsiri moja ya kisheria kuhusu umri wa mtoto na umri wa kuoa na kuolewa," ilieleza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa mkanganyiko wa tafsiri ya kisheria wa umri wa mtoto ulisababisha mahakama kuielekeza serikali kufanya marekebisho vifungu, hivyo ili umri wa kuoa na kuolewa uwe ni miaka 18.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa tangu kutolewa kwa uamuzi huo wizara imeendelea na utekelezaji wake na kuchukua hatua mbalimbali, ikiwamo kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya ndoa kwa kuweka masharti ya kuolewa ama kuoa uwe ni miaka 18.

"Wizara iliwasiisha bungeni mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya ndoa kwa kuweka masharti ya kuusawazisha umri wa kuoa ama kuolewa uwe ni miaka 18," taarifa hiyo ilieleza.

**WADAU WANENA**

Tapo la Wanawake na Wasichana Tanzania wanataka wabunge kutekeleza jukumu lao la kikatiba la kuitaka serikali ilete muswada kwa ajili ya mabadiliko ya sheria ya ndoa.

Pia wanataka Wizara ya Katiba na Sheria kusitisha mchakato wa kukusanya maoni kwa wananchi na kujielekeza kwenye kutekeleza uamuzi wa Mahakama ya Rufani kama ilivyoelekezwa kwenye hukumu ya kesi ya Rebeca dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exhaud Kigahe (kushoto), akikabidhiwa tuzo ya shukrani na Mwenyekiti wa Mradi wa Kiuchumi wa Mkinga, Nauel Ali Assad, katika uzinduzi wa mradi huo, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni wageni walohudhuria hafla hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ripoti ya CAG yasimamisha vigogo watano halmashauri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATUMISHI watano wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu wamesimamishwa kazi kwa tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka akiwamo Mhasibu David Assey anayedaiwa kukopa fedha Sh. milioni 6.7 kwa ajili ya matumizi ya ofisi na kuzipeleka kwenye akaunti binafsi.

Wengine waliosimamishwa ni Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi, Juma Mavumo, aliyekuwa Kaimu Mweka Hazina, Ramadhani Mwakamyanda, Mweka Hazina wa sasa, Respicius Kagaruki na Mkuu wa Kitengo cha Tehama, Nyanda Msirikale ambao wamesimamishwa kulingana na hoja za ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alibainisha hayo jana jijini hapa baada ya kukamilisha ziara yake ya siku mbili mkoani Manyara.

Alisema Julai 12, mwaka huu, aliyekuwa anakaimu Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo (David Assey) aliandika barua kwa kampuni binafsi kukopa Sh. milioni 6.7 kwa ajili ya matumizi ya ofisi na kuelekeza fedha hizo kuwekwa kwenye akaunti yake binafsi.

Kuhusu waliosimamishwa kutokana na hoja za CAG, Bashungwa alisema taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha wa 2020/21 ilielekeza Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi, Juma Mvumo achukuliwe hatua stahiki kwa kushindwa kuandaa vyema masharti ya zabuni na tangazo lake pamoja na kutofanya ufuatiliaji na uhakiki wa uhalali wa kampuni ya M/S Dicsamo Traders General Supplies Co. Ltd.

"Taarifa imeonyesha kuwa aliyekuwa Kaimu Mweka Hazina, Mwakamyanda na Mweka Hazina wa sasa, Kagaruki, wachukuliwe hatua kwa kulipa gharama za uwakala kwenye akaunti ya binafsi badala ya akaunti ya kampuni M/S Dicsamo Traders iliyopewa zabuni ya kukusanya mapato ndani ya halmashauri Sh. 188,499,328 (milioni 188.499).

"Taarifa ya CAG pia ilielekeza Ofisa TEHAMA wa Halmashauri, Msirikale na Mweka Hazina, Kagaruki wachukuliwe hatua kwa kushindwa kusimamia vyema mfumo wa mapato na kuacha mashine za kukusanyia mapato kuendelea kuwa nje ya mtandao kwa kipindi kirefu cha kati ya siku nane hadi 1,051 (takribani miaka 3) bila ufuatilia," alisema.

Bashungwa alisema watumishi hao wamesimishwa kazi ili kupisha uchunguzi kutokana na kusababishia hasara halmashauri na matumizi mabaya ya madaraka na kuagiza mabaraza ya madiwani kuacha tabia ya kukubali kutoa msamaha kwa watumishi waliotajwa kwenye ripoti ya CAG.

## JKCI leo kupima moyo bila malipo

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), leo inatarajia kufanya upimaji wa moyo na kutoa matibabu yake hapo hapo bila malipo kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa jirani.

Vilevile, kutakuwa na uchangiaji damu kwa hiari wenye lengo la kuokoa maisha ya wagonjwa na kwamba mgonjwa mmoja anayefanyiwa upasuaji wa moyo, amekuwa akihitaji kati ya chupa sita hadi saba za damu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano JKCI, Genofeva Mtemu, upimaji huo utafanyika kwa watoto na watu wazima katika viwanja vya taasisi hiyo vilivyoko ndani ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Mtemu alisema katika kuadhimisha Siku ya Moyo Duniani, wataalamu wa JKCI kwa kushirikiana na Pharmacy ya Zydus wataendesha upimaji huo.

"Upimaji huu utaanza kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi jioni. Kutakuwa na wataalamu wa lishe ambao watatoa elimu ya lishe bora ambayo itawapa wananchi uelewa na kufuata mtindo bora wa maisha ambao utawaepusha na magonjwa ya moyo pamoja na magonjwa yasiyoambukiza ambayo mtu anaweza kuyaepuka kwa kufuata ushauri wa kitaalamu," alisema.

Alifafanua kuwa watakaokutwa na matatizo ya moyo watafanyiwa uchunguzi zaidi na kupatiwa matibabu hapo hapo.

"Tunawaomba wananchi mjitokeze kwa wingi kupima afya zetu kujua kama mna matatizo ya moyo, ili kuanza matibabu mapema kwa atakayebainika kuwa mgonjwa," alisema.

HABARI KITAIFA

# Aeleza kortini ofisa usalama alivyouawa, kuporwa mil. 400/-

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imeelezwa jinsi watu wawili wanaodaiwa majambazi walivyomshambulia kwa risasi na kumuua Ofisa Mwandamizi wa Idara ya Usalama wa Taifa, Silvanus Mzeru mwaka 2014 maeneo ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

Watuhumiwa wa mauaji hayo ni madereva bodaboda; Kelvin Lilai na Revocatus Rugalabamu wanaodaiwa kushiriki matukio mawili ya kumpora fedha Mzeru zinazokadiriwa kuwa ni Sh. milioni 400.

Akitoa ushahidi dhidi ya watuhumiwa hao jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Joyce Minde, Sajenti Mohamed (47), alidai watuhumiwa hao pia walimuua mlinzi wa KK Security, Frank Silayo maeneo ya Oysterbay jijini Dar es Salaam.

Mohamed ambaye ni kiongozi katika kikosi maalum cha upelelezi wa makosa ya mauaji na makosa ya kutumia silaha, alidai kuwa Julai 15, 2014, yeye pamoja na wenzake walipewa maelezo na aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Camillus Wambura kuchunguza mauji ya Mzeru yaliyotokea Aprili 29, mwaka huo.

Alidai baada ya taarifa hiyo, Julai 16, 2014 alikwenda Kanda Maalum ya Dar es Salaam na kukutana na askari Nicolaus aliyekuwa mpelelezi wa tukio lililotokea uwanja wa ndege, ambapo wakati huo kulikuwa na mtuhumiwa Mohamed Kazembe.

"Nilifanya naye mahojiano na kunieleza yeye ni mhalifu wa matukio ya kutumia silaha, akishirikiana na wenzake Lilai, Chinga, Mashaka Mwafongo, Rugalabamu na Omary Said," alidai shahidi huyo.

Sajenti Mohamed alidai miongoni mwa matukio waliyoyafanya ni la Februari 21, 2014 majira ya saa 3:30 usiku eneo la Oysterbay, walivunja vioo cha gari aina ya Nissan Patrol na kuchukua fedha zinazokadiriwa kuwa ni Sh. milioni 100, mali ya Mzeru.

Alidai kuwa baada ya tukio hilo, wakati wanaondoka kulikuwa na mlinzi wa KK Security ambaye alijaribu kuwafuata na walimfyatulia risasi na kusababisha kifo chake na pia walifanya tukio la pili Aprili 29, 2014 maeneo ya uwanja huo wa ndege.

Alidai katika tukio hilo walifanikiwa kupora fedha za kitanzania na za kigeni zinazokadiliwa kuwa ni Sh. milioni 300 na kusababisha kifo cha Mzeru baada ya kumshambulia kwa risasi na kufanikiwa kumpora fedha hizo.

Sajenti Mohamed alidai walianza kuzifanyia kazi taarifa hizo, ambapo Julai 17, 2014 walipata taarifa kutoka kwa msiri Said kuwa ni dereva bodaboda na kijiwe chake na kuegesha TAZARA, Dar es Salaam.

"Tulishirikiana na msiri tukaweka mtego Julai 18, 2014 saa moja na nusu asubuhi, Said wakati anatoka nyumbani kwake tulifanikiwa kumkamata na tukafanya naye mahojiano," alidai.

Katika mahojiano hayo, Said alikiri kuhusika na matukio hayo mawili ya kumpora Mzeru na pia alishirikiana na Kazembe, Chinga, Mashaka, Rugalabamu, Lilai ambapo aliwaunganisha na kufanikiwa kumkamata Lilai.

Alidai mshtakiwa alikamatwa Julai 19, 2014 eneo la Nangurukuru wakati wakielekea Masasi kumkamata Lilai huku wakielekezwa na mtuhumiwa Said, ambapo kazi yao ilishia hapo baada ya kukutana na mtuhumiwa eneo hilo akiwa na gari lake aina ya IST.

Mtuhumiwa Lilai aliwataja washirika wake na aliwasaidia kumpata mtuhumiwa Rugalabamu, ambapo aliweka mtego na kumkamata Julai 20, 2014 wakafanya naye mahojiano na yeye aliwasaidia polisi kumpata Mwafongo.

Alidai Mwafongo alikiri anamiliki silaha tatu kinyume cha sheria na yeye pamoja na Chinga ndiyo walifyatua risasi katika matukio hayo mawili na silaha zake huwa anazihifadhi kwa dada yake, Lucy Mwafongo anayeishi maeneo ya Vingunguti, Mtaa wa Tupendane.

Alidai walizingira nyumba ya Lucy wakafanikiwa kumkamata na pia walifanikiwa kupata silaha na risasi zilizotajwa na kaka yake, baada ya tukio kuisha walimrudisha Kituo cha Polisi Oysterbay.

Alidai ilipofika saa nane usiku, Mwafongo aliwaeleza polisi kwamba kuna silaha nyingine ameifukia nyuma ya viwanda vya Tanganyika Packers na baada ya kufika eneo hilo mshtakiwa alijaribu kutoroka ndipo akapigwa risasi ya paja na wakati anadondoka risasi nyingine ikampata mgongoni, walimkimbiza hospitalini lakini baadaye walipata taarifa kuwa alipoteza maisha.

# Atinga kortini kuzuia harusi

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

MFANYABIASHARA maarufu, Wilfred Mushi (57), amefungua kesi kwa hati ya dharura katika Mahakama ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, akiomba itoe zuio la usambazaji wa kadi na michango ya harusi ya mtu anayedaiwa kutumia jina lake kuchangisha fedha kwa ajili ya kugharamia harusi yake.

Mushi anayefanya biashara ya mazao ya nafaka katika mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro, amefungua kesi hiyo, huku akitaka kulipwa fidia ya jumla ya Sh. milioni 50 inayotokana na madhara aliyoyapata ndani ya ndoa yake.

Anayedaiwa kutumia jina hilo kuchangisha fedha hizo kwa njia haramu ili kugharamia harusi yake inayotarajiwa kufungwa mwezi Novemba mwaka huu, ni mlalamikiwa wa kwanza, Wilbard James Mushi na wengine ambao ni Gudila Lyimo, Stanley Mushi, Wilson Mushi na Anna Mushi.

Maombi hayo namba 10 ya mwaka 2022 yanayotokana na kesi ya msingi namba tisa ya mwaka huu, yalifunguliwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Hai, Julieth Mawole.

Akiwasilisha maombi hayo, Wakili wa Mwombaji, Elia Kiwia, alidai mahakamani kuwa mteja wake (Wilfred Mushi), kati ya tarehe 16 na 20 ya mwezi huu (Septemba 2022), alipata taarifa kuna harusi itafungwa Arusha na tayari kuna kadi zinazosambazwa kwa jila lake na mtu aitwaye Wilbard James Mushi.

Wakili huyo alidai mteja wake alipofanya utafiti baada ya kupata taarifa hiyo, alizipata kadi hizo zilizokuwa na jina lake, familia yake ya Bwana na Bibi James Wilfred Mushi, kwamba wanaomba mchango wa harusi kwa ajili ya Wilbard (muoaji).

Aliendelea kudai kuwa baada ya kuzipata kadi hizo, James na mkewe Caroline Mushi, kulitokea mzozo wa ndoa ambao unakaribia kuvunja ndoa yao, wakizozana kwamba 'imekuaje bwana anakusanya fedha na mke hana taarifa?'.

Alidai kuwa katika mzozo huo, mke amemtuhumu mumewe kuwa na watoto nje ya ndoa.

Vilevile, Wakili Kiwia alidai kuwa dhamira ya kufungua shauri hilo ni kuitaka mahakama kutoa zuio ili kadi hizo zisiendelee kusambazwa, lakini pia zikusanywe zote, pia madhara ambayo ameyapata ndani ya ndoa, hivyo mteja wake anataka alipwe Sh. milioni 50 kama fidia ya madhara ya jumla.

Baada ya maombi hayo kutolewa, Hakimu Mawole alitoa amri ya kusitisha usambazaji wa kadi hizo na uchangishaji michango ya fedha kwa ajili ya harusi kwa mdaiwa wa kwanza, Wilbard.

Hakimu Mawole pia alitoa hati ya kuitwa shaurini (summons) kwa wadaiwa hao, huku wakitakiwa kujibu kwa maandishi utetezi wao ndani ya siku 21. Kesi hiyo imeahirishwa hadi Oktoba 19 mwaka huu itakapotajwa tena mahakamani huko.




# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kila mwananchi achukue tahadhari tishio la ebola

**SERIKALI** jana ilitangaza kuwa Tanzania iko kwenye tishio kubwa la kukumbwa na ugonjwa wa ebola ambao kwa miaka mingi umekuwa ikizisumbua nchi jirani ikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Katika kutangaza tahadhari ya ugonjwa huo, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliitaja mikoa ya Kagera, Mwanza, Geita, Mara na Kigoma kuwa kwenye hatari zaidi huku Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Songwe, Mbeya na Dodoma kuwa katika hatari ya kati kutokana na mwingiliano wa viwanja vya ndege na vituo vya mabasi yanayotoka nchi jirani.

Akitangaza hatari hiyo, Waziri Ummy alisema ugonjwa huo haujaingia nchini lakini kuna hatari kubwa kupata kutokana na ukaribu wa eneo lililoathirika zaidi na ugonjwa huo wilayani Mubende, Uganda na mpaka wa Tanzania na Uganda wa Mutukula. Wilaya hiyo iko umbali wa kilomita 130 kutoka makao makuu ya nchi hiyo, Kampala.

Kadhalika, Kampala hadi Mutukula mkoani Kagera ni umbali wa kilomita 220 na kutoka Mubende kwenda Mutukula kupitia Masaka ni umbali wa kilomita 230, hivyo kuwapo kwa hatari kubwa ya kuwapo kwa ugonjwa huo kama tahadhari haitachukuliwa.

Licha ya umbali huo, ebola pia inaiweka Tanzania katika hatari kutokana na mwingiliano wa shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia mipaka rasmi na isiyo rasmi. Watu wa Tanzania hasa walioko mipakani huvuka mipaka na kwenda nchi jirani sambamba na wa nchi hizo kuvuka mipaka na kuingia nchini. Hatari hiyo pia inatokana na kuwapo kwa wasafiri wa anga na nchi kavu kutoka na kuingia Tanzania.

Pamoja na kutoa tahadhari hiyo, Waziri Ummy alisema tayari serikali imeanza kuchukua hatua za kukabiliana na ugonjwa huo ikiwamo kupeleka timu ya wataalamu ya kukabiliana na magonjwa ya milipuko katika mikoa iliyo kwenye hatari zaidi na maeneo yote ya mipakani.

Mbali na kupelekea timu ya wataalamu, serikali imewaagiza wakuu wa mikoa na viongozi wa mamlaka za serikali za mitaa kuandaa mpango wa kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo, kuimarisha ufuatiliaji na kutoa taarifa ya wahisiwa wenye dalili za ebola katika maeneo yao kupitia mfumo wa magonjwa ya mlipuko na yanayopewa kipaumbele (IDSR).

Serikali imeshatoa tahadhari juu ya tishio la ugonjwa huo ambao katika miaka kadhaa iliyopita, uligharimu maisha ya watu wengi hasa nchini DRC huku Shirika la Afya Duniani (WHO) likiongoza kampeni ya kudhibiti tatizo hilo.

Tishio la ebola linakuja huku Tanzania na dunia haijasahau madhara ya UVIKO- 19, ugonjwa ulioikumba dunia na kusababisha watu kupatwa na maradhi hayo pamoja na wengine kupoteza maisha. Kwa mantiki hiyo, jamii inapaswa kuchukua tahadhari ikiwa ni pamoja na kufuata taratibu zote za kujikinga.

Sambamba na kujikinga, hatua madhubuti zikiwamo kuwapima watu wanaoingia nchini kupitia vyombo vya usafiri hasa kwenye viwanja vya ndege na vituo vya mabasi. Pia ziandaliwe kambi maalum za kuwaweka watu watakaohisiwa au kujulikana kuwa na ugonjwa huo.

Aidha, kama ilivyo kuwa kwa UVIKO - 19, elimu ya afya kuhusu kujikinga na maradhi hayo inapaswa kutolewa kwa njia mbalimbali yakiwamo matangazo na picha za vikaragosi zinazoonyesha namna ya kujilinda na hatari hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

### Hili la Wajiki kupigania kunusuru mabinti, linapaswa kuungwa mkono

**HONGERA** Taasisi ya Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), kwa kuzindua tena awamu ya tano ya kampeni itwayo 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', yenye lengo mahususi la kupambana na rushwa ya ngono, utetezi wa haki za kinamama na watoto, pamoja na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Si hivyo tu. Bali mmekuwa bega kwa bega na jamii pale mnapo baini kuwapo kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na, unyanyasaji kwa wanawake, pamoja na vitendo vinavyoashiria rushwa ya ngono. Hii ni hatua kubwa yenye azma ya kupata kizazi chenye usawa na kisicho na dosari ya vitendo hivyo.

Lakini mbali na vyote hivyo, makusudio ya kutumia kampeni hiyo, ni kupaza sauti kwa jamii juu ya kupiga vita rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia, jambo ambalo linapaswa kuungwa mkono na wengi, kwa sababu suala la kumlinda mtoto wa kike ni jukumu letu sote.

Jambo lililovutia zaidi, ni pale waliposoma tathimini ya utoaji wa elimu kwa awamu zilizopita na kubainisha kuwa vitendo vya ukatili wa kijinsia pamoja na rushwa ya ngono vimepungua hizi ni habari njema na inaonyesha ni kwa jinsi gani jamii inapata uelewa kupitia taasisi hiyo.

Katika uzinduzi wa awamu hiyo ya tano, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Janeth Mawinza, alisema kampeni itajikita zaidi katika kuwapa elimu waendesha bodaboda, bajaji, na daladala, akibainisha kuwa kundi hilo ndio linaloongoza kwa kuwaharibu watoto wengi, kwa kuwashawishi kufanya vitendo viovu kupitia madhaifu yao ya kuhitaji lifti .

Akatamka: "Kampeni hii italenga zaidi kuwapa elimu madereva wa bodaboda, bajaji, daladala, na mabasi ya abiria kwa kupita kila kituo kutoa elimu juu ya masuala ya rushwa ya ngono, pamoja na kutoa vibandiko ambavyo vimebeba ujumbe unaokemea vitendo hivyo.

"Sisi tunashughulika zaidi na watu wanaohusika na usafirishaji, hasa madereva. Mwanzoni kabla ya kuanza kwa kampeni hii, tulibaini madereva daladala, bodaboda, na bajaji ndio sehemu kubwa ambako watoto wanaharibikia ni mahali ambako vitendo vya rushwa ya ngono vimekithiri kwa hiyo sisi tukaona tuanzie huko."

Alisema katika mazingira hayo wamepata mabalozi wanawapatia elimu juu ya masuala ya rushwa ya ngono na wao wanaenda kuwapatia wenzao kwenye vituo wanavyopaki, pia wamefika hadi shuleni na kuunda vilabu mbalimbali vya kufundisha namna ya watoto hao wanavyoweza kujiepusha na vitendo hivyo

"Naweza kusema, kwa awamu nne zilizopita wamefanikiwa kufikisha elimu hii kwa ukubwa na baadhi yao wameelimika na wamejua maana ya rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia, anaendelea kuwa ofisini kwetu tunapokea kesi nyingi na tunawasaidia wengi kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria ili kuapata haki zao" anasema mkurugenzi huyo.

Pamoja na mambo mazuri ambayo taasisi hiyo imeyafanya kwa awamu nne zilizopita, lakni bado mkurugenzi huyo anaangusha kilio chake kwa wadau mbalimbali kujitokeza kufadhili mradi huo.

"Sisi tunafadhiliwa na Women Fund Tanzania (WFT), kwa miaka yote hiyo minne na huu wa tano. Kwa hiyo, tunaomba wadau wengine wajitokeze kwa sababu bado tunahitaji kufika mikoani, lakini uwezo wa kifedha kwetu ni mdogo

"Lengo ni kukomboa kizazi chetu wenyewe inauma na inasikitisha unapoona mtoto wa kike amebakwa au ameshindwa kupata ajira kwa sababu amegoma kutoa tendo la ndoa, kwa hiyo tunaomba wafadhili wengi zaidi ili tuifikishe elimu hii mbali zaidi," anasistiza.

Katika uzinduzi wa kampeni hiyo taasisi hiyo iliambatana na Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma Takukuru Mkoa wa Kitakukuru Kinondoni, Bibie Msumi, ambaye mbali na kuunga mkono jitihada hizo, pia anakemea watu kujihusisha na rushwa yoyote ile akitolea angalizo kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

"Rushwa ya ngono inaua, inasababisha mimba zisizo na mpangilio, inasababisha magonjwa ya zinaa, inadhalilisha utu, na inaharibu saikolojia ya mtu, kwa hiyo niwaombe watanzania wote kutoa taarifa takukuru pale unapobaini viashiria vya rushwa ya ngono

"Ukishindwa zaidi, fika ofisi zetu zilizopo Magomeni, Dar es Salaam unaweza kuja pale ukatoa taarifa na tukalifuatilia suala hilo bega kwa bega mpaka kuhakikisha linashughulikiwa," anasema.

Pia katika kuzindua kampeni hiyo, Mratibu Msaidizi Jeshi La Polisi Dawati la Jinsia Mkoa wa Kipolisi Ilala, Joyce Kajiru, alisema kazi ya dawati hilo ni kushughulikia kesi hizo na kuwapeleka mahakamani wote wanaokutwa na hatia ya rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia.

## 'Sekta ya habari ina mchango mkubwa kukuza demokrasia'

**Na Mwandishi Wetu, ZARAGOZA**

WAANDISHI wa habari na wadau wa habari takriban 1,000 kutoka nchi zaidi ya 70 duniani ikiwamo Tanzania, wanashiriki Kongamano Kuu la 73 la siku tatu kuhusu umuhimu wa sekta ya habari duniani lilioanza jana katika Mji wa Zaragoza, Hispania.

Akifungua kongamano hilo, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya WAN - IFRA, Vincent Peyregne, alisema sekta ya habari duniani ni muhimu katika kukuza demokrasia na uhuru wa habari.

"Kuwapo kwa waandishi wa habari katika taifa lolote duniani kunasaidia kukuza demokrasia, hivyo ni muhimu wakaheshimiwa na kupewa haki yao ya kupata habari," alisema.

Kwa mujibu wa Peyregne, pamoja na kupitia vikwazo vingi na kufanya kazi katika mazingira magumu, waandishi wa habari wameendelea kutoa taarifa za kinachoendelea duniani.

Pia alizungumzia umuhimu wa vyombo vya kuendana na mabadiliko ya teknolojia ya kidigitali ambayo hayaepukiki.


Alisema mabadiliko hayo yametingisha hata vyombo vya habari vikubwa duniani na kuathiri mapato na kuwa kuna haja ya kufikiria njia mpya zitakazoifanya sekta hiyo hasa magazeti kuendelea kuwapo.

Katika kongamano hilo waandishi wa habari nguli kutoka vyombo mbalimbali wamealikwa kuzungumzia uzoefu wao wa mazingira ya kazi katika nchi wanazotoka hasa katika suala la uhuru wa vyombo vya habari.

Peyregne alisema katika kuhakikisha vyombo vya habari vinathaminiwa, taasisi yake imesaidia kutoa mafunzo na fedha za miradi inayohusu uandishi wa habari, ili sekta hiyo ikue na kuendelea kusaidia kuwakilisha sauti za wasiosikika.

Kongamano hilo limegawanyika katika mijadala tofauti ikiwamo ya jinsi ya vyombo vya habari vinavyoweza kuwa endelevu katika kazi zake.

## KABWELA




# MOI yafanya upasuaji wa kibingwa Mtwara

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) kwa mara ya kwanza imetoa huduma ya upasuaji wa kibingwa katika Hospitali mpya ya Rufani Kanda ya Kusini mkoani Mtwara.

Katika kambi ya siku tano inayoendelea mkoani humo, wananchi 280 wamejitokeza siku ya kwanza kupata huduma za matibabu kutoka kwa wataalamu 11 wa MOI.

Upasuaji huo wa kibingwa wa mifupa umefanywa na jopo la madaktari bingwa, wauguzi na wataalamu wa usingizi kutoka MOI kwa kushirikiana na wataalamu wa Hospitali ya Rufani ya Kusini Mtwara.

Kiongozi wa jopo la wataalamu kutoka MOI, Dk. Albert Ulimali, akizungumza jana mkoani humo, alisema jopo la wataalamu linatoa huduma za kibingwa za mifupa, ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu, ikiwa ni pamoja na kuwafanyia upasuaji wagonjwa.

"Tuko hapa katika Hospitali ya Kanda Kusini, tumetumwa na kiongozi wetu wa MOI, Dk. Respicious Boniface, tuje kuanzisha huduma zetu hapa, tunashukuru mwitikio wa wananchi umekua mkubwa ambapo kwa siku ya kwanza peke yake tuliwahudumia zaidi ya wagonjwa ya 280," alisema Dk. Ulimali.

Dk. Ulimali pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa ujenzi wa Hospitali ya Kanda Kusini pamoja na usimikaji wa vifaa vya kisasa.

Pia alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmad Abass na Mkuu wa Wilaya Mtwara, Dunstan Kyoba kwa mapokezi mazuri.

Daktari Bingwa wa Mifupa kutoka MOI, Dk. Tumaini Minja, alisema upasuaji wa kwanza katika hospitali hiyo umefanyika kwa mafanikio makubwa na huduma hizo zitaendelea kupatikana hospitalini huko, hivyo wakazi wa mikoa ya kusini wajitokeze kupata huduma.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kusini Mtwara, Dk. Jeofrey Ngomo, aliishukuru MOI kwa kusogeza huduma za kibingwa kwa wakazi wa mikoa ya kusini na sasa wagonjwa hawatalazimika kufuata huduma hizo jijini Dar es Salaam.



# Waziri Bashungwa aivulia kofia TEA

**Na Mwandishi Wetu,** MBULU

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Innocent Bashungwa, amepongeza jitihada za Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) katika ujenzi wa miundombinu ya elimu hapa nchini.

Alitoa pongezi hizo jana mjini hapo wakati akifungua rasmi mabweni mawili yaliyojengwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA kwa ajili ya wanafunzi wa kike.

Mabweni hayo yamejengwa kwenye Shule ya Sekondari ya Kainam ya Mbulu mkoani Manyara.

Akifungua mabweni hayo, Bashungwa alipongeza TEA kwa kazi nzuri inayofanya katika kuboresha miundombinu ya elimu nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabweni hayo.

Alisema ujenzi wa mabweni hayo utasaidia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi hao kwani wataondokana na adha ya kusafiri umbali mrefu kwenda shuleni.

Awali, Kaimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kainam, Atnasi Massay, alisema mradi huo umesaidia wanafunzi kufanya vizuri kwa kuwa umewaepusha na vishawishi kwa kuishi katika mazingira ya utulivu.

"Kupitia mradi huu wa mabweni watoto wetu wamepata fursa ya kusoma na kupata utulivu na taaluma ya shule yetu imekuwa kwa maana sasa ni ya kwanza katika Halmshauri ya Mji wa Mbulu kitaaluma kwa matokeo ya mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne na cha pili mwaka 2020 na 2021", alisema.

"Sisi tumefurahishwa mno na ujenzi wa mabweni haya tunaipongeza serikali kupitia TEA huu ni msaada mkubwa sana kwetu na mkombozi kwa wasichana hawa," alisema.

Meneja Miradi wa TEA, Masozi Nyirenda, alisema TEA kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa, imetumia Sh. bilioni 1.39 katika miradi mbalimbali mkoani Manyara katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20.

# Maandalizi jukwaa sera ukatili yaiva

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

JOPO la wanaharakati wa haki za binadamu na watetezi wa makundi ya jamii ya pembezoni, wameanza maandalizi ya kuitisha jukwaa la kitaifa la kisera, litakalofanyika Novemba, mwaka huu.

Pamoja na mambo mengine, jukwaa hilo linalenga zaidi kuangalia sera na sheria zinazofifisha vita dhidi ya ukatili.

Akitoa taarifa kwa wadau wa masuala ya ukatili wa kijinsia wa mkoa wa Kilimanjaro, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la TUSONGE CDO, Aginatha Rutazaa, alisema watekelezaji wa mradi huo na washirika wenza, wameona kuna uhitaji mkubwa wa kuitisha kikao cha pamoja cha jukwaa la kisera, ambalo watakaa na watoa maamuzi kutoka kwenye maeneo mbalimbali kwenye ngazi za kijamii, kiwilaya, kimkoa na kitaifa.

TUSONGE CDO, inatekeleza Mradi wa Kukuza Usawa na Elimu ya Haki za Binadamu (AEHRE) katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, chini ya Kituo cha Kimataifa cha Elimu ya Haki za Binadamu (Equitas).

"Tunaona kabisa kwamba kuna uhitaji wa kuangalia zile sera, ambazo zimejitokeza au sheria zilizojitokeza kwenye majadiliano haya, kwa kuonyesha kwamba ilikuwa ni kikwazo katika kufikia ule usawa tunaosema wa kijinsia, lakini pia kutokomeza ukatili wa kingono, tunaouona kwenye jamii, hasa kwa wasichana na wavulana. "Tathmini hii imekuja na sura, ambayo imetuonyesha kwa kiasi kikubwa kwamba kazi kubwa iliyofanyika kuanzia Novemba 2021 mpaka sasa Julai 2022 ya kupambana kutokomeza ukatili wa kingono kwa wanawake, wasichana na vijana, tumeweza kufikia mafanikio.

# TCRA yatengeneza njia za ubunifu wa TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inawapa wabunifu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) fursa ya kufikisha ubunifu wao katika jamii ili kuwezesha utatuzi wa kero za jamii.

Uwezesho huo unafanywa kwa kuwapa rasilimali adimu za mawasiliano yakiwamo masafa, kikoa cha DOT TZ na namba fupi, yaani short codes bila kulazimika kulipia tofauti na ilivyokuwa awali.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dk. Jabiri Bakari, alitangaza neema hiyo hivi karibuni jijini Dar es Salaam, akisema lengo lao ni kuhakikisha wabunifu wapya wa TEHAMA hawabaki nyuma na badala yake wasaidie kuongeza uwezo wa Tanzania kujenga uchumi wa kidijitali.

"Tumejipanga kuhakikisha wabunifu wapya hasa wa sekta ya TEHAMA wanaoweza kutatua matatizo katika jamii yetu, wanapata rasilimali hizi adimu za mawasiliano, ili washiriki katika uchumi wa kidijitali," alisema.

Rasilimali za mawasiliano za TCRA ni pamoja na misimbo mifupi ya namba kama vile USSD; kikoa cha .tz, na masafa ya mawasiliano.

Kuhusu muda wa matumizi wa rasilimali hizo za mawasiliano, Dk. Jabiri alisisitiza kuwa zinaweza kutumika kwa kipindi cha miezi mitatu kutoka wakati wa mgao, lakini anayekabidhiwa anaweza kuomba muda zaidi ikiwa atahitaji na hasa ikiwa ubunifu wake haujafikia lengo la kutoa huduma.

Alisema TCRA inashirikiana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kuhakikisha kwa ubunifu wa TEHAMA waliohakikiwa, wanapata rasilimali wanazohitaji kupitia mchakato ambao TCRA inatoa rasilimali kwa wabunifu hao waliosajiliwa.

"Kwa wabunifu au wanaoanza kupata nyenzo za mawasiliano kwa huduma za majaribio kutoka TCRA, lazima kwanza wapate kibali kutoka COSTECH kisha wanapaswa kutuma maombi ya rasilimali za mawasiliano kwenda TCRA na kuambatanisha kibali kutoka COSTECH, nakala iliyothibitishwa ya kitambulisho cha Taifa cha mwombaji, sambamba na fomu nyingine zinazohitajiwa kwa kadri ya mwongozo uliopo," alisema.

Aliongeza kuwa wabunifu wanaohitaji kutumia rasilimali za mawasiliano zilizowekwa rasmi na TCRA kwa majaribio, watalazimika kutuma maombi kwanza kabla ya kutumia rasilimali hizo.

"Mwombaji anaweza kuwa mtu, kampuni au shirika. Watahitaji kutuma TCRA barua kueleza namna rasilimali hizo ikiwa watapewa zitakavyotumika, wapi zitatumika, lini wataanza kutumia na watapaswa kupata kibali cha COSTECH," alisema.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BESIX

Ballast Nedam

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA HUDUMA INAZOHUSIANA NA WAKALA WA MELI.**

**ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0009**

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza maandalizi ya awali ya ujenzi wa gati na kituo cha Upakiaji wa mafuta ghafi katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa utoaji wa huduma za:

**Wakala wa meli na huduma zinazohusiana na meli za mizigo na vifaa vya shughuli za baharini**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalopitia Uganda na Tanzania ikijumuisha gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Meli za Mafuta, Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:** Majukumu ya Mawakala wa Usafirishaji ni pamoja na :

- Kuhakikisha nafasi kwa meli inayoingia bandarini,
- Kumsaidia kupata boti za kuongoza na kuvuta meli, kukiwa na uhitaji,
- Kuhakikisha upatikanaji wa vibali vya forodha na huduma za bandari,
- Kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu kwa mabaharia (maji safi, malazi, viburudisho, usafiri na vibali, viza, matibabu, n.k.).
- Kusaidia na kurahisisha mawasiliano na mamlaka kwa wakati.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha vitu vifuatavyo:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo kusimamia kandarasi husika.
- Orodha ya uzoefu iliyo na historia ya ugavi / rekodi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika utekelezaji wa huduma za Kibali cha forodha, usafiri na huduma zinazohusiana na meli za mizigo na vifaa vya shughuli za baharini kulingana na viwango vya kimataifa katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linaloshabihiana
- Sera ya Ubora ya Kampuni na mipango ya afya na usalama eneo la kazi na uthibitisho wa: ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018), EN ISO 14732, EN ISO 90606-1, ISO 11484, EN ISO 90609-1, EN ISO 10893-8, 10893-11, au vyeti sawa;
- Kuzingatia kanuni za petroli na matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia, unashauriwa.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **Procurement@bbnjv.com. (Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **14 Oktoba 2022, saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

217067001

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BESIX

Ballast Nedam

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA HUDUMA ZA FORODHA, USAFIRI WA MIZIGO NA HUDUMA ZINAZOHUSIANA.**

**ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0010**

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza maandalizi ya awali ya ujenzi wa gati na kituo cha Upakiaji wa mafuta ghafi katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa utoaji wa huduma za:

**Forodha, usafiri na huduma zinazohusiana na mizigo inayoingia na kutoka nje ya nchi kwa njia ya anga, barabara na bahari.**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalopitia Uganda na Tanzania ikijumuisha gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Meli za Mafuta, Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA**:
Majukumu makuu chini ya mkataba yatajumuisha yafuatayo, pamoja na mambo mengine:

- Kufanikisha huduma za kibali cha forodha cha mizigo ya kuingia na kutoka nchini.
- Kudumisha mawasiliano kati ya BBNJV na Wasafirishaji wa Mizigo walioteuliwa ili kupata taarifa zote zinazohitajika na kuwasilisha nyaraka zote za mizigo, inayoingia na meli au anga, kwa mamlaka husika.
- Kuteua wafanyikazi watakaowajibika kusimamia kandarasi hii kwa ukamilifu.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo kusimamia kandarasi husika.
- Orodha ya uzoefu iliyo na historia ya ugavi / rekodi inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika utekelezaji wa huduma zinazohitajika za kufuatilia Kibali cha forodha, usafiri na huduma zinazohusiana kulingana na viwango vya kimataifa vya kawaida katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalolishabihiana.
- Sera ya Ubora ya Kampuni na mipango ya Afya na usalama eneo la kazi na uthibitisho wa Ubora: ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018), EN ISO 14732, EN ISO 90606-1, ISO 11484, EN ISO 90609-1, EN ISO 10893-8, 10893-11, au vyeti sawa;
- Kuzingatia kanuni za petroli na matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia, unashauriwa.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **Procurement@bbnjv.com** . **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **14 oktoba 2022, saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizokidhi matakwa ya awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni zao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

217067001

# ORODHA YA MAJINA YA WANACHAMA WA CCM WALIOTEULIWA KUGOMBEA NAFASI ZA UENYEKITI WA CCM WILAYA

**(a) TANZANIA BARA**

**1. MKOA WA ARUSHA**

| NA. | WILAYA | WALIOTEULIWA |
|---|---|---|
| 1. | KARATU | Lucian Akonaay KWASLEMA<br>Victoria Joseph MTENGA<br>Mustapha Kassim MBWAMBO<br>Sebastiana T. MASSAY |
| 2. | MERU | Ndewirwa Soori MBISE<br>Ephata Nnini NNKOH<br>Joshua Hungura MBWANA<br>Nathaniel Daniel KAAYA<br>Sara Martini MBISE |
| 3. | ARUMERU | Simon Ngoidimayye SANING'O<br>Noel Emmanuel SEVERE<br>Eng. David Saiguran LEMILIA<br>Esupat Elias NAIKARA |
| 4. | LONGIDO | Papa Nakuta MOLLEL<br>Joel Miagie MAUMBA<br>Joseph K. SADIRA |
| 5. | MONDULI | Wilson Lengima KURAMBE<br>Edward Sapunyu KONE<br>Sakaya Kabuti ALASHERI |
| 6. | NGORONGORO | Raphael Rise LON'GOI<br>Flora Olodi LAIZER<br>Abihudi Msemedi SAIDEYA<br>Lucas Oltusi OLEMASIAYA |
| 7 | ARUSHA | Wilfredy Ole Soillel MOLLEL<br>Elirehema Amos NNKO<br>Ally Juma MWINYIMVUA<br>Saipulani Abibakar RAMSSEY |

**2. DAR ES SALAAM**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | ILALA | Said Sultan SIDDE<br>Assaa Simba HAROUN<br>Salima Hamisi HILARY |
| 2 | KINONDONI | Kassim Shabani KAVITENDA<br>Shaweji Abdallah MKUMBURA<br>Pilly Athumani CHANDE |
| 3 | KIGAMBONI | Sikunjema Yahya SHABANI<br>Mponela Selemani MATHEI<br>Maimuna Mwinyipingu YUSUFU |
| 4 | UBUNGO | Lucas Michael MGONJA<br>Theresia Sarwat CHIHOTA<br>William MASANJA<br>Rogati Elias MBOWE |
| 5 | TEMEKE | Zena Yussuf MGAYA<br>Benard Mathew MWAKYEMBE<br>Evarist Ernest BARAGOMWA<br>Mariam John KAMBI |

**3. MKOA WA DODOMA**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | CHEMBA | Shabani Issa KILALO<br>Dr. Rogath Akiel MHINDI<br>Joseph Peter SAIN |
| 2 | BAHI | Stewart Ernest MASIMA<br>Ramadhani Juma MTAWA<br>Lawrence Uzzuca LWANJI |
| 3 | KONDOA | Abdallah Hussein MDEKE<br>Hija Bakari SURU<br>Kimolo Idd DARABU |
| 4 | MPWAPWA | Kepha Mapongo ISACK<br>Mark Salehe MGAZA<br>Donati Sasine NGHWAHENZI |
| 5 | KONGWA | Mussa Abdi MATARI<br>Winna Aizi KILONGE<br>Alfa Beda MWEGALWAWA |
| 6 | CHAMWINO | George Mathayo MALIMA<br>Lister Simon PETER<br>Asadi Bakari BARIDI |
| 7 | DODOMA MJINI | Meja (Mst) Johnick Risasi SALINGO<br>Charles Saimon MAMBA<br>Vanessa Frank MARIKA |

**4. MKOA WA GEITA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | BUKOMBE | Kevin Stephen MAKONDA<br>Matondo Kihanda LUTONJA<br>Robart oseph WANKA |
| 2 | GEITA | Barnabas Mhoja MAPANDE<br>Simon Luchagula NYAWAYI<br>Shadrack John MEDARD |
| 3 | MBOGWE | Lugenga Mohamed LUGENGA<br>Said Tangawizi BULIME<br>Odilia Francis MAHOLELO<br>Mathias Lusangija NYORORO |
| 4 | NYANG'WALE | Alhaj Adam Masoud MTORE<br>Solomn Ihare MABATI<br>Johaness Okinyi ABONG'O<br>Juster Zacharia KUMALIJA |
| 5 | CHATO | Goodluck Mafwimbo MUYABI<br>Rapael Ndaki MASAMBO<br>Barnabas Jacob NYEREMBE<br>John Matata STANSLAUS |

**5. MKOA WA IRINGA**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | IRINGA MJINI | Said Salim RUBBEYA<br>Elina Abel MARUMA<br>Leonard Raphael MGINA |
| 2 | IRINGA VIJIJINI | Costantino Teodos KIHWELE<br>Delfina Mwimble MTAVILALO<br>Yakub Japhary KIWANGA |
| 3 | KILOLO | Killian Edson MYENZI<br>Dr Chelastino Simbalimile MOFUGA<br>John Mwacheng'ombe KITEVE |
| 4 | MUFINDI | George Peter KAVENUKE<br>Zamoyoni Abdala KILYENYI<br>Daniel Ulindumu MWAISELA<br>Clever Marchon NDANZI |

**6. MKOA WA KAGERA**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | BUKOBA MJINI | Joas Muganyizi ZACHWA<br>Samson Celestin RWEBANGIRA<br>Murungi Badru KICHWABUTA<br>John Joseph MUGANGO |
| 2 | BIHARAMULO | Robert Alphonce MALULU<br>Anatory Kasazi CHOYA<br>Lucas Herman JOHN<br>Pilly Mkaka MAKUNENGE |
| 3 | BUKOBA VIJIJINI | Evarister Martine BABYEGEYA<br>Philipo Evarister KALOKOLA<br>Alistides Damian KWESIGABO |
| 4 | NGARA | Fadhil Christopher RUSAGE<br>George Jackison RUBAGORA<br>Hamis Hamad BALYANGA<br>Vitalis Misago NDAILAGIJE |
| 5 | MULEBA | Athumani Abdul KAHARA<br>Ludovick Dominic KABELINDE<br>Reinahold Tirutangwa MUJUNI |
| 6 | KYERWA | Abasi Mussa RUTALAMKA<br>Daniel Damian MUSABE<br>Flavius Mwebembezi KABALILA |
| 7 | KARAGWE | Paschal Kajura RWAMUGATA<br>Johansen Mufishagwe CHRISTIAN<br>Japhece Ezron RUZUMBA |
| 8 | MISENYI | Paskazia Sebastian NAKAWESI<br>Ferdinand John BANYENZAKI<br>Dr. Frank Theophil MUGANYIZI<br>Said Ibrahim SELUH |

**7. KATAVI**

| NA. | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1 | MPANDA | 1. Method Philip MTEPA<br>2. Emmanuel David MANAMBA<br>3. Mweji Kabudi JINYAM |
| 2 | TANGANYIKA | 1. Yassin M. KIBERITI<br>2. Matheo Z. LUCAS<br>3. Omar M. KAMWENDWE |
| 3 | MLELE | 1. Wolfugang Mizengo PINDA<br>2. Erick Joseph KAGUSA<br>3. Jojina Valeli KASAMYA |

**8. KIGOMA**

| NA. | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1 | KIGOMA VIJIJINI | 1. Deusidedth Syellu ALPHONCE<br>2. Halimenshi Kahena MAYONGA<br>3. Jeremiah Lameck BAYAGA |
| 2 | KIGOMA MJINI | 1. Ahmed Kakumba MWILIMA<br>2. Alh. Yassin Hamisi MTALIKWA<br>3. Masoud Mohamed MTABIRI |
| 3 | BUHIGWE | 1. Yasin John MDONYA<br>2. Ereneo Januari DYEGULA<br>3. Shauri Benedict KAYANDABILA |
| 4 | KAKONKO | 1.Samoja Sadock NDILALIHA<br>2. Fides Mahagara MUTWE<br>3. Fredrick Bisaga RUSIGA |
| 5 | KASULU | 1. Elias Yoram MASENDE<br>2.Mbelwa Abdallah CHIDEBWE<br>3.Veronica Petro NTIYALUNDURA |
| 6 | KIBONDO | 1. Hamis Salum TAHIRO<br>2.Evaristo Masigo BIDAGA<br>3.Sophia Edwini CHINDEYA<br>4.Abadani Manisha NTAWE |
| 7 | UVINZA | 1.Abdul Mpilipili KIGANZA<br>2.Majaliwa Zuber KAYANDABILA<br>3. Mohamed Khalfan GWAMA<br>4.Emmanuel John KARAYENGA |

**9. KILIMANJARO**

| NA. | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1 | MOSHI MJINI | 1.Alhaj. Omar Amin SHAMBA<br>2.Said Maulid MNDEME<br>3.Siri Seif NKYA<br>4.Faraji Kibaya SWAI |
| 2 | SIHA | 1.Edina Michael LUKUMAI<br>2.Luca Sendui LAIZER<br>3.Wilfred LUKA MOSSI |
| 3 | HAI | 1. Wang'uba W. MAGANDA<br>2.Christopher Shaban MADULU<br>3.Sophia Viggo REIFFENSTEIN<br>4.Ibahim Abdallah NDOSSA |
| 4 | MOSHI VIJIJINI | 1.Esther Richard KWAY<br>2. Abel Venance MASSAWE<br>3. Siril Ileti MUSHI |
| 5 | ROMBO | 1.Sophia Bartholomew KILAWE<br>2.Daniel Bonaventura SALEKIO<br>3.Anthony Joachim TESHA |
| 6 | MWANGA | 1.Jaffar Hamisi KANDEGE<br>2.Ibrahim Salim MNZAVA<br>3.Mamboleo Teri MSHANA |
| 7 | SAME | 1.Abdillah Suleiman MNYAMBO<br>2.Joseph Daniel KATERI<br>3.Beatrice Zilli MKINDI |

**10. LINDI**

| NA. | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1 | LINDI MJINI | 1.Abdallah Ally MADEBE<br>2.Leppy Hamisi NNEKE<br>3.Bakari Ali BWATAMU |
| 2 | NACHIGWEA | 1.Longnus NAMBOLE<br>2.Azizi Abdallah LIEGA<br>3.Raphael Petro SAANANE |
| 3 | KILWA | 1.Ally Kambi MANDAI<br>2.Saidi Ali TIMAMY<br>3.Raffi Hassani KUCHAO |
| 4 | LIWALE | 1.Mohamedi KITURA<br>2.Hemedi Abdallah NDEMANE<br>3.Kindamba Saidi MILINGO |
| 5 | RUANGWA | 1.Rashidi Hassan NAMKUBYA<br>2.Ibrahim Issa NDORO<br>3.Fatuma Rashidi NG'OMBO |
| 6 | LINDI VIJIJINI | 1.Athumani Seif HONGONYOKO<br>2.Livigha Musa LIVIGHA<br>3.Jenifa Kletus CHIMETA |

**11. MANYARA**

| NA. | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1 | HANANG' | 1. Thomas Simon AKONAAY<br>2. Samwel Singa QAWOGA<br>3.Emmanuel John GAMASA |
| 2 | KITETO | 1.Mohamedi Kiondo MAGULUKO<br>2.Bakari Mussa KILAMA<br>3.Hasani Erasto LOSIOKI |
| 3 | MBULU | 1.Afrikanus Samwel MMAO<br>2.Marco Daniel BADDO<br>3.Melkiadi Yakobo NARI |
| 4 | BABATI MJINI | 1.Elizabeth Bombo MALLEY<br>2.Frank Tlaghasi TIMOTHEO<br>3.Silas Wema GHALLO<br>4.Mohamed Farah OMAR |
| 5 | SIMANJIRO | 1.Kiria O. LAIZER<br>2.Ana Moinan SHININI<br>3.Haiyo Yamath MAMASITA |
| 6 | BABATI VIJIJINI | 1. Hhaibel Buu JACKSON<br>2.Aloyce Martin HAYUMA |

# HABARI KITAIFA

| | | |
|---|---|---|
| | | 3.Ezekiel Danghalo MAYO |

**12. MARA**

| NA. | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1 | RORYA | 1.Zephania Ombuo MIGIRE |
| | | 2.Hamis Petro MARANDI |
| | | 3.Ongujo Wakibara NYAMARWA |
| 2 | SERENGETI | 1.Jacob Begha GEHAMBA |
| | | 2.Mrobanda Japan MKOME |
| | | 3.Pasto Maiso MACHOTA |
| 3 | TARIME | 1.Marwa Daudi KEBOHI |
| | | 2.Mairo Marwa WANSOKO |
| | | 3.Nyerere Jackson MWERA |
| 4 | MUSOMA MJINI | 1.Benitha Benjamini KISHOBERA |
| | | 2.Magiri Benedictor MAREGESI |
| | | 3.Daudi Adam MISANGO |
| 5 | BUTIAMA | 1.Yohana Mwita MIRUMBE |
| | | 2.Christopher Marwa SIAGI |
| | | 3.Joseph Cosmas MAGESI |
| | | 4.Alfredy Mayani KIKUTE |
| 6 | BUNDA | 1.Sospeter Gomborojo MASAMBU |
| | | 2.Mayaya Abraham MAGESSE |
| | | 3.Eliya Mangarama SEENENE |
| 7 | MUSOMA VIJIJINI | 1.Gideon Matto EGWAGA |
| | | 2.Leftinant Chitala MUKAMA |
| | | 3.Denis M.Michael EKWABI |
| | | 4.Magafu Katura KITUNDULE |

**13. MKOA WA MBEYA**

| NA | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1. | MBEYA VIJIJINI | 1. Akimu Sebastian MWALUPINDI |
| | | 2. Japhet James MWANASENGA |
| | | 3. Ramadhani Mwantute MWANDALA |
| 2. | RUNGWE | 1. Meckson Moses MWAKIPUNGA |
| | | 2. Sam Aswulwisye MWAKAPALA |
| | | 3. Dr. Salatie Moyo MWAKYAMBIKI |
| | | 4. Elizabeth Sekile MWASONYA |
| 3. | CHUNYA | 1. Noel Zinginali CHIWANGA |
| | | 2. Shilla Nsungushe SHEYO |
| | | Edward Haisule MWASOTE |
| 4. | MBALALI | 1. Mbwilo Obadia MARY |
| | | 2. Mgao Pesipesi IGANAS |
| | | 3. Kitalima Jemsi LEONARD |
| 5. | MBEYA MJINI | 1. Afrey Athanas NSOMBA |
| | | 2. Tumpale Mwakisu LAIZER |
| | | 3. Moses Anyelwisye MWIDETE |
| 6. | KYELA | 1. Elias Ulisaja MWANJALA |
| | | 2. Rahabu Nsajigwa KAJENGA |
| | | 3. Patrick Mwanyosi MWAMPETA |

**14. MKOA WA MOROGORO**

| NA | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1. | MOROGORO MJINI | 1. Fikiri Hassan JUMA |
| | | 2. Hamza Yahya MFAUME |
| | | 3. Thadeo Sumuni MPULILA |
| | | 4. Francis Emily KAYENZI |
| 2. | MOROGORO VIJIJINI1. | 1. Gerold Filbert MLENGE |
| | | 2. Mohamed Athumani MZEE |
| | | 3. Rehema Muhamed MGAMBA |
| | | 4. Mzeru Deogratias PAUL |
| 3. | GAIRO | 1. Dastan Malema MZIWANDA |
| | | 2. Rehema Yhoana KIMOLETA |
| | | 3. Dunstan Daudi MWENDI |
| | | 4. Sebastian Charles MBWAIKI |
| 4. | ULANGA | 1. Asunta Antori NDITU |
| | | 2. Balua Hery PROSPER |
| | | 3. Haji Ahamadi MPANDA |
| 5. | KILOSA | 1. Amer Mbaraka AHMED |
| | | 2. Desderia Magnusi LIMBWENDA |
| | | 3. Michael Thomas MKOLOKOTI |
| 6. | KILOMBERO | 1. Mohamed Said MSUYA |
| | | 2. Mashaka Mohamed NGWEGA |
| | | 3. Samson Linus NGWILA |
| | | 4. Abdallah Salum KAMBANGWA |
| 7. | MVOMERO | 1. Asha Shabani KHALFANI |
| | | 2. Alfred Cosmas LUANDA |
| | | 3. Jaka Telesphory MICHAEL |
| | | 4. Maneno Khamisi CHISEPO |
| 8. | MALINYI | 1. Maximillian Japhal KIDAULA |
| | | 2. Peter Paul MKANIGALO |
| | | 3. Khalidi Adamu NALYOTO |

**15. MKOA WA MTWARA**

| NA | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1. | MASASI | 1. Arafati Ismail HASSANI |
| | | 2. Edward Victor MMAVELE |
| | | 3. Mariam Reube KASEMBE |
| | | 4. Margaret Joseph MALENGA |
| 2. | MTWARA VIJIJINI | 1. Nashir Mfaume PONTIYA |
| | | 2. Salima Ally MPAMBAIKE |
| | | 3. Swalehe Mohamedi LIVANGA |
| | | 4. Muharami Hassani MDIDIMA |
| 3. | NANYUMBU | 1. Bushiri Hassani MAGOMBO |
| | | 2. Rajabu Maganda CHILALA |
| | | 3. Rashidi Ally MROPE |
| | | 4. Zena Abasi STAUBI |
| 4. | NEWALA | 1. Jabili Mohamed MTANDA |
| | | 2. Ally Saidi MWAMBA |
| | | 3. Masudi Ismail MBELENJE |
| 5. | MTWARA MJINI | 1. Habiba Ally BAKARI |
| | | 2. Salumu Hassani NAIDA |
| | | 3. Swalehe Rashidi HITTU |
| 6. | TANDAHIMBA | 1. Ismail Abdallah MKADIMBA |
| | | 2. Farida Bakari CHILUNDA |
| | | 3. Kasimu Swalehe LIHUMBO |

**16. MKOA WA MWANZA**

| NA | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1. | ILEMELA | 1. Suzana Clement KABULA |
| | | 2. Mwl. Angelina OMUYANJA |
| | | 3. Yusuph Ernest BUJIKU |
| 2. | KWIMBA | 1. David Mayala MULONGO |
| | | 2. Sabana Lushu SALINJA |
| | | 3. Samson Mayunga KADASO |
| | | 4. Paul Sospeter GAMBAGO |
| 3. | NYAMAGANA | 1. Zebedayo Jonas ATHUMAN |
| | | 2. Peter John BEGGA |
| | | 3. Patrick NYABUGONGWE |
| 4. | SENGEREMA | |
| | | 1. Chasama Chasama KAMATA |
| | | 2. DM Mark Augustine MAKOYE |
| | | 3. Daud Bugisha MASELE |
| 5. | UKEREWE | 1. Ally Hamis MAMBILE |
| | | 2. Maxmillian MANDAGO |
| | | 3. Asia Omary ULIMWENGU |
| 6. | MISUNGWI | 1. Medard Daud MWIJAGE |
| | | 2. Michael Lushinge MASANJA |
| | | 3. Anthony Bahebe MASELE |
| 7. | MAGU | 1. Hassan Said JIMBO |
| | | 2. Enosy Ndobeji KALAMBO |
| | | 3. Jonathan Nkalawa LUPONDIJE |

**17. MKOA WA NJOMBE**

| NA | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1. | MAKETE | 1. Ona Amos NKWAMA |
| | | 2. Clemence Mwawite NGAJILO |
| | | 3. Peter T. MPONDA |
| | | 4. Ales Kete MBOGELA |
| 2. | WANGING'OMBE | 1. Frank Titus CHAULA |
| | | 2. Hamis Nurdin DILMURAD |
| | | 3. Monika John MGUMBA |
| 3. | LUDEWA | 1. Satanley Haule KOLIMBA |
| | | 2. Thobias LINGALANGALA |
| | | 3. Teopista MHAGAMA |
| | | 4. Silvester Alfons MGINA |
| 4. | NJOMBE | 1. Edward Pius MGAYA |
| | | 2. Joyce Zabron GAKYE |
| | | 3. Justin Idfonce NUSULUPIA |

**18. MKOA WA PWANI**

| NA | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1. | KIBAHA MJINI | 1. Bundala Maulid BUNDALA |
| | | 2. Mwajuma Amiri NYAMKA |
| | | 3. Sauda MPAMBALYOTO |
| | | 4.AbdallahAbushekhe MDIMU |
| 2. | KIBITI | 1. Abdul Jabiri MAROMBWA |
| | | 2. Abdallah Seif MPILI |
| | | 3. Juma Kassim NDARUKE |
| 3. | KISARAWE | 1. Khalfani Shabani SIKA |
| | | 2. Pazi Rajabu MAGIMBA |
| | | 3. Maalim Ramadhani KAVURUGA |
| 4. | RUFIJI | 1. Rajabu Omari MBONDE |
| | | 2. Hussein Yusufu LIKOSELO |
| | | 3. Nuru Omari MUHANI |
| 5. | KIBAHA VIJIJINI | 1. Mkali Saidi KANUSU |
| | | 2. Athumani Shabani ZANDA |
| | | 3. Angolile Aroni MWAKAJINGA |
| | | 4. Amina Ally KOBO |
| 6. | MAFIA | 1. Hassani Shomari PANGO |
| | | 2. Mohamed Hassan FAKI |
| | | 3. Hadija Salumu NASSORO |
| 7. | BAGAMOYO | 1. Abdul Rashid ZAHORO |
| | | 2. Amiri Idi MKANG'ATA |
| | | 3. Joyce Emanuel ABDI |
| 8. | MKURANGA | 1. Juma Said MAGAHILA |
| | | 2. Hadija Muhsin MATITU |
| | | 3. Sheni Omary KILINDO |
| | | 4. Nassoro Ally CHUMA |

**19. MKOA WA RUKWA**

| NA | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1. | KALAMBO | 1. Alfred Sokoni MWANGA |
| | | 2. Vitus Joseph NANDI |
| | | 3. Julias January TETE |
| 2. | SUMBAWANGA VIJIJINI | |
| | | 1. Engelbert Helman MWANISAWA |
| | | 2. Mahamud Leonce MGWENO |
| | | 3. Chrisant Joseph KALASA |
| 3. | NKASI | 1. Keissy Salum Soud ALJABRY |
| | | 2. Joshua Yortani MGAYA |
| | | 3. Kasawanga Adam SOSPETER |
| 4. | SUMBAWANGA MJINI | 1. Anuary Mohamed SAID |
| | | 2. Chami Siegfried CHASUKA |
| | | 3. Justus Athanaz KASALAMA |

**20. RUVUMA**

| NA. | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1 | NAMTUMBO | 1.Agrey Atupele MWANSASU |
| | | 2.Kassim Abdul NTARA |
| | | 3.Zuberi Said LIHUWI |
| | | 4.Vintan Lazarus NJEREKELA |
| 2 | NYASA | 1.Fidelis Kalodwick DUWE |
| | | 2.Abel Emmanuel KOMBA |
| | | 3.Moses Fulkwart NDUNGURU |
| | | 4.Charles Mackenzie HAULE |
| 3 | SONGEA | 1.Hamis Abdalah ALLY |
| | | 2.Cesilia William MAPUNDA |
| | | 3.Mwinyi Abdalah MSOLOMI |
| 4 | TUNDURU | 1.Ally Rashid SIMBA |
| | | 2.Rashidi Yunus MKOTA |
| | | 3.Abadallah Adam MTILA |
| 5 | SONGEA VIJIJINI | 1.Christa Joseph KOMBA |
| | | 2.Thomas Simon MASOLWA |
| | | 3.Twaibu Yusuphu MTOYOMBA |
| 6 | MBINGA | 1.Godluve Joakim KIGAE |
| | | 2.Joseph Agustino MDAKA |
| | | 3.Thabita Aidan LUNGU |

**21. SHINYANGA**

| NA. | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1 | SHINYANGA VIJIJINI | 1.Edward Helege NGELELA |
| | | 2.Anna James NG'WAGI |
| | | 3.Peter Shija KAWIZA |
| | | 4.Wenzetu Msabaha MGEJA |
| 2 | SHINYANGA MJINI | 1.Mokhe Warioba NASSOR |
| | | 2.Magile Anold MAKOMBE |
| | | 3.Pendo John SAWA |
| 3 | KISHAPU | 1.Ntelezu Malisha SHIJA |
| | | 2.Joyce Mduma BAYA |
| | | 3.Mafungwe Kulwa SEMBE |
| | | 4.Kashinje Juma BULUGU |
| 4 | KAHAMA | 1.Thomas Muyonga LUHAMYA |
| | | 2.Constantine Francis MAKOYE |
| | | 3.Michael Kulwa NSILE |

**22. SIMIYU**

| NA. | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1 | BARIADI | 1.Juliana Wille MAHONGO |
| | | 2.Zacharia Kwanza SHILIKALE |
| | | 3.Samwel Mweipagi HIBA |
| 2 | MASWA | 1.Eng. Paul Ndushi JIDAYI |
| | | 2.Mercy TIMANYWA |
| | | 3Marco BUKWIMBA |
| | | 4.Onesmo MAKODA |
| 3 | BUSEGA | 1.Kauli Idaso MAYALA |
| | | 2.Ramadhani Jimmy MSOKA |
| | | 3.Daud Juma NG'HINDI |
| 4 | ITILIMA | 1.Peter Bahini NONI |
| | | 2.Joseph Chimaguli KABALO |
| | | 3.Mhuli Ngeleja LUBUYI |
| 5 | MEATU | 1.Abdillah Hassan HAJI |
| | | 2.Philip Kahema KITINYA |

**23. SINGIDA**

| NA. | WILAYA | WALIOTEULIWA KUGOMBEA |
|---|---|---|
| 1. | SINGIDA MJINI | 1.Lucia Andrea MWIRU |
| | | 2.Athuman Hamis TIKAE |
| | | 3.Maulidi Juma SELEMANI |
| | | 4.Hassan Rajabu TATI |

INAENDELEA UKURASA 25



**HABARI ARUSHA**

# Tanzania yakabiliwa na uhaba wa madaktari upasuaji njia ya mkojo

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

TANZANIA inakabiliwa na uhaba wa madaktari bingwa wa upasuaji wa maradhi ya njia ya mkojo na uzazi, kutokana na waliopo ni 100 kutokukidhi mahitaji kulingana na idadi ya wagonjwa.

Rais wa Chama cha Madaktari Bingwa wa Upasuaji wa Maradhi ya Njia ya Mkojo na Uzazi (TAUS), Prof. Chalonde Yongolo, alisema hayo jana jijini hapo wakati akizungumza kwenye kongamano la kisayansi pamoja na mkutano mkuu wa TAUS.

Prof. Yongolo alisema idadi ya madaktari bingwa katika sekta hiyo, bado ni ndogo na kwa idadi iliyopo, daktari mmoja anahudumia wastani wa wagonjwa 600,000.

"Changamoto ya kuwapo madaktari bingwa inachangiwa na kutokuwapo kwa mafunzo ya awali nchini, juu ya masuala ya udaktari katika mfumo wa mkojo na uzazi. Mafunzo hayo yalikuwa yanatolewa nje ya nchi ila kwa sasa yameanza kutolewa rasmi nchini, hivyo tunatarajia kupata idadi ya madaktari bingwa wa kutosha," alisema.

Pia alisema wanataka kuhakikisha wanakuwa na mikakati ya kuwa na madaktari bingwa katika kila wilaya ili kuziba pengo hilo.

Awali, akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema uwapo wa chama hicho utasaidia kutoa elimu kwa jamii juu ya changamoto hizo na kuona umuhimu wa kuwaona wataalamu mapema kwa ajili ya kupunguza ukubwa wa tatizo.

Mongella aliwataka kujitangaza zaidi ili watambulike huku akiwataka kutoa elimu zaidi kwa jamii.

Naye Katibu Mkuu wa TAUS, Dk. Degratius Mahenda, alisema watu wenye umri kuanzia miaka 50 na kuendelea, ndio wanakabiliwa na changamoto ya matatizo ya mfumo wa mkojo na uzazi.

Sababu kubwa kwa mujibu wa Dk. Mahenda, ni kutokana na wengi wao kutokuwa na elimu ya kutosha ya kuwahi kuona wataalamu kabla ya tatizo kuwa kubwa zaidi.

Dk. Mahenda alisema kwa kipindi hiki elimu inaendelea kutolewa na kusaidia wananchi wengi kufika vituo vya afya na kupata huduma.

Alisema wamejipanga kuhakikisha wanatoa elimu zaidi kwa jamii ili wawe na uelewa wa kutosha katika masuala hayo na kuona umuhimu wa kupata matibabu na ushauri mapema.

Naye daktari bingwa wa upasuaji katika mfumo wa mkojo, uzazi kwa wanaume na upandikizaji wa figo, Dk. Victor Sensa, alisema wamejipanga kuhakikisha wanahamasisha vijana wengi waliopo vyuoni, kujiunga na fani hiyo, huku wakiiomba serikali iwanunulie vifaa kwani viliyopo ni vichache havitoshi.

# TANAPA yamtunuku tuzo Rais Samia

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limempa tuzo Rais Samia Hassan Suluhu ya kitambaa na kuthamini mchango wake wa kuinua sekta ya utalii nchini kwa kuhakikisha watalii wameongezeka na kuingiza fedha za kigeni, kupitia filamu yake ya The Royal Tour.

Pia TANAPA imetoa tuzo mbalimbali kwa wadau wao wa utalii waliofanya vizuri kwenye nyanja mbalimbali.

Akikabidhi tuzo ya Rais Samia kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, aliyepokea kwa niaba yake jana katika hafla iliyoandaliwa na shirika hilo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini TANAPA, Jenerali Mstaafu George Waitara, alisema Rais Samia amestahili tuzo hiyo kwa jitihada zake alizofanya za kufufua sekta ya utalii nchini.

"Rais amepambana kuinua sekta hii na sasa tunaona watalii wamefika Bara na Visiwani sababu ya jitihada na ubunifu wake wa kitengeneza filamu hii. Hali ya sekta hii ilikuwa mbaya na wadau wengi waliathirika baada ya janga la UVIKO -19. Sasa wote tuna furaha wageni wamefurika sababu ya jitihada na ujasiri wa Rais Samia," alisema.

Pia alisema kwa hali ilivyo sasa wanaamini ifikapo mwaka 2025/26 watalii wataongezeka kutoka milioni 1.5 ya sasa hadi kufikia milioni tano na kukusanya mapato yatokanayo na utalii Dola za Kimarekani bilioni sita.

Akipokea tuzo ya Rais Samia kwa niaba yake, Waziri Chana alishukuru TANAPA kwa kutambua ujasiri na kuthamini mchango wake wa kufufua sekta hiyo huku aliahidi kufikisha kwake tuzo hiyo. Alisema tuzo hiyo na zingine zimetolewa wakati mwafaka kwa sababu kila mwaka Septemba 27, huadhimishwa Siku ya Utalii Duniani.

"Nawaomba wadau wa utalii tuendelee kushirikiana na serikali ili kufikia lengo la kupata watalii hawa. Tunatarajia kupokea na naamini tutafanikiwa kwa sababu hali ya watalii kuingia nchini ni mzuri na kila mmoja anafurahia sababu ya jitihada za Rais Samia," alisema.

Kuhusu tuzo zingine zilizotolewa ni za kusafirisha watalii kwa boti, kupiga kasia kwa mtumbwi, kuruka kwa parachuti, usafirishaji kwa njia ya ndege, kambi za kudumu za watalii, kuingizia mapato makubwa TANAPA na kupanda farasi.

Filamu ya The Royal Tour ilizinduliwa Aprili 18, mwaka huu, New York, Aprili 21 Los Angeles nchini Marekani na Aprili 28 mkoani Arusha nchini, huku Mei 7 ikizinduliwa Zanzibar na Mei 8 jijini Dar es Salaam.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**BODI YA MFUKO WA BARABARA**

## KUTOA TAARIFA ZA HALI YA BARABARA KWA KUTUMIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI



***Bodi ya Mfuko wa Barabara imeunda Mfumo wa Kielektroniki wa kufuatilia hali ya barabara (e-Monitoring Application). Mfumo huu umeundwa mahsusi kuwawezesha wananchi, hasa watumiaji wa barabara, kushiriki katika kusimamia na kutunza miundombinu ya barabara katika maeneo wanayopita kwa kutuma taarifa muhimu za hali ya barabara.***

### Je ni taarifa gani mtumiaji wa barabara anaweza kutuma?

Taarifa ambazo mwananchi anaweza kutuma ni pamoja na barabara kujifunga, daraja au kalavati kubomoka au kuzolewa, mashimo hatarishi barabarani, ajali, miti kuanguka barabarani, gari kumwaga oil barabarani, gari kutengenezewa barabarani na wizi au uharibifu wa samani za barabara.



Barabara kukatika



Ajali barabarani



Shimo hatarishi barabarani



Sehemu ya barabara kuzolewa na maji

### Je mtumiaji wa barabara atatuma wapi taarifa hizo?

Taarifa hizo zitapelekwa kwa Wakala wa Barabara za Kitaifa (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) pamoja na Bodi ya Mfuko wa Barabara ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Aidha, mtoa taarifa atapokea mrejesho jinsi taarifa yake itakavyokuwa inafanyiwa kazi.

Tanzania National Roads Agency TANROADS

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY TARURA Improved Roads For Sustainable Development

### Je mtumiaji wa barabara atatumaje taarifa hizo?

Kupitia Mfumo huo, mtumiaji wa barabara anaweza kutuma taarifa kwa kutumia simu-janja (smart phones) au simu za kawaida (kitochi).

Taarifa hizo zinaweza kutumwa kwa njia ya maandishi, picha au video kutegemeana na aina ya simu.





**Jinsi ya Kupakua App ya Kutolea Taarifa**
1. Fungua "Play Store" au "App Store"
2. Tafuta neno "Barabara"
3. Bonyeza kitufe cha "Install"
4. Subiri mpaka ifike 100%
5. Bonyeza kitufe cha "Open" na uendelee kwa kufuata maelekezo.

**Au tuma taarifa kwa kufuata utaratibu ufuatao:**
1. Piga *152*00#
2. Chagua 4
3. Chagua 5
4. Fuata maelezo.

Je mtumiaji wa barabara atalipia gharama za kutuma taarifa hizo?


Bodi ya Mfuko wa Barabara itagharamia malipo yote ya kutuma taarifa na hivyo mwananchi hatalipa gharama yoyote.

Je maelezo zaidi juu ya Mfumo huo yanapatikanaje?

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Bodi ya Mfuko wa Barabara kupitia:**

Bodi ya Mfuko wa Barabara,
Makao Makuu Dodoma,
11 Barabara ya AMMAR,
41107 Dodoma Makulu, Dodoma
**Simu :** +255 26 2963277-8
**Nukushi:** +255 26 2963279-80
**Barua pepe:** info@roadsfund.go.tz
**Twitter:** @rfb_tz
**facebook:** www.facebook.com/RFBTZ/
**Instagram:** @rfb_tz

217059602





# Dereva Machame kortini madai ajali kuua watembea kwa miguu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

DEREVA wa basi la abiria, mali ya Kampuni ya Machame Express, Kombo Hassan, aliyesababisha ajali iliyoua watembea kwa miguu watatu katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, ameburuzwa kortini kujibu kesi inayomkabili.

Kombo (38), alifikishwa jana katika Mahakama ya Wilaya ya Moshi, baada ya kusababisha ajali hiyo Septemba 21, mwaka huu, katika eneo la Capetown, Mbuyuni, Manispaa ya Moshi.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka iliyosomwa mbele ya Hakimu Mkazi Erasto Philly, dereva huyo anadaiwa kusababisha vifo vya watu hao akiwa anaendesha basi hilo lenye namba za usajili T525 DZP.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa waliopoteza maisha katika ajali hiyo ni Kalista August (63) na wajukuu zake wawili, Jesca Taze (9) na Witnes Shija (7) wote wa familia moja ambao wanasoma Shule ya Msingi Mawenzi na Shule ya Msingi Muungano.

Akisoma hati hiyo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Nitice Emmanuel, alidai kuwa wanafunzi hao walifikwa na mauti wakiwa njiani kuelekea shuleni pamoja na bibi yao.

Emmanuel alidai kuwa kabla ya watu hao kupoteza maisha, watoto hao ambao ni wa darasa la nne na darasa la pili pamoja na bibi yao, walikuwa wakivuka barabara.

Ilidaiwa katika hati hiyo ya mashtaka kwamba mshtakiwa Kombo alitenda kosa hilo kinyume cha Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 2002 kifungu 40(1)(A), 63(2)(A) na 27(1)(A).

Baada ya kusomewa kosa hilo, Hakimu Erasto, aliahirisha kesi hiyo namba 191 ya mwaka 2022, akisema itarejea tena mahakamani hapo Oktoba 10, mwaka huu, kwa ajili ya kusomewa maelezo ya awali.

# Ukosefu choo stendi watishia mlipuko kipindupindu na kuhara

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA



HATARI kubwa ya magonjwa ya mlipuko ikiwamo kuhara na kipindupindu yanawanyemelea wafanyabiashara wadogo na abiria wanaotumia Kituo cha Mabasi cha Sanya Juu, Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, kutokana na kukosekana huduma ya choo eneo hilo.

Kwa sasa abiria, wananchi na wafanyabiashara wadogo hasa wa wanaofanya biashara ya chakula, maarufu kama mamalishe, wanalazimika kujisitiri kwa kujisaidia pembezoni mwa mabasi madogo ya abiria na kuta za majengo yaliyoko mkabala na kituo hicho.

Kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wakazi wa Sanya Juu, waliozungumza na Nipashe katika mahojiano maalum, waliiomba idara ya afya ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha, kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo ili kuepusha kuzuka kwa magonjwa ya mlipuko.

John Kileo, mmoja wa madereva wa mabasi madogo yanayofanya safari kati ya Bomang'ombe na Sanya Juu, alisema wengi wao wanalazimika kutembea umbali kidogo kwenda kujisaidia kwenye chanzo cha maji kilichoko karibu na stendi hiyo.

Naye Brigita Alex alisema kwa zaidi ya miezi sita sasa, watu wanajisaidia sehemu hizo huku akiiomba halmashauri ya wilaya hiyo kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo kwa haraka.

Anna Reuben, mamalishe wa eneo hilo, alisema choo cha umma kilichokuwapo awali kilijaa na serikali haikufanya utaratibu mwingine wa kukihuisha kwa kunyonya taka ili kitumike tena.

"Wateja wamekuwa wakiwasumbua baada ya kupata huduma ya chakula, wenye haja ndogo wanajisaidia kwenye ukuta na wa haja kubwa, inabidi kuwaonyesha choo kinachotumiwa na Kituo cha Polisi Sanya Juu. Hii ni hatari, ndiyo maana tunaomba halmashauri warekebishe hiki choo cha zamani walau," alisisitiza Reuben.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Duncan Urassa, alipoulizwa kuhusu malalamiko hayo, alisema: "Mimi ndiyo kwanza nimeyapata kwenu hayo malalamiko.

"Nakwenda kuzungumza na Mkurugenzi Mtendaji (Upendo Mangali) ili tuone tunafanya nini kunusuru hayo magonjwa ya mlipuko yasijitokeze, halafu ndipo tuchukue hatua nyingine kwa wahusika."


MWANGA HAKIKA BANK

DEFINING TOMORROW TODAY

**TANGAZO KWA WALIOKUWA WAFANYAKAZI WA MWANGA HAKIKA BANK LIMITED ZAMANI IKIITWA (EFC TANZANIA MICROFINANCE BANK, HAKIKA MICROFINANCE BANK NA MWANGA COMMUNITY BANK) AMBAO HAWAJALIPA MIKOPO YAO KULINGANA NA MAKUBALIANO**

**MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** inawataarifu na kuwataka wale wote wenye picha na majina hapo chini waliokuwa wafanyakazi wake ambao wanadaiwa mikopo na hawajalipa mikopo yao kwa mujibu wa makubaliano, kwamba wanatakiwa kurejesha fedha wanazodaiwa au kufika tawi lolote la **Mwanga Hakika Bank Limited** lililoko karibu kwa ajili ya kupata ufafanuzi na kulipa deni au kukubaliana jinsi ya kulipa madeni yao. Benki inatoa siku 14 (kuanzia tarehe ya tangazo hili) kwa wadaiwa sugu wote kutekeleza agizo hili.

Kukaidi agizo hili, Benki itachukua hatua za kisheria ili kuweza kurejesha fedha zake au,kukamata mali zao n.k.

**Mwanga Hakika Bank Limited** haitahusika na athari zozote zitakazotokana na matangazo ya taarifa za wadaiwa sugu kwasababu walikaidi agizo na notisi ya siku kumi na nne (14) iliyotolewa katika gazeti la **Mwananchi** la tarehe **Aprili 29, 2022** siku ya Ijumaa.

**MAJINA NA PICHA ZA WADAIWA;**



RAMADHANI ABDALLAH MSUYA



JAPHET WILLSON MSHANA.



RASHID ABEID KAJIA



THERESIA RAPHAEL LYAMBIKO



ELISAMEHE ZAWADIEL MSHANA



HUSNA RAMADHANI MAULID



JOEL GEORGE MSHANA



HASSAN BULLALI ALLY



HUSSEIN RASHID HUSSEIN



MARTIN THOMAS DIYAMI



INNOCENT REGNALD MACHA



AMANI BAKARI CHITANDA

**Kwa maelezo zaidi ya jinsi ya kuweza kulipa deni lako wasiliana na tawi la Mwanga Hakika Bank Limited lililopo karibu yako au kitengo cha ukusanyaji madeni makao makuu ya Benki kupitia mawasiliano yafuatayo; Simu namba: +255747666511, Barua pepe: recovery@mhbbank.co.tz**

**Imetolewa na:**
**Uongozi Wa Mwanga Hakika Bank Limited**

217068302

ama

ALHAMISI SEPTEMBA 29, 2022

AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 18

**Unateswa na mapunye na michirizi Sugu, muwasho? Sasa tiba hii hapa**



Ukurasa 19

Ilivyo hatari ya kichaa cha mbwa, mbinu za kujihami 'hakuna tiba'




Ukurasa 14

**Makubwa Hospitali ya Bugando inavyotibu saratani ya mtoto na uhalisia ulioko nchini**

AKIWA MKUTANONI MAREKANI...

# Waziri Ummy: Kila mwaka watoto 800 wanakutwa na saratani nchini

**Na Yasmine Protace**

MZIZI wa saratani ukoje? Inaelezwa kwamba kwenye mili ya binadamu kuna chembe hai nyingi zinazozaliana, kukua na kufa kwa mpangilio maalum.

Na kwa kuwa chembe hizo zinapobadilika na kuanza kuzaliana, hata kukua kwa utaratibu usio wa kawaida, ndio inatajwa kuwa mwanzo wa maradhi hayo ya saratani.

Inaelezwa chembe za saratani hufuata mfumo huo usio wa kawaida, zinazaliana haraka zaidi bila ya mpangilio na kukua kwa haraka zaidi na kuna wakati kuwa na umbile kubwa zaidi.

Kiafya, inaelezwa chembe hizo za saratani zisipodhibitiwa mapema, zina uwezo wa kusambaa na kumea sehemu nyingine za mwili wa mhusika.

**UNAJUAJE IPO?**

Saratani zipo za aina nyingi. Ni uvimbe unaojitokeza popote katika mwili wa binadamu, hauna maumivu yoyote mwanzoni kama kuna saratani.

Ni ugonjwa unaotokea kwa kuharibika na kubadilika chembe hai, na inapoanza kuzaliana, huitwa seli za kansa, hali inayowapata binadamu, wanyama na baadhi ya viumbe.

Inatajwa seli hiyo inaharibika, pia inarekebishika ikiwahiwa. Mara zote zisiporekebishwa, zinakuwa si za kawaida katika hali isiyohitajika mwilini na ndio huzalina zikiitwa seli kansa.

Seli hizo zisizokubalika, hutumia zile za kawaida kuzaliana na kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa kutumia damu ya mtu.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (katikati), akiwa na wadau kutoka Taasisi ya Global HOPE ya nchini Marekani, katika mkutano wa pembezoni baada ya Mkutano wa 77 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, jijini New York. **PICHA: MPIGAPICHA MAALUM**

Kansa ni ugonjwa unaotajwa kuua sana, ikikadiriwa duniani hadi ifikapo mwaka 2030, vifo huenda vikafika wastani milioni 13.1 kwa mwaka na aina ya kansa zinazoongoza kuua kila mwaka ni za: mapafu, tumbo, ini, utumbo na matiti.

**KWA WATOTO**

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema kila mwaka ni takriban watoto 800 hugundulika na ugonjwa wa saratani nchini, hivyo kuchangia ongezeko la vifo vinavyotokana na ugonjwa huo.

Ummy anayasema hayo katika kikao na Taasisi ya Global Hope iliyoko Texas nchini Marekani katika mkutano wa pembezoni, baada ya Mkutano Mkuu wa 77 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) jijini New York, Marekani.

Anafafanua:" Lakini kama serikali, tumeendelea kuboresha matibabu ya saratani kwa watoto, ili kuokoa maisha yao."

Waziri Ummy anasema inakadiriwa watoto wenye saratani wanaoendelea kuishi zaidi ya miaka miwili wanaogundulika ni kati ya asilimia 20 hadi 40, huku katika nchi zilizoendelea ni zaidi ya asilimia 80.

Anataja sababu ni kuchelewa kufanyika uchunguzi, wengine kutowajibikia tiba, gharama za usafiri na malazi, uchache wa vituo vinavyofanya uchunguzi na uhaba wa watumishi wenye ujuzi.

Ummy anamshukuru Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Global Hope, Dk. David Poplack, kwa msaada wanaoipatia Tanzania, kufadhili programu na kuwajengea uwezo watumishi, hususan katika fani za ubingwa bobezi wa matibabu ya saratani na magonjwa ya damu zaidi ya 10, wakitoa vifaa vya uchunguzi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Waziri anaiomba taasisi hiyo kuongeza idadi ya Watanzania wanaopatiwa ufadhili wa mafunzo ya utoaji huduma za saratani kwa kada za uuguzi, madaktari wafamasia na wataalamu maabara.

Pia ana ombi la kujengewa uwezo Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, katika kutoa huduma hizo kwa ujenzi na kupatiwa vifaa vya kisasa vya kuhudumia saratani.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Global Hope Dk. Polack, anasema, taasisi hiyo ipo tayari kushirikiana na Tanzania kutekeleza miradi ya kuimarisha huduma za saratani kitaifa.

***• Soma zaidi ya kansa kwa watoto uk. 14.***

AFYA

# Makubwa Hospitali ya Bugando inavyotibu saratani ya mtoto

• Pata simulizi ya mzazi jinsi mwanawe alivyoponyeshwa



Baadhi ya wazazi na watoto waliohudhuria katika maadhimisho ya mwezi wa kujenga uelewa kwa jamii juu ya saratani ya watoto. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

KWA wakazi wa Kanda ya Ziwa, saratani ni miongoni mwa magonjwa yanayoogopwa zaidi. Hata hivyo, waathirika huchelewa kufika kwenye matibabu na wanapolazimika kufika, muda unakuwa siyo rafiki, hata wakaangukia hatua mbaya.

Takwimu zinaonyesha ni ugonjwa unaoua wengi duniani, huku nchini kukiwapo ongezeko inayotajwa asilimia 45 ndio wanafika hospitalini wakiwa wamechelewa. Mikoa ya Kanda ya Ziwa inatajwa kuongoza kwa wagonjwa wengi, watoto na watu wazima.

Saratani ya watoto inaelezwa idadi ya watoto wanaofika katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando kupata matibabu ya saratani, wanakutwa na ugonjwa huo wakiwa katika hatua ngumu kutibika.

Bingwa wa Magonjwa ya Saratani na Damu kwa watoto hospitalini hapo, Dk. Heronima Kashaigili, anasema watoto 250 wenye saratani wanafika na kupatiwa matibabu hospitalini Bugando kila mwaka, sawa na watoto 20 kwa mwezi.

Dk. Kashaigili anasema katika Maadhimisho ya Mwezi (Septemba) wa Kujenga Uelewa kwa Jamii Juu ya Saratani ya Watoto yaliyofanyika hospitalini chini ya udhamini wa shirika la kimataifa linalotoa msaada wa tafiti za magonjwa ya saratani (ICCARE).

Anasema, mara nyingi saratani za watoto zikiwahiwa zinatibika na kuna ushahidi baadhi wamepona wakiendelea vizuri, ingawa kuna nafasi ndogo ya kujirudia, lakini bado inatibika.

> **Tangu afanyiwe upasuaji nafuata maelekezo ya madaktari, ikiwemo kuhudhuria kliniki kwa wakatina hivi sasa amemaliza kutumia dozi yake na vipimo vya madaktari vinaonyesha amepona kabisa na hana saratani.**

"Kutokana na uelewa kuwa chini watoto wengi wanafika hospitali (Bugando) wakiwa wamechelewa na wakiwa katika hatua ambayo inahitaji gharama sana kuitibu hiyo saratani," anaeleza.

Dk.Kashigili anafafanua saratani za watoto zipo na zinatibika, zinapogundulika mapema na hazina kisababishi maalumu, nyingi zinatokea na nyingine zinasababishwa na mabadiliko ya vinasaba huku dalili za ugonjwa huo mara nyingi zinafanana na magonjwa mengine ya kawaida ya watoto.

"Ulimwenguni kote tunatumia mwezi huu wa Septemba kuelimisha jamii kuwa dalili fulani wakiziona kwa mtoto, lazima wawahi mapema kituo cha kutoa huduma na wafikirie jambo la saratani," akifafanua:

"Ikiwamo upungufu wa damu, kuvimba tezi, kuvimba tumbo, kupungua uzito, kupata makovu, kukosa hamu ya kula, kuvuja damu, maumivu ya mwili, utando mweupe kwenye macho japo siyo kila utando ni dalili ya saratani na nyingine."

Anasema zamani watu walidhani ugonjwa unaowahusu watu wazima pekee, lakini ukweli hata watoto wanaugua saratani hasa ya matezi, figo, jicho na damu.

"Natoa wito kwa wazazi na jamii kuachana na imani potofu juu ya ugonjwa huo na badala yake wawapeleka watoto wao mapema katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya uchunguzi na kuanza matibabu mapema," anasema mtaalamu huyo.

### RAIS WA WADAU

Rais wa ICCARE nchini, Hillary Sued, anasema wametafiti na kubaini wagonjwa wengi walifika kutibiwa saratani hospitalini Bugando, wameishia kwenye dozi ya kwanza, kwa sababu gharama za kusubiri matibabu kuwa juu, hivyo wanatokomea na wengine wamefariki.

"Kutokana na changamoto hizo, ICCARE ilianzisha programu ya kuwasaidia watoto wenye saratani na waangalizi wao kumudu gharama za matibabu ya ugonjwa huo kwa kuwalipia hosteli, chakula na baadhi ya gharama zinazojitokeza wakati wa matibabu," anaeleza.

Meneja wa Ubia, Uwezeshaji na Mawasiliano wa mradi wa TCCP, Dk. Sarah Maongezi, anasema, tatizo lililopo katika huduma za saratani nchini ni wagonjwa kukosa taarifa sahihi, hata wakafika hospitalini katika hatua mbaya.

Anaeleza sababu ya uelewa mdogo wa jamii kuhusu saratani, kunachangia wagonjwa wengi kufikia hospitali wakiwa katika hatua ya tatu na ya nne. Hivyo, mradi huo unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa(AFD) na Aga Khan Foundation (AKF) unanuia kuboresha miundombinu na vifaa tiba vya kuhudumia saratani.

Anataja maeneo yanayoangaliwa kutoa maboresho yanajumuisha huduma na uhamasishaji elimu ya saratani katika jamii, kuendeleza na kukuza raslimali watu, kukuza taaluma za matibabu na kudumisha ushirikiano na utafiti wa saratani nchini.

### HALI NCHINI

Bingwa wa Upasuaji wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza, Sekou-Toure, Dk.Athanas Ngambakubi, anasema mwaka 2020 kunakadiriwa watu milioni 1.1 duniani waligundulika kuwa na saratani na kati yao 711,429 walifariki kutoka Afrika.

Dk. Athanas anasema Tanzania kulikuwapo na watu 40,464 waliopata ugonjwa huo na kati yao 26,945 walifariki, akitaja kuwepo aina 10 za saratani zinazoongoza, ambazo ni: Mlango wa kizazi, matiti, tezi dume, umio, ngozi, tumbo, ini, kibofu cha mkojo, haja kubwa na mapafu."

Bingwa wa tiba magonjwa ya saratani upande wa mionzi kutoka Hospitali ya Bugando, Dk. Beda Likonda, anaeleza jamii ikipata takwimu sahihi, elimu, tiba na tiba shufaa, inaweza kuleta mabadiliko chanya dhidi ya maradhi hayo.

Anasema kuna haja ya kuboresha huduma za afya kuanzia hatua za vituo vya tiba vikiwamo vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya na mikoa.

Makamu wa Rais Dk.Philip Mpango, akizindua jengo la wodi ya saratani katika hospitali ya Bugando, anasema njia sahihi ya kupunguza vifo vya saratani, ni kupitia wagonjwa wengi watakapopata matibabu kamilifu, akisema serikali imeshatoa Sh. bilioni 3.1 za ununuzi wa mashine ya mionzi.

Anaeleza serikali inaendesha harakati za kupambana na ugonjwa huo, huku elimu za kuondokana na vihatarishi vinavyochangia hatari hizo ikisisitizwa ambazo ni kufanya mazoezi, mlo kwa usahihi na kupunguza utumiaji pombe.

### SIMULIZI YA ALIYEPONA

Mkazi wa Mkolani Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza, Mecktilda Suluja, anasimulia ugonjwa wa saratani ya ini ulivyomtesa mwanawe, namna alivyowahi hospitali na hata akapona.

Anasimulia kwamba Jula mwaka jana, ikangundulika mtoto wake kuwa na uvimbe tumboni na akihisi ni la kawaida, lakini baada ya mwezi mmoja hali hiyo ikamtisha.

Mnamo Agosti mwaka jana, anasema akaenda hospitali kutibiwa na vipimo vinaonyesha dalili hata akashauriwa kwenda hospitalini Bugando na baada ya uchunguzi, kukagundulika ni saratani.

Suluja anasimulia kwamba binafsi akashtuka sana na wakaanza matibabu ya kemikali na baadaye walimpeleka Hospitali ya Taifa Muhimbili, alikofanyiwa upasuaji kuondoa sehemu iliyoathirika na ugonjwa huo.

"Tangu afanyiwe upasuaji nafuata maelekezo ya madaktari, ikiwemo kuhudhuria kliniki kwa wakatina hivi sasa amemaliza kutumia dozi yake na vipimo vya madaktari vinaonyesha amepona kabisa na hana saratani," anasimulia mzazi huyo.

AFYA

# Daktari bingwa: Maradhi ya akili tunaishi nayo, tunahofia kupima

## • Tukiingiza hesabu, zipo zaidi ya 100

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KILA inapofika siku ya Oktoba 10 ya kila mwaka, dunia inadhimisha Siku ya Afya ya Akili, ambayo ni kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Inaenda mbali kwa kurejea taarifa ya WHO mwaka 2019, kuna wastani kila sekunde 40 inayopita kuna wastani wa mtu mmoja anafariki kwa kujiua, huu kila mwaka wanakufa 800,000 duniani wakijiua, huku kukiwapo mtazamo wa kuongezeka.

Hapo inaibua swali la msingi, afya ya akili ni nini? Ufafanuzi wake ni kwamba "ustawi wa akili, kujitambua kwa ufanisi, uhuru, umahiri, utegemezi wa ulimwengu, na kujitambua kwa uwezo wa kiakili na kihemko, kati ya wengine."

Daktari wa Afya ya Akili kutoka Hospitali ya Rufani Mkoa wa Morogoro, Martin Andrew, anaueleza ustawi wa mtu, kwamba ni uwezo wa kukabiliana na hatua za kawaida za maisha, kazi yenye tija na mchango kwa jamii yake.

Anasema suala la kujiua na kuua linahusishwa na matatizo ya afya ya akili na sasa imefika hatua mtu haoni thamani ya ama maisha yake au mwingine, jambo linaoibua haja ya kupatikana tiba na elimu ya saikolojia haraka.

"Ubongo ni mithili ya jalala unabeba taka zote. Unafanana na kompyuta ambayo ina tenga la uchafu ambao bila kuusafisha kule ulipo, huwezi kujiridhisha kuwa umeondoka," anaeleza.

Pia anaangukia ufafanuzi kwamba afya ya akili inabeba tafsiri ya usalama wa kiakili na kisaikolojia au kutokuwapo usumbufu akilini, mfano msongo wa mawazo.

Inaelezwa kwamba, panapokuwapo mawazo chanya kibinadamu katika utendaji binafsi wa kila siku, inatoa uwezo wa kuridhisha, kimawazo na kitabia.

Ni jambo linalojumuisha uwezo wa mtu kufurahia maisha na kutengeneza mlingano, baina ya shughuli zako kimaisha pamoja na jitihada za kufika uwiano mzuri kisaikolojia, kutoka kwenye msongo unaotokana na magonjwa, misiba pia shida.

Uwezo wa mtu kuwa timamu kiakili huhusisha mtu kuweza kutatua matatizo yanayomkabili yahusuyo msongo wa mawazo katika maisha, shughuli za uzalishaji na mchango wa mtu husika katika jamii.

Dk. Andrew anawataka wanajamii kuona umuhimu wa kupima afya ya akili, kama wanavyopima magonjwa mengine, ili wajitambue na kupata tiba inapobidi, kuwaepusha na matukio mabaya, ikiwamo mauaji.

Anasema watu wengi wana tabia ya kupima magonjwa kama UTI, malaria na Ukimwi, huku



Mtu anayesadikiwa kuwa na shida ya afya ya akili.



Martin Andrew ambaye ni Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Akili katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Morogoro. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

wakiacha afya zao za akili, ambayo ndiyo tafsiri kuu, kichwa na mwili kwa magonjwa mengineyo.

Anaifafanulia Nipashe kwa kutumia nukuu ya kitaalamu kwamba: "Afya ya akili ni suala la mtu kujitambua binafsi yupo wapi na anafanya nini katika kupambana na msukumo wa maisha." Pia anasema zipo sababu za afya ya akili katika mikondo ya kijamii, saikolojia na kimaumbile, huku magonjwa ya akili yapo zaidi ya 100 yanayoweza kumpata kila mtu kwa wakati na namna yake.

Kwa mujibu wa bingwa huyo, suala la mtu kujiua linaangukia pale anapokosa thamani ya maisha yake, hata wengineo, hata kuweka msisitizo na umuhimu wa kupatikana elimu ya saikolojia na kundi la vijana likiwa wahusika wakuu.

### WADAU NA TATIZO

Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Shamira Abdalah, kupitia umoja wao uitwao Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA, anasema kutolewa nasaha hizo vyuoni, kutawasaidia wanafunzi walioko kwenye mapenzi, wawe na busara kuamua, penye migogoro kati yao.

Hapo anatoa mfano, mkasa wa mauaji ya wanafunzi wawili hivi karibuni katika chuo kikuu kimojawapo hivi karibuni, yamehusishwa na wivu wa kimapenzi.

> "Ubongo ni mithili ya jalala unabeba taka zote. Unafanana na kompyuta, ambayo ina tenga la uchafu ambao bila kuusafisha kule, ulipo huwezi kujiridhisha kuwa umeondoka.

Katibu wa kampeni ya SMAUJATA mkoa wa Morogoro, Jesca Kagunila, anakiri kuwepo shida kwenye suala la mauaji ya kijamii yakijumuisha chanzo cha afya ya akili katika kukabiliana nayo, wamejipanga kutoa elimu shuleni na kwenye vijiweni vya bodaboda na mtu wanajamii mmoja mmoja.

Jesca ambaye ni Ofisa Ustawi wa Jamii mkoani Morogoro, anaorodhesha jamii sasa imekosa; hofu ya Mungu, haina usawa, ina visasi na kukosekana maadili, utamaduni na kujiungia katika utamaduni wa kisasa.

Anasema katika kupambana na hali hiyo, ni vyema suala la malezi likashika kasi kwa wazazi kuwa ndio msingi bora wa kuimarisha jamii inayozunguka, ili baadaye watoto, vijana hadi wazee wasiwe na mioyo mizito kufika hatua ya mauaji.

"Ubongo ni mithili ya jalala unabeba taka zote. Unafanana na kompyuta, ambayo ina tenga la uchafu ambao bila kuusafisha kule, ulipo huwezi kujiridhisha kuwa umeondoka.

"Hivyo, wakati mwingine unajidanganya kuwa umesamehe kumbe bado umeyabeba kichwani. Hali inayopelekea kukuchosha na baadaye kukufanya ufikie uamuzi magumu," anafafanua.

### KAULI YA WHO

Taarifa ya WHO inaeleza tatizo la afya ya akili halizungumzwi sana katika jamii, lakini kwa baadhi ya magonjwa ya akili huanzia miaka 14 na kuendelea, jambo linalohatarisha zaidi usalama wa afya ya akili.

WHO inasema matatizo ya afya na ugonjwa wake hayachagui, kama yalivyo magonjwa mengine yanayoweza kumpata mtu yeyote, pasipo kujali jinsia, rika, desturi, rangi, dini, wasio na elimu, mali na hali ya ulemavu wa namna mbalimbali.

Shirika hilo linakana matatizo ya ugonjwa wa akili kutokana na udhaifu wa mtu au tatizo katika hali yake, ikisisitiza umuhimu wa kuzingatia tiba kudhibiti ugonjwa wa akili, pia namna ya kuwajali na kuwatunza wenye maradhi ya akili, hali inayowasaidia kurejea maisha ya kawaida.

Taarifa inasema jamii zinazowatenga na hata kuwaficha wenye ugonjwa wa akili, ikijumuisha kuwafungia chumbani na kuna wakati huwa ni giza, hivyo kuwazidishia athari za kiakili, sambamba na dhana ya kuwapatia majina yasiyofaa.

WHO inafafanua, kuwapo familia zinazowaficha na ndiyo jamii yenye hali hiyo ya akili wakihofia kunyanyapaliwa na jamii zao, kujihami na vidole vya unyanyapaa; laana na mikosi, jambo ambalo baya, japo hakuna ukweli.

AFYA

# Wanafunzi mabinti wanavyosaka kinga rasmi za mimba zahanati

• Wakunga: Wote wateja wetu rasmi; hawaipendi njia wanayochaguliwa



Ofisa Muuguzi kutoka Hospitali ya Muhimbili-Mloganzila, akifunda wanafunzi wa Shule ya Sekondari Malamba Mawili, Dar es Salaam, kuhusu magonjwa ya kuambukizwa kwa njia ya kijinsia, mwaka jana. **PICHA: MTANDAO**

**Na Pilly Kigome**

KATIKA jamii suala la mimba za ututoni kwa wasichana wadogo, limekuwa ni mtihani mkubwa. Pia namna ya kulitatua ni mtihani mkubwa, imechangia watu kupishana katika kutatua tatizo hilo.

Wako waliokaa mbali nalo, kwa kuwa wameshaona ni tatizo lisilozuilika, wako wengine wameona watumie mbinu mbadala za asili na wapo wanaotumia dini zao.

Kutokana na adha ya mimba za utotoni, serikali kupitia vyombo vyake vya afya, imeamua kukabiliana na tatizo hilo kwa uwazi ndani ya jamii kwa kuwafungulia milango mabinti kufika katika vituo vya afya wapewe elimu sahihi ya njia za uzazi, kwa mipango kama ya watu wazima, kukabili shida hiyo.

Serikali kupitia mkakati huo na kampeni maalum na njia hizo, tayari kuna vituo vya afya vimeshaanza kutekelezwa na mabinti hao wanapatiwa huduma hiyo, katika vituo mbalimbali vya afya nchini. Moja ya wakala wa mfano wanaotekeleza jukumu hilo ni Zahanati ya Gerezani iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam.

**HALI IKO HIVI**

Muuguzi Mkuu Mwandamizi wa Afya ya Jamii kutoka zahanati hiyo, Masha Kawambwa, anaiambia Nipashe kwamba huwa wanapokea watu wa kada zote katika huduma ya uzazi wa mpango, wakiwamo watoto wenye umri chini ya miaka 18, nao wanahudumiwa pindi wafikapo kupata huduma hiyo.

> **Njia hiyo ya kuzuia mapenzi inafaa pale inaposhindikana kabisa kwa binti kuacha mapenzi, wakati huo huo wanataka kutimiza malengo yao ya kimaisha.**

Masha anasema hawasiti kutoa huduma hiyo kwa watoto na iko kisheria, ikiwa na baraka ya Wizara ya Afya, akifafanua awali idadi ya watoto wanaofika kufuata huduma hiyo walikuwa wachache, lakini kadri elimu inavyozidi kutolewa, watoto wanajitokeza kwa wingi kupata huduma ya kinga za mimba.

Anasema, dira kuu katika hilo ni kutamani watoto wanatimiza malengo yao ya kimaisha na elimu kwa ujumla. Katika kituo hicho kunatolewa huduma kuanzia miaka 14 na kuendelea kwa wenye uhitaji na kabla ya mhusika kupatiwa huduma, anapewa elimu stahiki kuhusiana na njia hizo.

Kwa mujibu wa muuguzi huyo, katika njia hizo za uzazi wa mpango, kuna za muda mrefu ambazo na za muda mfupi, akivitaja ni kitanzi, vijiti na zile za muda mfupi ni vidonge, sindano, kalenda na mipira ya kiume na kike.

Mwaka jana 2021, vijana waliojitokeza chini ya umri miaka 19 kuanzia miaka 14 hadi 19, mwezi Januari walikuwa 76 waliojitokeza na mwezi Februari, walijitokeza 43. Kufika Machi walikuwa 36; mnamo Aprili 35; Mei walikuwa 26; Juni 79; Julai wako 93; Agosti 49; Septemba 57; Oktoba 33; Novemba 29 na Desemba 42.

Mtaalamu huyo anaiambia Nipashe, kuwa vijana wanapofika kituo hicho cha afya, huwa wanaanza kwa kupatiwa elimu ya njia zote za uzazi wa mpango na wanaohudumia afya.

Katika hilo, anasemahuwa wanatoa ushauri kwa wasichana hasa kwa walio wazito kukubali njia ya kufunga ndoa kwa muda mrefu, hivyo wanawashauri watumie njia ya kalenda na mipira na ndio wako wengi.

"Tukiwa kama wahudumu wa afya, pindi tunapotoa elimu tunatoa uhuru kwa mteja achague njia ambayo anaona ataweza kuimudu," anasema akisisitiza njia za uzazi wa mpango imekuwa suluhisho kwa watoto na wanafunzi kwa ujumla, kuwawezesha kutimiza malengo yao.

**MGANGA MKUU**

Mganga Mkuu wa zahanati hiyo, Dk. Joseph Robert, anaiambia Nipashe kuwa njia hizo zimeweza kuleta malengo chanya kwa watoto, kwa kuwa wanaweza kutimiza malengo yao wakiwa mbali na mimba zisizotarajiwa.

Dk. Robert anafafanua kwamba, njia bora zaidi kwa vijana ni ya kalenda na mipira, ikilinganishwa na nyinginezo kwa kuwa ni salama, ila anashauri vijana ambao bado hawajazaa, njia ya sindano na kijiti ni hatari kwao, kwani inaweza kuwakwamisha uzazi.

Anasema njia za kitanzi na vidonge, vinaweza kutumiwa na yeyote, lakini anashauri bora kuliko zote ni kuacha mapenzi kwa mabinti wajikite zaidi masomoni, kwani kukutana kimwili kwa namna yoyote ni kichocheo cha zinaa masomoni.

Mganga huyo anasema, njia hiyo ya kuzuia mapenzi inafaa pale inaposhindikana kabisa kwa binti kuacha mapenzi, wakati huo huo wanataka kutimiza malengo yao ya kimaisha.

**HALI YA MITAANI**

Dodoso ya Nipashe ilitinga mitaani na kushuhudia kuwapo mwitikio wa wazazi kupeleka watoto wao kwenye vituo vya afya, wakapatiwe huduma hiyo. Ni hoja inayoleta manufaa katika kumsogeza mtoto kimasomo na kuzuia mimba za utotoni.

Ushuhuda mmojawapo wa Nipashe ilikuwa pale eneo la Mbagala, Dar es Salaam, kukishuhudiwa mkasa wa binti mwanafunzi wa kidato cha kwanza, amekataa kutaja jina lake, umri na shule anayosoma, anapokiri kuwa anatumia njia hizo za kujikinga na mimba, pasipo wazazi wake kujua.

"Natumia tayari, nimeshachoma sindano mbili hadi sasa, nataka nifike mbali kimasomo nitimize ndoto zangu za kuwa injinia," anaeleza msichana huyo.

Pia mwingine anayejitambulisha (jina tunalo), msichana wa umri miaka 16, mkazi wa Dar es Salaam, anaungana na mweziwe akikiri kuwa katika orodha ya wanaotumia njia za uzazi wa mpango, akihamia kwenye sindano, baada ya kuachana na njia fupi.

Anaeleza sababu ya uamuzi wake ni kugundua matumizi ya mpira yako hatarishi kwake na kwa ujumla na kwamba wao wanafunzi wanaeleza kufurahia kupatikana huduma hiyo, kwani imekuwa mkombozi kwao kwa kuruhusiwa.

Nipashe inapodadisi vigezo vya uamuzi wao, imebaini wasichana watatu, kati ya watano iliyozungumza nao, wamedai wamejiongeza wenyewe kwa kuwa tayari wana uhusiano wa kimapenzi, hivyo wanashiriki kupata huduma hizi bila ya wazazi wao kujua.

Pia mabinti wawili wameeleza wamefika hatua hiyo kwa ushirikiano wa wazazi wao, wote wakisimulia hata mara ya kwanza ilikuwa vigumu kuafiki, lakini baadaye wakalazimika wawaachie, kwa mtazamo kuwawezesha watimize malengo yao kitaaluma.

Hata hivyo, kuna wazazi waliopewa msimamo kupinga kupeleka watoto wao wanaona kufanya hivyo kutaleta chachu ya mtoto kufanya mapenzi, jambo ambalo sio sawa kwao kushiriki mapenzi katika umri mdogo.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe, umegundua kuna upande wa watu wazima, nao njia hizo zimekuwa za ukombozi kwa wanawake wengi, ili kuwarahisishia kupanga idadi ya watoto, wakiwafanya wapumzike katika kipindi cha malezi.

**NJIA ZA KIENYEJI**

Pia imeelezwa kwamba kuna njia za kienyeji za uzazi wa mpango, kukishuhudiwa baadhi ya wanawake wakitumia, hata sio wengi wenye utashi nao.

Nipashe ikamdadisi muuza dawa za asili mwenye asili ya Kimasai anayethibitisha uwepo wa njia hizo. Lakini kwa sasa, analalamika wana changamoto ya wateja, wengi wakikimbilia kwenye dawa za kisasa.

AFYA

NYUMA YA PAZIA ANGALIZO LA WAZIRI...

# Namna Ebola inavyoshika jamii na nafasi Tanzania ilikosimama

**Na Maulid Mmbaga**

UGONJWA ebola sasa umegonga hodi upya taifa jirani Uganda inayopakana na Tanzania, ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Hiyo inachukua sura, huku Shirika la Afya Duniani (WHO) likitaja kirusi hicho kilichobainika mara ya kwanza mwaka 1976 katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wakati huo ikiitwa Zaire na nchini Sudan, ni hatari na kina uwezo kusababisha kifo kwa asilimia 90.

Wakati Tanzania ikitahadharisha wananchi wake, ugonjwa huo chanzo cha kirusi chake hadi sasa hakijulikani, lakini popo aina ya Pteropodidae anatajwa kuwa mbebaji wa kirusi hicho, kwa marejeo ya ushahidi uliopo wa kisanyansi.

Inaelezwa, kati ya mwaka 2013 na 2016 zaidi ya watu 11,000 walifariki kutokana na janga la Ebola Afrika Magharibi kuanzia nchini Guinea; ndani ya kipindi hicho, nako DRC hapakuwa salama na janga hilo. Mwaka 2014 viongozi wakuu wa nchi za Afrika Magharibi walikutana siku kadhaa nchini Liberia kuweka mikakati ya kudhibiti homa ya Ebola iliyoendelea kuliandama eneo hilo.

Walijadili umuhimu wa kuongeza ushirikiano kufikia muafaka wa kuishinda homa hiyo, ambayo hadi sasa inazidi kugharimu maisha ya wananchi.

Viongozi waliohudhuria mkutano huo uliofanyika mjini Monrovia ni pamoja na kutoka Sierra Leone, Guinea, Mali na Liberia, pia mkutano ulizijumuisha nchi jirani za Nigeria, Ivory Coast na Senegal.

Aliyekuwa mwakilishi wa Umoja wa Mataifa anayehusika na kampeni kukabiliana na Ebola, Anthony Banbury, aliwahimiza viongozi hao kuendelea kukutana ili kubadilishana ujuzi na taarifa muhimu kuhusu njia mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huo.



Wataalamu wa afya nchini Liberia, wakitoa huduma ya kuzuia kusambaa virusi vya Ebola. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### VIFAA TIBA & ELIMU

Naibu Waziri wa Afya nchini, Dk Godwin Mollel, anatoa maelekezo kwa waganga wakuu wa mikoa na halmashauri nchini, waimarishe utoaji elimu, ufuatiliaji wa ugonjwa, uchunguzi wa kitaalam na kuhakikisha upatikanaji vifaa tiba na kinga muhimu katika maeneo yao.

Dk. Mollel anawashauri wananchi kote kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa Ebola, baada ya nchi jirani Uganda kuthibitisha mlipuko mpya, akitamka: "Nimewaelekeza kuimarisha uchunguzi wa wageni wanaoingia nchini kupitia mipaka yetu ikiwemo matumizi ya vipima joto."

Vilevile anawataka wananchi kuchukua tahadhari, ikiwamo kunawa mikono kwa maji safi na sabuni, kuepuka kugusa mwili au maji ya mwili wa mhisiwa au mgonjwa wa Ebola na kuepuka safari zisizo za lazima kutembelea maeneo yaliyoathirika.



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel.

### MAPAMBANO UPYA

Waziri wa Afya wa Uganda, Margaret Muhanga, amethibitisha mlipuko mpya, baada ya kutokea kifo cha aliyepata maambukizi ya ebola, anayeeleza mwathiriwa alionyesha dalili kabla ya kuugua ugonjwa huo.

Anasema, timu ya kliniki imeshatoa sampuli za majaribio na kwamba matokeo yanathibitisha kuwa mgonjwa alikuwa na ugonjwa wa Ebola.

"Uganda ina uzoefu mkubwa katika kushughulikia milipuko na magonjwa ya milipuko ya aina hii, wizara imetuma timu katika wilaya ya Mubende kuimarisha ufuatiliaji na ufahamu wa jamii, umma unahimizwa kuwa waangalifu na watulivu wakati timu zikichukua hatua zinazohitajika," anasema.

Pia, anaeleza Wizara ya Afya Uganda na washirika wengine wametuma timu ya majibu ya haraka sehemu ya mlipuko huo ulioibuka, ili kusaidia timu katika ufuatiliaji wa anwani na udhibiti wa visa.

Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika, Dk. Matshidiso Moeti, anasema mkasa wa aina hiyo ambao ni nadra na ulithibitishwa na Taasisi ya Utafiti wa Virusi ya Uganda na kwamba, imechukuliwa sampuli kubaini virusi hivyo haraka.

Nchi hiyo ya Afrika Mashariki, iliripoti mlipuko wa ugonjwa huo mara ya mwisho mwaka 2012.

### MAAMBUKIZI YANAVYOTOKEA

Inaelezwa kuwa maambukizi ya virusi hivyo hutokea pindi mtu anapoambukizwa kupitia sehemu wazi ya mwili wake unapogusana na majimaji ya mgonjwa wa Ebola, pia kupitia matapishi, choo, mate, mbegu za kiume na damu.

WHO inasema maambukizi yanaweza kutokea, pia iwapo ngozi wazi ya mtu asiye na ugonjwa huo itakumbwa na maji yenye kirusi yaliyomo kwenye nguo chafu za mgonjwa, mashuka au sindano zilizotumika.

Pia, inabainisha kwamba zaidi ya wahudumu 100 wa afya wamekumbana na mazingira yenye maji, kutoka mwili wa mgonjwa wa ebola pindi wanapokuwa wanatoa huduma kwa wagonjwa hao.

> **"WHO haishauri familia au jamii kuhudumia wagonjwa wanaoweza kuwa na dalili za ebola majumbani mwao, badala yake wagonjwa husika wapate huduma stahiki hospitali au kituo cha afya.**

"Hii hutokea iwapo hawana mavazi stahili ya kujikinga au hawakuzingatia taratibu za kujikinga pindi wanapohudumia wagonjwa.

"WHO inataka watoa huduma wa afya katika ngazi zote iwe hospitali, kliniki, zahanati au vituo vya afya wapatiwe taarifa juu ya ugonjwa wa ebola, unavyoambukizwa na wazingatie mbinu za kuzuia kuenea kwake.

"WHO haishauri familia au jamii kuhudumia wagonjwa wanaoweza kuwa na dalili za ebola majumbani mwao, badala yake wagonjwa husika wapate huduma stahiki hospitali au kituo cha afya," inasema WHO.

Hata hivyo, inasisitiza mazishi ya waliofariki dunia kwa Ebola yafanyike kwa kiwango kikubwa cha kujikinga na mavazi, huku wanaofariki wazikwe mara moja, chini ya usimamizi wa wataalamu wa afya.

WHO inasema, mtu anaweza kuambukizwa kirusi cha ebola, iwapo damu yake au majimaji mwilini yana kirusi hicho, huku ikisisitiza wagonjwa wa ebola wanapaswa kuwa chini ya uangalizi wa hali ya juu kutoka kwa wataalamu na wafanyiwe uchunguzi kuhakikisha kirusi hakipo tena mwilini kabla ya kurejea nyumbani.

Wataalamu wa afya wanabainisha kwamba, wanaume waliopona ugonjwa huo, bado wanaweza kuambukiza kupitia kujamiiana ndani ya wiki saba baada ya kupona, hivyo wanashauriwa kutoshiriki tendo hilo kwa muda tajwa, na iwapo atalazimika, basi atumie kinga.

Wataalamu hao wa afya, wanaeleza wakati wa mlipuko wa ugonjwa huo, walio hatarini kuambukizwa Ebola ni wahudumu wa afya, wanafamilia au watu walio karibu na mgonjwa wa Ebola, waombolezaji wanaoshika maiti ya mgonjwa kama sehemu ya ibada ya mazishi.

### DALILI ZAKE

Wataalamu wanabainisha dalili za Ebola ni: Homa ya ghafla, uchovu uliokithiri, maumivu ya misuli, maumivu kichwa, koo kukauka, ambayo hufuatiwa na kutapika, kuhara, vipele, figo kushindwa kufanya kazi, pamoja na ini, na wakati mwingine damu kuanza kuvunja ndani na nje ya mwili.

"Baada ya dalili hizo kuonekana, ugonjwa unaweza kubainika kati ya siku mbili hadi 21 na hapo ndipo mgonjwa anaweza kuambukiza wengine, na kwamba wakati ugonjwa haujabainika, mtu hawezi kuambukiza mtu mwingine.

AFYA

# Unateswa na mapunye, michirizi sugu, mwasho? Sasa tiba hii hapa

• Majibu ya maswali wanayohoji wagonjwa haya...

**Na Dk. Mussa Zaganza**

SUALA la tiba ya ngozi, huendana na maswali mengi ya wagonjwa kuhusu hali ya mwili wao. Baadhi yanayotawala ni yafuatayo:

SWALI: Nina shida kubwa ya kuwashwa mwilini na hasa baada ya kuoga. Ni tatizo la miaka mingi zaidi ya 20, hata nirudie kujipaka sabuni mara ngapi, hainisaidii.

DAKTARI: Moja ya matatizo ya kiafya yanayowasumbua watu wengi duniani na kuwanyima raha ya maisha, ni tatizo la mwili kuwasha baada ya kuoga.

Muwasho baada ya kuoga, unaweza kujitokeza mwili mzima au unaweza kuhusisha baadhi ya sehemu za mwili. Pia, hali hii inaweza kuendelea kwa muda wa dakika chache au inaweza kuchukua muda mrefu na kwa baadhi ya watu hili linaweza kuwa tatizo sugu.

Ingawa tatizo hili la kiafya ni kama matatizo mengine, lakini baadhi ya watu kwa kukosa taarifa sahihi hulihusisha na imani potofu. Ukweli wa mambo ni kwamba, kuna sababu nyingi zinazochochea kutokea tatizo hili na baadhi hazina madhara makubwa, lakini sababu zingine zinaweza kuwa hatarishi kwa maisha.

Miongoni mwa sababu za kutokea muwasho wa mwili baada ya kuoga, ni za kimazingira na sababu zingine zinahusiana na hitilafu za urithi wa vinasaba vya kijenetiki, katika mfumo wa kinga ya mwili wa mhusika.

Wakati mwingine tatizo hili linaweza kuwa dalili muhimu inayoonyesha baadhi ya magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza kama vile matatizo ya figo, ini, tezi, shingo, matatizo ya mfumo wa damu, kisukari, saratani ya mitoki na msongo wa mawazo.

Baadhi ya tafiti zinabainisha sababu za mazingira, ni pamoja na uchafuzi wa mazingira ya hewa kwa kemikali zenye sumu zinazopatikana katika moshi wa tumbaku na mifuko ya plastiki.

Pia, kuna dawa za kufanyia usafi majumbani, kuua wadudu waharibifu, mabaki ya wadudu, vumbi ndani ya nyumba inayobeba vimelea vya magonjwa, pamoja na uchafuzi wa hewa kama moshi wa magari na ule unaozalishwa na viwanda mijini.

Vitu hivi huufanya mwili kuathirika na kutengeneza mazingira ya ndani ambayo yanachochea kutokea kwa muwasho, pindi mwili unapopata msisimko, hali ambayo hujulikana kama mzio. Muhimu, kapime vipimo hivyo kisha tuwasiliane.

***SWALI: Nini chanzo cha dawa za kuondoa michirizi?***

***DAKTARI:*** Chanzo cha tatizo ni kwenye ngozi ya binadamu ina matabaka matatu, yaani tabaka la juu, tabaka la kati na tabaka la chini. Michirizi ya ngozi huanzia katika tabaka la kati ambalo kimsingi ndilo linaloipatia ngozi uimara na uwezo wa kuvutika.



Hali ya mchirizi kwenye ngozi ilivyo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Mapunye kichwani kwa mtu

> **Utafiti mwingine uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Sayansi za Tiba, Tehran huko Iran nao ulionyesha kuwa kuchua misuli kwa mafuta ya mizeituni wakati wa ujauzito, hupunguza uwezekano wa kupata michirizi ya ngozi.**

Sehemu hii ya ngozi inapovutika kupita kiasi ndani ya kipindi kifupi na ikaendelea kuwa katika hali hiyo, ngozi huvimba na kusababisha kuchanika kwa nyuzi za ngozi ziitwazo 'collagen'. Hali hii, pia husababisha upungufu wa 'elastin' na 'fibronectin' vitu ambavyo huifanya ngozi kuwa imara na kuvutika kwa urahisi.

Hali hii kwa wanawake hujitokeza zaidi wakati wa ujauzito kiasi kwamba asilimia 90 ya wanawake wajawazito hupata tatizo hili kwa ukubwa unaotofautiana.

Jinsi ya kukabiliana nalo; njia ya kwanza ya kukabiliana na tatizo hili, ni kuzingatia kanuni bora za lishe pamoja na kunywa maji ya kutosha kila siku. Ni vizuri kula chakula chenye madini ya kutosha ya zinki na aina mbalimbali za vitamin, ili kuimarisha afya ya ngozi.

Njia nyingine inayosaidia kukabiliana na tatizo hili ni kuchua misuli kila mara, ili kuongeza kiasi cha damu. Utafiti uliofanyika nchini Uturuki mwaka 2012, unaonyesha kuwa wanawake wanaochua misuli kwa angalau dakika 15 kwa kutumia mafuta ya mlozi wanapunguza uwezekano wa kupata michirizi ya ngozi.

Tuwasiliane kama tatizo linaendelea.

Utafiti mwingine uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Sayansi za Tiba, Tehran huko Iran nao ulionyesha kuwa kuchua misuli kwa mafuta ya mizeituni wakati wa ujauzito, hupunguza uwezekano wa kupata michirizi ya ngozi.

***SWALI: Punye ni ugonjwa wa ngozi, 'Tinea Capitis' au nini?***

***DAKTARI:*** Aina hii ya maradhi ya fangasi hushambulia eneo la kichwa pekee ukiacha eneo la uso. Kwa maneno mengine, aina hii ya fangasi haishambulii uso bali hushambulia eneo lililobaki la kichwa.

Huwashambulia kina nani?... Haya hushambulia watu wote wa jinsia na umri wote, ingawa huonekana zaidi kwa watoto wadogo.

Fangasi hawa hushambulia watoto wadogo ambao hawajafikia umri wa balehe na mara nyingi huacha kushambulia pale mtoto anapofikia umri huo wa balehe.

Mwonekano wake; Mapunye huweza kushambulia eneo lote la kichwa au sehemu tu ya kichwa. Eneo la ngozi ambalo lina mashambulizi ya mapunye huwa na umbo linalofanana na sarafu.

Eneo hili la ngozi lililoathirika kama lina nywele, basi hunyonyoka, hivyo mwonekano wa mfano wa sarafu huonekana vizuri tu hata bila kutumia jicho la kitaalam.

Dalili zake; Ukiachilia mbali mwonekano wa mapunye kama nilivyoeleza hapo juu kuna dalili nyingine za maradhi haya. Hizo ni:

* Eneo la ngozi lililoshambuliwa kuwasha (ingawa si mara zote)

* Kubadilika kwa rangi ya ngozi ya eneo lenye maambukizi

*Ukitazama kwa makini eneo ambalo lina mashambulizi ya maradhi haya utagundua kuna vidoti vyeusi ambavyo vinaonyesha eneo ambalo nywele imeng`oka kutokana na maradhi.

*Ngozi kubanduka kwenye eneo lenye maambukizi

*Ngozi kukauka kwenye eneo lenye maambukizi.

*Mara nyingine usaha pia huweza kuonekana kwenye eneo la ngozi lililoshambuliwa na fangasi hawa (hii kwa kitaalam huitwa kerions)

*Kama maradhi haya yakikaa bila kutibiwa kwa muda mrefu, husababisha dalili nyingine kuonekana kama kutoka kwa maji maji kwenye eneo la ngozi lililoathirika pamoja na kutoka kwa harufu mbaya kwenye eneo la ngozi lililoathiriwa na vimelea hivi vya fangasi.

**JARIBU DAWA HIZI**

Kwanza, Ndimu au limau: Kabla kwenda kukoga Msugue limau ndani ya kichwa na baadae yale maganda ya limau yatie katika maji ya kukoga, yaani yawe maji ya uvuguvugu halafu ukoshe kwa maji yale kwanza na baadae utumie maji yaliyo safi.

Pili, 'Fenugreek' kwa lugha ya kiswahili inaitwa Uwatu. Uwatu. Unachukua vijiko viwili vya chai vya Uwatu unazilowesha katika maji usiku mzima ili zipate kulainika, halafu unaziponda ponda na baadae unapakaa ndani ya kichwa na uache kwa muda wa saa moja na baadae zikoshe. Ikiwa utafanya hivi siku zote, mba wataondoka.

Tatu, Mshubiri Mwitu au Aloe Vera kwa jina lingine. Iponde na kisha upake kichwani kila siku, mara mbili asubuhi na usiku.

Nne, kuna udongo tuliouvumbua hivi karibuni wa 'natural clay'. Tumia dawa mojawapo sio zote, tafadhali kisha utupe mrejesho.

***• Mwandishi ni mtaalamu bingwa wa nywele na ngozi, anapatikana katika taasisi ya Natural Skin Solution na kazi hizo zinapatikana bure kupitia njia ya mtandao 'Online Skin Solution'. Simu yake ni + 255 713 039876.***

AFYA

## WIKI YA KICHAA CHA MBWA

# Ilivyo hatari ya kichaa cha mbwa, mbinu za kujihami 'hakuna tiba'

**Na Idda Mushi,** Morogoro



MBWA ni mnyama muhimu katika maisha ya binadamu, akisaidia usalama, mapambo ya nyumba, kufanya mazoezi, kuburudisha na kuwa sehemu ya marafiki katika maisha ya binadamu.

Kumtunza mbwa ni jambo la msingi, ili mbwa awe na afya njema anavyohitaji binadamu, mahitaji ya malazi mazuri, mafunzo, chakula, tiba na chanjo, kumdhibiti dhidi ya magonjwa ni muhimu.

Kichaa cha mbwa ni ugonjwa unaoenea kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu. Umekuwa ukisababishwa na virusi aina ya RNA na nchini, ndiye mwenezaji mkuu wa ugonjwa huo kwa binadamu na wanyama wengine kama ng'ombe na wale wa porini. Hadi sasa hauna tiba, bali unakingwa kwa chanjo na kuzingatia ufugaji bora.

Ugonjwa huo umekuwa ukienezwa kwa njia ya mate kutoka ya mnyama aliyeathiriwa, pia hewa au kupandikizwa kiungo cha mwili kama figo kutoka kwa mtu mwenye maambukizi ya kichaa cha mbwa. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine inachukua hatua kuukabili na Profesa Hezron Nonga, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anataja jitihada hizo ni kutoa chanjo.

Anasema mwaka 2020/2021 walitoa dozi kwa mbwa 986,195 na paka 5,152, wakati mwaka 2021/2022 waliongeza idadi kwa kuchanja mbwa 1,608,244 na paka 6,833.

Pia, kuanzia mwaka wa fedha uliopo sasa, kati ya Julai hadi mwezi huu, anasema wamechanja mbwa 323,638 na paka 28,933 kwenye halmashauri 101 nchini, huku katika Wiki ya Maadhimisho ya Kichaa cha mbwa duniani; Septemba 26 hadi Oktoba 02 ya kila mwaka, wanakusudia kuchanja mbwa na paka 60,000.

Anataja dalili kuu ya ugonjwa ni mbwa au mnyama mwingine anabadilika tabia, ama kuwa mkali au mpole zaidi,

Pia, anakosa hofu yake ya kawaida kwa binadamu, anashindwa kula, kukwepa maji na anapooza miguu ya nyuma, anadondosha mate mengi, ulimi kuning'inia nje, anabweka kila mara, anatoa mlio usio kawaida.

Anataja mazingira hatarishi ya kupata ugonjwa huo ni uwepo wa mbwa wanaozurura mitaani, kukaa karibu na maeneo ya hifadhi za wanyamapori, kuchokoza au kumchezea na ambaye hajachanjwa maradhi hayo.

**NAMNA INAVYOMFIKA**

Profesa Nonga anasema baada ya maambukizi, mgonjwa anachukua muda mfupi, anahisi dalili au wakati mwingine zinachelewa, kati ya mwezi mmoja na mitatu.

> **Epuka kuwa katika mazingira ya kung'atwa na mbwa na endapo umeng'atwa, osha jeraha kwa sabuni na maji mengi yanayotiririka kwa dakika 15, na kidonda kisifungwe, kisha nenda haraka kwenye kituo cha kutoa huduma za afya.**

Wataalamu wanasema kwa binadamu, ugonjwa huo unashambulia mwili haraka sana, anaanza kuwa na dalili zisizo za kawaida kama uchovu, homa, kuharisha, kutapika na pindi virusi wakianza kushambulia mfumo wa neva, huanza kuonekana kuwa mwenye wasiwasi mwingi, mgomvi, analegea sana, kupooza, anavimba ubongo akishindwa kumeza maji.

Tatizo hili linadaiwa kusababishwa na kukaza misuli ya shingo na mgonjwa anaanza kuogopa maji, anapata degedege na anafikia hatua ya kifo.

Inatajwa wastani wa wagonjwa wote hufa kati ya saba hadi 14, tangu kuambukizwa.

**KATIBU MKUU MIFUGO**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulika na Mifugo, Tixon Nzunda, anasema kaulimbiu ya mwaka huu ni "Kichaa cha Mbwa, Afya Moja, Vifo Sifuri" na mgeni rasmi kwenye kilele jijini Dodoma, anatarajiwa kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki.

Nzunda anasema, ni maadhimisho yanayofanyika katika vituo vyote vya kutoa huduma za mifugo nchini, wakichanjwa bure mbwa na paka na huduma inaendelea hadi kilele cha maadhimisho.

"Epuka kuwa katika mazingira ya kung'atwa na mbwa na endapo umeng'atwa, osha jeraha kwa sabuni na maji mengi yanayotiririka kwa dakika 15, na kidonda kisifungwe, kisha nenda haraka kwenye kituo cha kutoa huduma za afya," anasema Katibu Mkuu Nzunda.



Profesa Hezron Nonga, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**WAFUGAJI**

"Mimi nafuga mbwa lakini kwakweli sijawahi kumpa chanjo yeyote, nampenda mbwa wangu, nikitoka nikipata mifupa namletea, usiku na mchana namuacha analinda hapa nyumbani, hata nikiwa sipo hakuna mtu anasogea kwangu, lazima abweke na mtu aogope kusogea jirani," anatamka Sauli Daudi, mkazi wa Vibandani, kata ya Mbuyuni, mjini Morogoro.

Mkazi mwingine wa Kilakala, Morogoro, Jumanne Kilegu, anasema anafuga mbwa na kumpeleka kwenye josho kumsafisha, kumpa chakula kila jioni na kumfunga, akizingatia chanjo na tiba pindi anapohisi au kugundua ni mgonjwa.

"Mbegu hii nimepata kwa rafiki yangu mmoja anaishi Dar es salaam, lakini ni huyu dume ni chotara, ni Germany Shepherd, ni mkali sana, anaweza kubadilika kutokana na hali atakayokuwa nayo," anasema Jasper Malya , mkazi wa Bondwa Kasanga, Kata ya Mindu, mjini Morogoro.

**MBWA WA NCHINI**

Prof. Nonga, anaendelea kusema kuwa zaidi ya asilimia 98 ya mbwa wanaofugwa nchini ni asili (mongrel) na wachache wa kisasa hufugwa mjini.

Anabainisha, tahadhari stahiki inapoamuliwa, ikiwemo kuhakikisha mbwa anafungiwa kwenye banda au mnyororo muda wote wa mchana na kwa mbwa wanaotumika kwa kazi za kuchunga mifugo au kuwinda, ni vema wakawa chini ya uangalizi wa mwenye mbwa ili wasidhuru watu wengine.

Anasema, hadi sasa, serikali imeshaandaa kanuni za chanjo na uchanjaji ya mwaka 2020, ambazo zinamlazimisha kila mfugaji kuchanja mbwa wake dhidi ya kichaa cha mbwa.

**KINACHOENDELEA MOROGORO**

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, hadi sasa nayo inachukua hatua katika maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani, ikishirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, pia Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), kwa kuelimisha wananchi madhara ya ugonjwa huo kwa binadamu.

Akinukuu taarifa ya Shirika la Afya Duniani WHO, Ofisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Manispaa ya Morogoro Dk. Tito Kagize, anasema kila mwaka takribani watu 1,500 hufariki dunia kwa kichaa cha mbwa.

Anasema, takwimu zinaonesha kadri mbwa wengi wanavyochanjwa, ndivyo maambukizi na vifo kwa wanadamu kutokana na ugonjwa huo vinapungua.

Dk. Kagize anarejea Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, kwamba idadi ya mbwa wanaofugwa katika familia zilikohesabiwa ni 10,800, lakini kuna wengime zaidi hawafugwi kwa kuzingatia sheria na kanuni za ufugaji mbwa hao, hivyo kuhatarisha afya ya jamii.

Kuhusu uchanjaji mbwa, anasema kwa Manispaa ya Morogoro, bado hali sio nzuri sana, kwa sababu mwamko uko duni.

"Takwimu zinaonesha kuwa tunachanja mbwa chini ya asilimia 75 ya idadi ya mbwa waliopo, kiasi ambacho kikifikiwa ndio kinga ya mbwa inakuwa imefikiwa.

"Kwa mwaka 2021/2022, idadi ya mbwa waliochanjwa ilifikia 5,886 sawa na asilimia 55 ya mbwa wanaofugwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro,"anaelezea ofisa huyo.

Hapo anasisitiza kwamba, kichaa cha mbwa ni hatari sana kwao, hivyo kila mmoja anapaswa kuchukua tahadhari kujilinda.

AFYA

## KUKITHIRI MATUKIO YA UNAJISI WA MTOTO...

# Imefika zama za kumpa ulinzi mkali kiafya, hadi nafsi yake



Kundi la wanafunzi wa umri mdogo, mbao kimsingi wanahitaji ulinzi mkubwa wa jamii. **PICHA: MAKTABA**

**Na Beatrice Moses**

"Masudi amekuwa jambazi ukikutana naye ukimbie mbali kama sivyo atakudhuru ...." ni wimbo ulioimbwa na nguli nchini, Marijan Rajab, sasa ni marehemu.

Nimejikuta nakumbuka wimbo, kwa sababu baada ya kuusikia ulinijaza hofu, hasa kwa kuwa nilikuwa na umri mdogo wakati huo, sikuwa na uwezo wa kupambanua vyema ujumbe .

Nilipata wakati mgumu nilipokuwa natembea kuenda shule au narejea nyumbani, nililazimika kuhakikisha naongozana na wenzangu na hatua hiyo pekee ndiyo ilikuwa inanipa amani, japo shule haikuwa mbali na kambi za jeshi tulizokuwa tunaishi.

Kikubwa hasa kilichonipa hofu, ni kwamba sikumfahamu Masudi aliyeimbwa ni nani, hivyo mtu ambaye simfahamu nilimhisi huenda ndiyo Masudi aliyeimbwa.

Nakumbuka kuna wakati nilipotumwa nililazimika kutimua mbio huku, nikiwa na tahadhari hasa ninapomuona nisiyemfahamu.

Nimekumbuka hayo kutokana na matukio ya vitendo vya kikatili vinavyoendelea kuripotiwa na vyombo vya habari, ni wazi wasanii wana kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha wanatengeneza kazi za nyimbo au tamthilia za kuelimisha hasa watoto jinsi

> "Ni aina ya magumu yanayotokea hata katika siku za karibuni ikiwamo wiki hii, kukiwepo mwendelezo wa ripoti za matukio ya namna hiyo ya mauaji na udhalilishaji kijamii.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo.

gani wanaweza kuishi kwa tahadhari kwa kuwa mbakaji hajulikani kwa sura yake.

Mnamo Juni mwaka huu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria , Mary Makondo, alitoa wito kwa jamii kuwa mstari wa mbele kupinga unyanyasaji na ukatili kijinsia dhidi ya watoto.

Makondo akakaririwa na vyombo vya habari, ikiwamo tovuti ya wizara anayotumikia, ikiwa na andiko linalobainisha wito huo, katika uzinduzi wa Kampeni ya Siku 10 za Kupinga Ukatili Dhidi ya Watoto, Juni 6, 2022, jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa Takwimu za Jeshi la Polisi Tanzania, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka jana, kuna jumla ya matukio 11,499 ya ukatili dhidi ya watoto yalitolewa taarifa katika vituo vya Polisi.

### JICHO LA POLISI

Taarifa hiyo inataja mikoa iliyoongoza idadi ya matukio kwenye mabano kuwa ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na Mkoa wa Kipolisi Ilala (489).

Hata hivyo, ripoti ubakaji inatajwa kuongezeka kitaifa hata kufika 5,899, mimba kwa wanafunzi 1,677 na ulawiti jumla yake 1,114.

Ni aina ya magumu yanayotokea hata katika siku za karibuni ikiwamo wiki hii, kukiwepo mwendelezo wa ripoti za matukio ya namna hiyo ya mauaji na udhalilishaji kijamii.

Anatoa rai kwa, watendaji wote wa serikali katika ngazi mbalimbali pamoja na wadau wa haki za watoto kuungana kupaza sauti kwa pamoja, ili kusaidia kuongeza uelewa wa watu kuhusu haki na ulinzi wa mtoto ambao ni jukumu la jamii nzima.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ni "Tuimarishe Ulinzi wa Mtoto; Tokomeza Ukatili Dhidi yake, Jiandae Kuhesabiwa."

Ni wazi kwamba kwenye kauli hiyo, tayari imetekelezwa kwa ushirikiano wa aina yake, ni vyema sasa yaliyosalia nayo yapewe uzito na kutekelezwa ipasavyo isibaki kuwa, pasipo matendo.

Andiko hilo linamkariri pia Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mohamed Hamis, kwamba tume inapinga na kulaani vitendo vya ukatili kwa watoto kwa kuwa hakuna siku inayopita bila ya vyombo vya habari, kuripoti taarifa za ukatili wanaofanyiwa watoto.

Imebainishwa kwamba, tume imekuwa ikifanya uchunguzi wa malalamiko mbalimbali yanayohusu kuvunjwa haki za watoto na kubaini watoto wengi wanakosa ujasiri wa kutoa taarifa za ukatili wanaokutana nao.

Pia, baadhi yao wamekuwa wakiyumbishwa na wanafamilia wasio wema, hivyo kuficha maovu yanayotendeka katika jamii.

Ni hali inayoendelea, huku kukiendelea ushuhuda wa matukio hata baadhi kuripotiwa kufungwa kwa matukio ya ulawiti, huku kukiwepo taarifa za watoto kufanyiwa vitendo hivyo na watu wa karibu.

Hapo inajenga maana gani? Ni kwamba malezi ya sasa yana changamoto kubwa, hasa kutokana na utandawazi unaohusisha teknolojia, hivyo ni vyema mapambano ya ukatili dhidi ya watoto namna tofauti yaendelee.

Mwanamuziki Marijan alipoimba alisikika redioni, hata luninga zilimilikiwa na baadhi wenye ukwasi, lakini sasa mabadiliko ya luninga za kutosha, vituo vya radio vimeongezeka, simu mkononi na matumizi mitandao ya jamii.

Hivyo, wasanii nao wanatakiwa kutumia vipaji vyao kadri walivyojaliwa kuhakikisha ujumbe wa kuwaelimisha watoto, kuhusu kuepuka mazingira yanayoweza kusababisha kufanyiwa ukatili.





## Uharibifu mazingira wapunguza mvua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya mikoa nchini imeanza kupata mvua chini ya asilimia 50 katika miaka ya karibuni kulinganishwa na miaka 20 iliyopita kutokana na uharibifu wa mazingira.

Vilevile, hali hiyo inatajwa kuathiri shughuli za uzalishaji hasa kilimo na hivyo kusababisha mikoa hiyo kukabiliwa na uhaba wa chakula, jambo linalohitaji jitihada za makusudi kukabiliana nalo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, alibainisha hayo juzi wakati wa makabidhiano ya hati ya makubaliano na vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa urejeshwaji endelevu wa mazingira ya ikolojia katika Bonde la Mto Ruaha na Ziwa Rukwa.

Hati hizo zilikabidhiwa kwa wakurugenzi watendaji wa halmashauri mbili za Mkoa wa Mbeya ambazo ni Mbarali inayotekeleza mradi katika Bonde la Mto Ruaha na Mbeya inayotekeleza mradi katika Bonde la Ziwa Rukwa.

Waziri Jafo alisema hali ya ukame katika baadhi ya maeneo nchini imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli mbalimbali za kibinadamu.

Alisema kuna baadhi ya maeneo nchini miaka 20 iliyopita yalikuwa yanapata mvua juu ya wastani lakini kwa sasa yanapata mvua ya kawaida na yale ambayo yalikuwa yanapata mvua ya wastani kwa sasa yanapata mvua ya chini ya wastani.

"Katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu wakulima wanalima kilimo ambacho siyo cha uhakika kutokana na mabadiliko ya tabianchi, sasa ni lazima tuchukue hatua za ziada kukabiliana na tatizo hili, vinginevyo hali ni mbaya sana," alisema Dk. Jafo alionya.

Mratibu wa mradi huo kitaifa, Damas Mapunda, alisema mradi huo unatekelezwa katika nchi 10 duniani na kwa Tanzania unatekelezwa kwenye mikoa mitano ambayo ni Mbeya, Njombe, Iringa, Rukwa na Katavi.

Alisema gharama za utekelezaji wa mradi huo ni dola za Marekani milioni 11.2 (Sh. bilioni 25.8) ambazo alisema zinatokana na ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Mazingira chini ya Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP).

"Lakini kuna mchango wa nchi ambapo sisi tunachangia dola za Marekani milioni 75.4 na muda wa utekelezaji wa mradi huu ni miaka mitano na ulianza 2021, utakamilika mwaka 2026," alisema.

Mapunda alifafanua kuwa fedha ambazo Serikali ya Tanzania inachangia, zinatolewa na wizara pamoja na halmashauri ambazo zinatekeleza mradi huo.

Baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri za mkoa wa Mbeya ambazo zinatekeleza mradi huo, walisema wamebaini kuwapo vikwazo katika utekelezaji wa mradi huo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbeya, Nicholous Tindwa, alisema moja ya matatizo waliyoyabaini ni uvamizi wa vyanzo vya maji na maeneo oevu ambako baadhi ya wananchi wanafanya shughuli zao za kibinadamu ikiwamo kilimo na ufugaji.

# Mbaroni kwa tuhuma mtandao wizi pikipiki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limeendelea kudhibiti mtandao wa wizi wa pikipiki na mauaji ya waendesha pikipiki za abiria (bodaboda) ndani ya maeneo ya mkoa huo baada ya kunasa baadhi yao.

Juzi Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamini Kuzaga, alisema katika msako waliofanya hivi karibuni waliwakamata watu wawili wanaodaiwa wamekuwa wakijihusisha na wizi wa pikipiki hizo. Kamanda Kuzaga aliwataja watu hao kuwa ni Samwel Mwampangata (27), mkazi wa Ngonga wilayani Kyela na Yona Sabeli (46), mkazi wa Mbegele wilayani humo kwa tuhuma za wizi wa pikipiki mbili.

Alisema watuhumiwa hao kwa nyakati tofauti walikamatwa na walipopekuliwa walikutwa na pikipiki za wizi zenye namba za usajili MC 808 DHR ambayo ilikuwa inatumiwa na Mwampangata.

Alisema walipofuatilia walibaini kuwa mtuhumiwa alikuwa kwenye harakati za kuisafirisha pikipiki hiyo kwenda katika nchi jirani ya Malawi ambako baadhi yao wamekuwa wakiiba na kuzipeleka.

Alisema pikipiki hiyo imeshatambuliwa na mmiliki aitwaye Elieza Mwandagani (18) ambaye ni dereva bodaboda katika eneo la Serengeti wilayani Kyela.

"Lakini Sabeli alikuwa akitafutwa kwa muda mrefu kwa tuhuma za kuvunja stoo na kuiba pikipiki ya serikali yenye namba za usajili STL 8531 aina ya Yamaha ambayo ilikuwa mali ya Mamlaka ya Bonde la Ziwa Nyasa," alisema Kamanda Kuzaga.

"Pikipiki hii alikamatwa nayo akiwa tayari amefungua namba za usajili na kutenganisha baadhi ya vifaa ili kurahisisha kwenda kuiuza mahali ambako tunaendelea kumhoji," alisema.




Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Nyasa, Paul Lugongo (katikati), akizungumza wakati wa uzinduzi wa tawi la BRAC Tanzania Finance Ltd Nyasa, mkoani Ruvuma hivi karibuni. Wengine ni wafanyakazi wa BRAC. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi mila wafanya matambiko kuzuia ajali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa mila katika Mkoa wa Mbeya wamefanya matambiko kwenye miteremko ili kuzuia ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara na kusababisha madhara kwa binadamu na vyombo vya usafiri.

Matabiko hayo yamefanyika kwenye miteremko yote ya Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) na kwenye barabara ambazo zinaingia katikati ya Jiji la Mbeya ikiwamo barabara ya kutoka Chunya na Barabara ya Mbeya-Kasumulu.

Viongozi hao walifanya matambiko hayo juzi ikiwa ni wiki moja baada ya viongozi wa dini kufanya maombi maalum ya kuzuia ajali kwenye maeneo hayo.

Akizungumza baada ya kumaliza matambiko hayo kwenye mteremko wa Mlima Iwambi, Chifu wa Bonde la Mbalizi, Ezelina Mpoli alisema waliamua kufanya matambiko kutokana na kukithiri kwa ajali kwenye maeneo hayo.

Alisema wao wanaamini kwamba baadhi ya ajali hizo zimekuwa zikisababishwa na masuala ya ushirikina unaofanywa na baadhi ya watu wenye imani potofu ambao wamekuwa wakiamini kwamba damu za watu zinaleta utajiri.

Alisema wataendelea kukemea na kufanya matambiko kila mwaka kwenye maeneo yote ya miteremko ili kuhakikisha ajali hizo zinakoma na watu wanaendelea kuishi kwa amani kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

"Hatujaanza leo kufanya matambiko yetu, tulishafanya mwaka jana kwenye mteremko huu wa Mbalizi na tunamshukuru Mungu ajali zimepungua sana kwenye eneo hili, sasa hivi tumekubaliana kwamba tutakuwa tunafanya matambiko kila mwaka badala ya kufanya ajali zikitokea," alisema Chifu Mpoli.

Alisema wameruhusiwa na serikali ya mkoa kufanya matambiko hayo na hivyo wataendelea kushirikiana na serikali kukabiliana na matatizo mengine yanayoukabili mkoa huo.

Chifu wa Kata ya Itende jijini Mbeya, Juma Jojo, alisema barabara zinajengwa na binadamu na vyombo vya moto vinatengenezwa na binadamu na hivyo ajali zinaweza kuzuiliwa na binadamu wenyewe kwa kila mmoja kutekeleza majukumu yake vizuri.

Alisema katika uchunguzi wao walibaini kuwa ajali hizo nyingi siyo za kawaida na zinasababishwa na binadamu wenye imani za kishirikina.

"Kuna ajali zimekuwa zikitokea lakini hatuoni damu, ila watu wanakuwa wameumia na wengine wamekufa, sasa kama ni watu wanasababisha tunaomba waache na kama ni za Mungu, basi tunaomba atusamehe maana inakera watu wanakufa na wengine wanajeruhiwa," alisema Jojo.

Chifu wa Kijiji cha Holongo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Adam Mwazwebha, aliiomba serikali iendelee kuwashirikisha kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo ndani ya mkoa huo.

Alisema viongozi wa mila wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kukemea maovu kwenye jamii pamoja na kulinda mazingira yasiharibiwe na hivyo ni vyema serikali ikaendelea kuwatambua.

Hivi karibuni zilitokea ajali mfululizo katika eneo la mteremko wa Shamwengo zikihusisha magari mbalimbali ambapo zaidi ya watu 30 walipoteza maisha na wengine kujeruhiwa.



## Waziri Ndalichako ataka utambuzi wenye ulemavu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amewaagiza maofisa ustawi wa jamii na maofisa maendeleo ya jamii kufanya utambuzi wa watu wenye ulemavu mapema ili kusaidiwa.

Prof. Ndalichako alitoa maagizo hayo juzi alipokuwa akifungua mafunzo ya mwongozo wa taarifa wa utambuzi wa mapema na afua stahiki kwa watoto wenye ulemavu kwa watendaji hao nchini.

Alisema maofisa hao wanatakiwa kuwatambua mapema ili kusaidia familia husika za watoto hao kupewa elimu ya kuwatunza.

Waziri huyo alisema watoto hao wenye ulemavu wakibainika mapema wakiwa bado wachanga au wadogo, kuna aina za ulemavu zitatibika na kuwaondolea ulemavu mtoto husika.

Alisema wako wazazi wanaowaficha watoto wenye ulemavu nyumbani na kuwanyima haki zao za kimsingi kama elimu na kutoka nje.

Waziri Ndalichako aliwataka kuhakikisha wanakuwa na takwimu za watoto wenye ulemavu kwenye maeneo yao pamoja na kujua aina za ulemavu ili kusaidiwa.

Pia aliwahimiza kuwaunganisha watu wenye ulemavu walioko kwenye maeneo yao na fursa za kiuchumi zinazotolewa na serikali kupitia asilimia 10 ya mapato ya halmashauri.

"Wako wenye ulemavu hawajui kama kuna mikopo inatolewa na serikali hivyo wakipewa elimu itawasaidia kuendeleza kiuchumi na kielimu," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto Wizara ya Afya , Dk. Ahmad Makuwani, alisema wizara hiyo inatambua umuhimu wa kuimarisha mfumo wa utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu katika kuzuia na hata kupunguza athari za ulemavu kwa mtoto katika makuzi yake.




Naibu Waziri wa Kilimo, Athony Mavunde (wa tatu kulia), akifuatilia mada baada ya kuzindua mafunzo ya siku mbili ya kilimo biashara kwa watu wenye ulemavu yaliyoandaliwa na Foundation of Disabilities Hope (FDH) na kudhaminiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), jijini Dodoma jana. Wengine ni Mkurugenzi wa FDH, Martin Kihumbe (kulia), Mkurugenzi wa Uhusiano wa Umma wa SBL, John Wanyancha (wa pili kulia), Mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Neema Kweka (kushoto) na Mkuu wa Divisheni ya Kilimo Mkoa wa Dodoma, Yustina Munishi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wataka mfuko kusaidia watu wenye ulemavu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuharakisha mchakato wa mfuko wa watu wenye ulemavu nchini ili kuwasaidia kupata mikopo elimu ya kati pamoja fursa za kiuchumi.

Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Kitaifa kwa Watu wenye Ulemavu, Dk. Lucas Kija, alitoa ombi hilo wakati wa uzinduzi wa baraza hilo uliofanyika jijini hapo juzi.

Dk. Kija aliomba serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kuharakisha mchakato wa mfuko wa watu wenye ulemavu ambao utawasaidia kupata mikopo ya elimu ya kati.

Alisema kutokana na serikali kutokuwa na mikopo kwa elimu ya kati mfuko huo ukizinduliwa utawasaidia watu wenye ulemavu wanaotaka kujiendeleza kielimu kunufaika.

Kija alibainisha kuwa mfuko huo upo kisheria kwa mujibu wa sheria ya watu wenye ulemavu namba tisa mwaka 2010 kifungu 57 na akaunti yake ilishafunguliwa Benki Kuu (BoT) na Benki ya NMB hivyo wanaomba ofisi ya Waziri Mkuu kuharakisha mchakato wake ili kuanza kufanya kazi.

Kadhalika alitaja faida za kuanzishwa kwa mfuko huo ni kutolewa kwa ruzuku kwa vyama vya wenye ulemavu nchini na kijiendesha.

Mwenyekiti huyo alisema mfuko huo pia utasaidia kufanya utafiti mbalimbali katika kutatua matatizo mbalimbali yanayohusiana na ustawi wa kundi hilo.

Aidha, Dk. Kija alisema mfuko huo utawezesha wenye ulemavu kupata fursa za kiuchumi pamoja na kusaidia matumizi ya kuendesha shughuli za baraza.

Naye Mkurugenzi wa Kitengo cha Watu wenye Ulemavu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Ajira na Wenye Ulemavu, Rashid Maftaa, alisema mapendekezo hayo yameshapokelewa na yanaendelea kufanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria.

Alibainisha faida za mfuko huo ni kuwezesha programu mahsusi za huduma za marekebisho ya ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma za afya.

## Waziri ataka bajeti jumuishi kijinsia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imewataka wakurugenzi wa sera na mipango kutoka wizara mbalimbali na waratibu wa masuala ya jinsia kuhakikisha kuwa bajeti watakazoziandaa zinakuwa za mlengo wa kijinsia.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma wakati akifungua kikao kazi cha kutoa maoni kwenye andiko la rasimu ya hali ya jinsia Tanzania Bara.

Dk. Gwajima aliwataka pia wakurugenzi hao na waratibu kuhakikisha miradi yote ya maendeleo inakuwa na ushiriki sawa kati ya wanawake na wanaume.

"Nawataka wakurugenzi wa sera na mipango na GFP kuhakikisha wanatoa maoni kwa ajili ya kuboresha rasimu yetu ya hali ya jinsia hapa nchini, kuhakikisha sera, mipango na programu za kisekta zinaweka kipaumbele katika masuala ya kijinsia.

"Kuhakikisha GFP wanatoa taarifa ya kila baada ya miezi mitatu kuhusu utekelezaji wa bajeti inayozingatia masuala ya jinsia katika uhalisia wake na kuiwasilisha kwenye wizara yenye dhamana na masuala ya jinsia, kuwe na fomati rasmi ya uwasilishaji taarifa hizo toka kila wizara," alisema.

Aidha, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau muhimu ambao ni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Masuala ya Wanawake (UN- Women) imeandaa rasimu ya hali ya nchi kuhusu jinsia.

"Hivyo ni imani yangu kuwa kila mshiriki atapata nafasi ya kuipitia ili kutoa maoni yatakayowezesha kuboreshwa kwa rasimu yetu ya andiko hili ili kuwa na andiko bora lenye takwimu za uhakika na wawakilishi kutoka katika maeneo na sekta mbalimbali," alisema.

Kadhalika, alisema uwepo wa usawa wa kijinsia katika nyanja zote utasaidia kuweka uhalali wa mipango inayohusu masuala ya kiuchumi na yanayohusu sekta ya elimu hasa katika ushiriki sawa kwenye masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (STEM).

Pia alisema kutasaidia kuwepo na ushiriki sawa katika uongozi na ngazi za maamuzi na usawa katika masuala ya afya bora, kilimo na sekta zingine zote.

"Tanzania kama ilivyo kwa wanachama wa Umoja wa Mataifa, imeridhia na inatekeleza mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda kuhusu kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi.

"Mfano, kupitia Azimio la Ulingo wa Beijing mwaka 1995, Tanzania iliamua kujikita katika maeneo manne ya kipaumbele ambayo ni kuwawezesha wanawake kiuchumi, wanawake na haki za kisheria, usawa katika elimu, mafunzo na ajira na wanawake katika nafasi za uongozi na ngazi za uamuzi," alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Amon Mpanju, alisema lengo la kikao kazi hicho cha siku moja ni washiriki kutoa maoni yao ambayo yatasaidia kuboresha rasimu hiyo.

Hata hivyo, alisema andiko hilo litakuwa nyenzo katika masuala ya kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi.

# ZECO kutumia bil. 174/- kutoa huduma ya umeme

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Umeme Zanzibar (ZECO) linatarajia kutumia Sh. bilioni 174.52 kutekeleza majukumu yake mwaka huu wa fedha, ikiwamo ununuzi wa umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), sawa na ongezeko la asilimia 2.9 kulinganishwa na bajeti yake ya mwaka uliopita.

Meneja Mkuu wa Shirika hilo, Mshenga Haidar Mshenga, alibainisha hayo jana ofisini kwake mjini Zanzibar, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mwelekeo wa shirika kwa mwaka wa fedha 2022/23 na mafanikio kwa mwaka 2021/22.

Alisema fedha hizo zitatumika katika ununuzi wa umeme kutoka TANESCO, usambazaji na ujenzi wa miundombinu ya umeme, uendeshaji wa shirika na matumizi mengine.

Alisema kuwa katika kutimiza dhamira ya kusambaza huduma za umeme ili kukidhi mahitaji ya taifa katika hali ya ubora na usalama, shirika limepanga kuongeza ufanisi na ukusanyaji wa mapato, kupunguza upotevu wa umeme na kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa huduma ya umeme.

Meneja huyo alisema katika majukumu ya kuwaunganishia huduma ya umeme wananchi kwa wakati, shirika limeshaingiza vifaa vya kutosha zikiwamo nyaya, nguzo, mita na vifaa vingine ili kumaliza tatizo la kusubiri huduma kwa muda mrefu.

Alisema ZECO ina utaratibu wa kutenga fedha kupitia bajeti yake ya kila mwaka kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini, kwa mwaka wa fedha 2022/23 imekusudia kupeleka umeme katika vijiji 42 kwa Unguja na Pemba.

Akizungumzia tatizo la umeme mdogo, meneja huyo alisema katika kuimarisha huduma hiyo, watafanya maboresho ya maeneo 69 ya Unguja na 30 ya Pemba, ili kuondoa tatizo la transfoma kuzidiwa, pia uchakavu wa miundombinu ya umeme.

Alisema Serikali ya Zanzibar imepata mkopo wa dola milioni 142 kutoka Benki ya Dunia ambazo zitazalisha umeme wa jua katika Kijiji cha Makunduchi, ujenzi wa vituo vya kupozea na kusafisha umeme Welezo, Matemwe na kuboresha umeme zaidi ya nyumba 80,000.

Alisema mbali na maboresho yanayofanywa kupitia ZECO, kuna mradi wa Uimarishaji Sekta ya Nishati na Upatikanaji wa Huduma ya Umeme Zanzibar (ZESTA) wa miaka sita, sasa upo katika hatua ya kufanyiwa tathmini.

Akizungumzia mafanikio ya ZECO kwa mwaka 2021/22, meneja huyo alisema wamefanikiwa kupeleka umeme visiwa vidogo vyote vyenye makazi ya watu ikiwamo Kokota na Njau Kaskazini, Pemba.

Meneja huyo alisema shirika linakabiliwa na shida ya malimbikizo ya madeni kwa taasisi za serikali na taasisi binafsi, wizi na hujuma za umeme ambapo wateja 64 walikutwa na makosa hayo kwa mwaka 2021/22 na kuwataka wananchi kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa miradi ya umeme ili miradi ikamilike.

Ofisa Habari wa shirika hilo, Haji Omar Chapa, alisema kuchelewa kupatikana kwa huduma ya umeme kwa baadhi ya maeneo ni kutokana na idadi ya wananchi wanaotaka huduma ya umeme kuwa kubwa.

Alisema ZECO imeboresha kituo cha kupokea taarifa kwa asilimia 50 kwa kuweka mifumo mipya ya mawasiliano ili kutatua matatizo kwa haraka.



Naibu Waziri wa Miundombinu, Usafirishaji na Mawasiliano Zanzibar, Nadil Abdullatif (kushoto), akijadiliana jambo na Mwakilishi wa Viti Maalum, Shadia Muhammed Suleiman, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wananchi 2,300 wadai mabilioni benki iliyozuiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema kufuatia Benki ya FMBE kuwekwa chini ya ufilisi na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) tangu Mei mwaka 2017, Wazanzibar 2,297 wameathirika na uamuzi huo wakiwa wanadai fedha zao Sh. bilioni 22.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya, alibainisha hayo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, alipojibu hoja za wajumbe wa baraza hilo waliochangia taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu hali ya uchumi. Hoja ya hatima ya wananchi walioweka fedha zao katika benki hiyo iliibuka wakati wa mjadala huo na serikali kutakiwa kutoa ufafanuzi wa kina.

Waziri Saada alisema serikali inafuatilia kwa karibu suala la fedha za wananchi walizoweka katika benki hiyo ambazo ni nyingi japo suala hilo limechukua muda mrefu pasi na wananchi kupata haki zao. Alisema Benki ya FBME iliwekwa chini ya ufilisi na BoT mwaka 2017 kwa kuzingatia kifungu cha 61 (1) na 41 (a) cha sheria iliyoanzisha taasisi hiyo ya kusimamia sekta ya fedha nchini.

Alizitaja hatua zilizochukuliwa mara baada ya ufilisi huo zinajumuisha BOT iliiteua Bodi ya Bima ya Amana kwa ajili ya kufuatilia na kuwalipa wateja walioweka fedha zao katika benki hiyo.

Waziri huyo alizitaja hatua zingine ni kuundwa kwa kamati kufuatilia suala hilo na kulimaliza nje ya mahakama kwa ajili ya kuharakisha malipo.

Alisema wamiliki wa benki hiyo ambao wapo Cyprus, wanakabiliwa na kesi nyingi ambazo zimefunguliwa na watu na kampuni mbalimbali na ndiyo sababu ya kuchukua muda mrefu kukamilisha malipo kwa wananchi.

"Sisi tumeanza kulifuatilia suala hili kwa kuunda kamati ambapo tunataka kulimaliza nje ya mahakama... hawa wamiliki wana kesi zipatazo 67," alisema.

Waziri huyo aliwataka wananchi walioweka fedha zao katika benki iliyofilisiwa, kuendelea kuwa na subira huku serikali ikilifuatilia suala hilo kwa karibu kujua hatima yake.

"Serikali inafahamu maumivu wanayoyapata wananchi walioweka fedha zao katika benki hiyo ambazo ni nyingi, Sh. bilioni 22 ni fedha nyingi ambazo wananchi wanazihitaji kwa matumizi mbalimbali," alisema.

Akiwasilisha ripoti ya Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Sabiha Filfil Thani, aliitaka serikali kulifuatilia suala hilo kwa kuwa waathirika wake wengi ni wafanyabiashara.

Aliitaka serikali kuja na msimamo madhubuti kuhusu suala hilo kwa kuwa baadhi ya matapeli wanautumia mwanya huo kuwadanganya wananchi walioathirika na tatizo hilo.

## Wizara yakiri tishio ukataji wa mikoko

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesema ukataji wa mikoko umefikia asilimia 70 huku ukiwa tishio kwa mabadiliko ya tabianchi na athari za kimazingira.

Waziri wake, Shamata Shaame Khamis alikiri kuwapo tishio hilo alipojibu swali la Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar, aliyetaka kujua mikakati ya wizara kukabiliana na kasi ya ukataji wa mikoko na athari zake.

Shamata alikiri kuwapo kasi ya ukataji wa mikoko ambayo kwa Kisiwa cha Pemba ipo kwa asilimia 70 huku Unguja ipo kwa asilimia 20.

Alisema serikali inalifahamu tishio la kutoweka kwa mikoko kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya kuni na ujenzi wa nyumba za makazi.

Alisema kuwa kwa mujibu wa Sheria za Hifadhi ya Misitu ya Taifa, mikoko haitakiwi kukatwa kwa matumizi ya kuni na imeingizwa katika miti ya hifadhi ya mazingira.


Alisema kitendo cha wananchi kukata mikoko kwa wingi katika maeneo ya fukwe ni kukaribisha maji ya bahari kuingia hadi kwenye makazi ya wananchi na kusababisha athari kubwa.

"Vipo baadhi ya visiwa vidogo Pemba wananchi wameanza kuvihama kutokana na kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya makazi ambayo imesababishwa na wananchi kukata mikoko," alisema.

Aliitaja mikakati inayochukuliwa na wizara kwa sasa ni kutoa elimu kwa wananchi kuotesha kwa wingi mikoko katika maeneo ya pembezoni mwa fukwe ili kuzuia athari za mmomonyoko wa ardhi.

Alisema mikoko ni maarufu kwa kuzuia kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya fukwe na makazi ya wananchi huku ikihifadhi baionuai nyingi za viumbe vya baharini.

"Tumewataka wananchi mmoja mmoja pamoja na vikundi kuja kuchukua miche ya mikoko na kuiotesha pembezoni mwa bahari, hatua ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia kasi ya maji ya bahari," alisema.





# Madiwani waagiza watumishi walipwe

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATUMISHI wa serikali na wazabuni wanaidai Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga Sh. milioni 671.5 zinazotokana na madeni.

Kati ya fedha hizo, Sh. milioni 669.7 ni madeni ya watumishi wa manispaa hiyo na Sh. milioni 1.8 ni kwa ajili ya malipo ya wazabuni waliotoa huduma mbalimbali.

Hayo yalibainishwa juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha kujadili taarifa ya hesabu za mwisho za halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/22 ulioishia Juni 30, 2022.

Katika taarifa hiyo, madiwani hao walieleza kusikitishwa kuona madeni ya watumishi ambayo wanadai kwa kipindi kirefu Sh. milioni 669.7 pamoja na wazabuni Sh. milioni 1.8 ambao hutoa huduma mbalimbali kwenye halmashauri hiyo.

Diwani wa Masekelo, Peter Koliba, alisema siyo vyema watumishi wa halmashauri hiyo kuendelea kudai madeni yao kwa kipindi kirefu bila kulipwa, hivyo uangaliwe utaratibu wa kuwalipa.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, pia alizungumzia suala hilo la malipo kwa watumishi na wazabuni na kuagiza kila idara iangalie madeni ambayo wanadaiwa na watumishi wake na kuanza kuyapunguza.

Jasinta pia aliwataka madiwani na watumishi wa halmashauri hiyo kuendelea na kasi ya ukusanyaji mapato ya ndani kama ilivyo sasa huku akisisitiza kutumia lugha nzuri wakati wa kufanya kazi hiyo.

Mkuu wa wilaya alihimiza usimamizi wa fedha za miradi ya maendeleo ili itekelezwe kwa ubora.

Katika hatua nyingine, Manispaa ya Shinyanga imetoa Sh. milioni 156.4 kwa vikundi 11 vya ujasiriamali vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia utaratibu wa kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuwezesha mikopo kwa makundi maalum.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, John Tesha, akizungumza juzi kwenye hafla fupi ya kukabidhi fedha za mikopo kwa vikundi hivyo, alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22 halmashauri hiyo ilitoa mikopo ya Sh. milioni 379 kwa vikundi 21.

"Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga tumekuwa tukitoa fedha nyingi za mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia asilimia 10 za mapato ya ndani na kati ya mwaka 2015 hadi 2022 tumeshatoa jumla Sh. bilioni 1.4 kwa vikundi 170," alisema Tesha.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, alivitaka vikundi hivyo kurejesha mikopo hiyo kama taratibu zinavyotaka ili kutoa fursa kwa vikundi vingine na kukopa.

# Wanafunzi hatarini kukosa madawati 6,000 sekondari

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI wanaotarajiwa kuhitimu darasa la saba mwaka huu katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wako hatarini kukosa madawati kutokana na kuwapo kwa upungufu wa samani hizo 6,000 katika shule za sekondari.

Hiyo inatokana na makadirio ya kuwa na ufaulu wa asilimia 85 kwa wanafunzi hao katika mtihani huo, halmashauri hiyo inatarajia kupokea wanafunzi 9,870 wa kidato cha kwanza mwakani huku wanaohitimu kidato cha nne mwaka huu katika sekondari mbalimbali wakiwa 3,082.

Ofisa Elimu wa Sekondari wa Manispaa hiyo, Anastazia Manumbu, alibainisha hayo juzi wakati wa hafla ya kukabidhi viti na meza 62 kwa ajili ya wanafunzi vilivyotolewa na Benki ya CRDB Kanda ya Magharibi.

Viti hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni tano vilikabidhiwa kwa Shule ya Sekondari Mama Samia iliyoko Kata ya Majengo wilayani Kahama.

Alisema kwa sasa hawana upungufu wowote wa viti na meza katika shule zote za serikali, lakini ifikapo mwakani watapokea wanafunzi wapya 9,870 na watakuwa na upungufu wa viti na meza 6,000 na kuwaomba wadau wa elimu kuungana na serikali kutatua tatizo hilo pale watakapohitajika. Mkuu wa Shule hiyo, Joyce Jewe, alisema ilianza kutoa huduma mwaka jana ikiwa na viti na meza 360 na wanafunzi 227 na kwa jumla ya wanafunzi 547 (wavulana 284).

Alisema shule hiyo ina walimu 19 na kati ya hao, 15 ni wameajiriwa na serikali na wanne ni wa kujitolea ambao wanapewa posho na kutokana na mchango wa wananchi.

Akikabidhi vifaa hivyo, Meneja wa CRDB Kanda ya Magharibi, Jumanne Wagana, alisema wamekuwa wakishirikana na serikali kutatua shida mbalimbali katika sekta ya elimu na mwaka juzi walitoa viti na meza 100 katika Sekondari ya Kitwana.

Alisema lengo la kutoa viti na meza hizo ni kuboresha miundombinu ya wanafunzi ili wasome katika mazingira rafiki.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, alipongeza benki hiyo kwa kuwa mstari wa mbele kujitoa na kusaidia sekta ya elimu.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12, mwaka huu, inabainisha kuwa katika halmashauri 77 zilizokaguliwa, kuna uhaba wa vyumba vya madarasa 74,735, nyumba za walimu 73,135, ofisi za walimu 5,112, viti 65,889, meza 185,840 na matundu ya vyoo 111,931, akipendekeza serikali ichukue hatua za haraka kuboresha miundombinu iliyopo na kujenga mipya.




Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (mwenye miwani), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 156.4 kwa vikundi 11 vya ujasiriamali vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kupitia asilimia 10 za fedha za mapato ya ndani ya halmashauri juzi, ili wapate mitaji na kufanya shughuli za maendeleo na kujikwamua kiuchumi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mlipuko wa nguzo za umeme wazua taharuki

**Elizabert Seleman,** SENGEREMA

WANANCHI wa Kijiji cha Luchili katika Halmashauri ya Buchosa wamekumbwa na taharuki kutokana na nguzo za umeme kulipuka wilayani Sengerema mkoani Mwanza baada ya lori kugusa nyaya za umeme.

Taharuki hiyo ilitokea jana kwa wananchi hao, huku Msimamizi wa Ufundi wa Shirika la Umeme (TANESCO) wilayani Sengerema, Photunatus Magai, akitoa ufafanuzi kuhusu tukio hilo.

Msimamizi huyo alisema dereva wa gari hilo alikuwa akiendesha gari pasi na umakini na kusababisha kugusa nyaya za umeme kulikosababisha nguzo tano kuanguka na kulipuka. Alisema hakuna madhara ya kiafya yaliyotokea na tayari TANESCO imeanza kurejesha huduma hiyo kwa wananchi wa kijiji hicho na maeneo mengine ambayo yameathiriwa na tukio hilo.

Wakizungumzia tukio hilo, baadhi ya wakazi wa kijiji hicho walisema gari ambalo lilikuwa likisomba udongo maalum kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Luchili-Nyanzenda, liligusa nyaya za umeme na kusababisha mlipuko wa moto kwenye nguzo tano.

Wananchi hao walisema moto huo ulitokea kutokana na walichokiona kama uzembe wa dereva kwa kuendesha gari bila kuwa tahadhari na hivyo kugusa nyaya hizo.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Neema William alisema hakuna madhara ambayo yalitokea kwa wananchi na kuwataka madereva wawe makini wanapokuwa barabarani.

HABARI

# Ukraine, Marekani, NATO zalaani kura ya Russia

**KYIV,** Ukraine

UPIGAJI kura unaotajwa kama maoni ya kuamua majimbo ya Ukraine yanayoshikiliwa kujiunga na Russia umemalizika, huku maofisa wanaoiunga mkono Moscow wakisema mikoa yote minne imeamua kujiunga na nchi hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na DW, kura hiyo ilipigwa kwenye mikoa ya Donetsk na Luhansk kwa upande wa mashariki na Kherson na Zaporizhzhia kusini.

Kwa mujibu wa maofisa waliowekwa na Moscow, asilimia 99 ya wapigakura waliojitokeza katika jimbo la Donetsk, 98 Luhansk, 93 Zaporizhzhia na 87 katika jimbo la Kherson wakidai kuwa wametaka kujiunga na Russia.

**Mataifa 27 wanachama wa EU yanatafakari vikwazo vipya dhidi ya Urusi kwa kuandaa kura hizo tata.**

Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Marekani, Antony Blinken, alisema mataifa ya Magharibi hayatatambua kura hiyo, na kwamba Marekani itaungana na Albania kuwasilisha azimio la kulaani kura hiyo katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UN).

Balozi wa Marekani kwenye Umoja huo, Linda Thomas-Greenfield, alisema kura hiyo inaweza kufunguwa njia kwa mambo mengine makubwa na mabaya zaidi. Huku Katibu Mkuu wa Muungano wa Kijeshi wa NATO, Jens Stoltenberg, akisema kura hiyo haina uhalali.

**ZELENSKY ATOA NENO**

Akihutubia taifa hilo baada ya matokeo hayo kutangazwa Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alidai kuwa wakazi wa majimbo hayo walilazimishwa kupiga kura chini ya mtutu wa bunduki na kwamba watalazimishwa pia kupigana vita dhidi ya Ukraine, huku akiapa kuilinda mipaka ya nchi yake.

"Tutawalinda watu wetu wa Kherson, Zaporizhzhia, Donbas, Kharkiv na Crimea, kituko kilichofanywa kwenye maeneo hayo yanayokaliwa hakiwezi hata kuitwa igizo la kura ya maoni. Tulijuwa tangu mwanzo yapi yatakayokuwa matokeo yake.

"Hata Shirika la Ujasusi halikulazimika kufanya kazi kubwa, takwimu zilizopikwa zimetangazwa, Urusi hata haijifichi, jibu pekee kwa kitendo hiki cha mvamizi ni kuisaidia zaidi Ukraine na nawashukuru washirika wetu ambao wamethibitisha uungaji mkono wao kijeshi, kifedha na kwa vikwazo," alisema Zelensky. **DW**

## ORODHA YA MAJINA YA WANACHAMA WA CCM WALIOTEULIWA KUGOMBEA NAFASI ZA UENYEKITI WA CCM WILAYA

INATOKA UK. 10

23. SINGIDA
NA. WILAYA — WALIOTEULIWA KUGOMBEA

1. SINGIDA MJINI
1. Lucia Andrea MWIRU
2. Athuman Hamis TIKAE
3. Maulidi Juma SELEMANI
4. Hassan Rajabu TATI

2. SINGIDA VIJIJINI
1. William Mwang'imba NYALLANDU
2. Jumanne Abdalah KUMALA
3. Hamisi Rajabu NKUNGU

3 MANYONI
1. Grace Hosea MLULE
2. Elia Abrahamu NOLLO
3. Jumanne Ismail MAKHANDA

4. IKUNGI
1. Japhari Hamisi DUDE
2. Mika Lucas LIKAPAKAPA
3. Shabani Dude ITAMBU

5. IRAMBA
1. Samwel Ashery JOEL
2. Daniel Athumani SIMA
3. Elias Kitalama MKOMA

6. MKALAMA
1. Lameck Clement ITUNGI
2. Apolo Samwel MASANJA
3. Mpazi Napengwa PAULO

24. SONGWE
NA. WILAYA — WALIOTEULIWA KUGOMBEA

1. SONGWE
1. Hamad Ramadhani JUMA
2. Fatuma Hussein NKELANZA
3. Mabrouk Albert MWAISELO

2. MBOZI
1. Willson Mwima SIMBEYE
2. Majaliwa Leopard MLAWIZI
3. Saimon Ndosta MBOYA

3. ILEJE
1. Patrick Alisile GHAMBI
2. Maisha Withus SILWIMBA
3. Assa Michael MBEMBELA

4. MOMBA
1. Silvester Martin LWILA
2. Weston Allam SIMWELU
3. Frank Mofati MBEMBELA
4. Sophia Daimon MWANJANJA

25. TABORA
NA. WILAYA — WALIOTEULIWA KUGOMBEA

1. KALIUA
1. Elias Kaseko GITTI
2. Selemani Denis ONESMO
3. Rashid Juma NAMBARI

2. SIKONGE
1. Alaija Jordan MWIGA
2. Anna Wilison CHAMBALA
3. Nassor Juma KALUNGWANA

3. IGUNGA
1. Mafunda Jingweka TEMENYA
2. Amos Jegu MAHENE
3. Abubakar Shaaban ABDALLAH

4. TABORA MJINI
1. Dunia Yusufu DUNIA
2. Tausi Maulid KAPAYA
3. Mohamed Athumani KATETE

5. URAMBO
1. Mussa Shaban MOHAMED
2. Emmanuel Chrisantus SOKO
3. Emmanuel Kefas GEMBE

6. NZEGA
1. Lt. (Mst) Maganga Midelo SENGELEMA
2. Alex Maziku KILONDELA
3. Madebe Nhale KALEKWA

7. UYUI
1. Lubasha Saidi MAKOBA
2. Hamza Abdallah SHOO
3. Tabu Abdalla MPAMBWE

26. TANGA
NA. WILAYA — WALIOTEULIWA KUGOMBEA

1. KOROGWE MJINI
1. Robert William BAGO
2. Thobias Mugweta NUNGU
3. Stephen Ngwanyemi MDOE

2. KOROGWE VIJIJINI
1. Nassoro Hemed NASSORO
2. Ally Abdallah WAZIRI
3. Hemedi Bakari KINGAZI

3. MUHEZA
1. Laick Said GUGU
2. Peter Joseph MHANDO
3. Hussein Hassan KISIMBO

4. MKINGA
1. Abdallah Seif SINGANO
2. Ismail Omari KASSOMO

5. LUSHOTO
1. Rashid Hassan SHEKARATA
2. Ally Kassim DAFFA
3. Hussein Selemani JAMBIA
4. Sadakati Hamisi KIMATI

6. HANDENI
1. Amiri Ramadhani CHANGOGO
2. Ahmadi Salehe CHIHUMPU
3. Ramadhani H. DILIWA

7. KILINDI
1. Alhaji Mohamed Rajabu ZAMBO
2. Hamisi Said KAMAU
3. Mohamed Rajabu KUMBI

8. TANGA
1. Meja (Mst) Hamisi Bakari MKOBA
2. Selemani Bakari ZUMO
3. Hamida Abass MOHAMED

9. PANGANI
1. Twalibu Mohamed AKIDA
2. Abdallah Mahmoud ABDALLAH
3. Pilli Ally OMARI

(b) Kwa Upande wa Zanzibar

1. KASKAZINI PEMBA
NA. WILAYA — WALIOTEULIWA KUGOMBEA

1. MICHEWENI
1. Maryam Omar ALI
2. Ali Massoud KOMBO
3. Hidaya Omar KHAMIS

2. WETE
1. Ali Bakari ALI
2. Khamis Ali HAMAD
3. Juma Shaaban JUMA

2. KASKAZINI UNGUJA
NA. WILAYA — WALIOTEULIWA KUGOMBEA

1. KASKAZINI 'A'
1. Haruna Juma HASSAN
2. Ali MAkame KHAMIS
3. Foum Haji KOGE

2. KASKAZINI B
1. Ali Khamis ALI
2. Zamir Makame BARO
3. Simba Haji MCHA
4. Ali Maabadi OMAR

3. KUSINI PEMBA
NA. WILAYA — WALIOTEULIWA KUGOMBEA

1. CHAKECHAKE
1. Suleiman Juma ALI
2. Ali Mohamed Ali CHANDE
3. Khamis Salim KHAMIS

2. MKOANI
1. Chumu Abdalla ABDALLA
2. Ali Juma NASSOR
3. Bikombo Ali OMAR

4. KUSINI UNGUJA.
NA. WILAYA — WALIOTEULIWA KUGOMBEA

1. KATI
1. Ali Abdulla HAJI
2. Hidaya Juma MAKAME
3. Hassan Mrisho VUAI
4. Hassan Mussa BAKARI

2. KUSINI
1. Shafi Hamadi ALI
2. Mgana Idi KHAMIS
3. Ali Hilal MNOGA

5. MAGHARIBI
NA. WILAYA — WALIOTEULIWA KUGOMBEA

1. DIMANI
1. Omar Mzee HASSAN
2. Maabadi Ali MAULID
3. Hussein Ali MJEMA (KIMTI)

2. MFENESINI
1. Idd Sultani LUWAMBO
2. Mbarouk Mrakib MBAROUK
3. Daud Silas MUKAKA
4. Kesi Mashaka NGUSA

6. MJINI.
NA. WILAYA — WALIOTEULIWA KUGOMBEA

1. AMANI
1. Ndiye Rajab ALI
2. Seif Amir SEIF

2. MJINI
1. Abdalla Rashid ABDALLA (Mamba)
2. Juma Fakih CHUM
3. Hamid Bilal GHARIB
4. Hamid Mbwana SAID

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ERNEST RICHARD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S2354/0541/2016** kilichotolewa na Baraza La Mitihani La Taifa kupitia **EAGLES SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/384349/2022**

---

**IN THE COURT OF TANZANIA (COMMERCIAL DIVISION) AT ARUSHA**

**MISC.COMMERCIAL APPLICATION NO.15 OF 2018**
**(Arising from Commercial Case No.3 of 2022)**

**STEPHEN MAHENDEKA MGANGA...,..APPLICANT**
**VERSUS**
**BEST WAY CAPITAL MANAGEMENT LIMITED (BCM)...RESPONDENT**

**SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION**

**TO:**
**Managing Director,**
**Best Way Capital Management Limited (BCM)**
**P.o.Box 105395,**
**DAR ES SALAAM .**
**Mobile :0758126202**

TAKE NOTICE that the Applicant has instituted a suit against you with particulars of claim set out in the application field in this Court.

Service of the Summons on you has been ordered by means of this publication. You are directed to collect copies of the summons and application from the Court's Registry,P.O.Box 3140 Arusha.

You are hereby summoned to appear in this Court in person or by an Advocate or an agent duly authorised on 18th day of October,2022 at 09:00 a.m .when this application will be mentioned.

TAKE FURTHER NOTICE that, should you default to enter appearance in Court on the day and time mentioned above, the case will proceed and ruling may be given in your absence.
Given under my Hand and the Seal of Court this 26th day of September,2022.

DEPUTY REGISTRAR
ARUSHA

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY**
**AT DAR ES SALAAM**
**CIVIL CASE NO. 39 OF 2021**
**MUSSA SHAIBU MSANGI......................PETITIONER**
**VERSUS**
**CHIEF EDITOR, TANZANIA MPYA ONLINE TV...............1ST RESPONDENT**
**TANZANIA MPYA MEDIA COMMUNICATION LIMITED............2ND RESPONDENT**

**SUMMONS FOR PUBLICATION**

**TO:**
**CHIEF EDITOR,**
**TANZANIA MPYA ONLINE TV,**
**DAR ES SALAAM,**

**WHEREAS,** the above mentioned case has been fixed for mention 4th day of OCTOBER, 2022 at 9:00 AM before Hon DR. J.L. MASABO-judge you are required to appear in this court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that day aforementioned, the suit will be heard and determined in your absence.
**GIVEN under my HAND and SEAL of Court 4TH day of AUGUST, 2022**

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY**
**AT DAR ES SALAAM**
**CIVIL CASE NO. 39 OF 2021**
**MUSSA SHAIBU MSANGI.................PETITIONER**
**VERSUS**
**CHIEF EDITOR, TANZANIA MPYA ONLINE TV..............1ST RESPONDENT**
**TANZANIA MPYA MEDIA COMMUNICATION LIMITED..............2ND RESPONDENT**

**SUMMONS FOR PUBLICATION**

**TO:**
**TANZANIA MPYA MEDIA**
**COMMUNICATION LIMITED,**
**DAR ES SALAAM,**

**WHEREAS,** the above mentioned case has been fixed for mention 4th day of OCTOBER, 2022 at 9:00 AM before Hon DR. J.L. MASABO-judge you are required to appear in this court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
TAKE NOTICE that in default of your appearance on that day aforementioned, the suit will be heard and determined in your absence.
**GIVEN under my HAND and SEAL of Court 4TH day of AUGUST, 2022**

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ABUU S. NDUNGURU**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SANLG YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC.430 AEQ.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

TAARIFA YA POLISI

**MBE/MBE/RB/385237/2022.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**WALTER ERNEST NKYA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 703 CUR – SUZUKI SWIFT.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

Taarifa ya Polisi:

**DAR/GOG/RB/125392/2021.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 827 OF 2022**

**In the matter of the Estate of the late VICTOR EDWARD SHAYO**

**AND**

**In the matter of Application for letters of administration by MONICA VICTOR SHAYO**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 17 Day of 10,2022.

**Dated at DAR ES SALAAM this 22 day of 09, 2022.**

Senior Resident Magistrate

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Sultan ageuka mshauri mitandaoni

Na Mwandishi Wetu

MSANII na Mtangazaji, Idris Sultan, ameibuka na kuwashauri watu kwamba, uzinzi unachoma sana uchumi katika taifa lolote.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Sultan, amesema kuwa katika uzinzi wanawake tu ndio hunufaika na si wanaume.


"Uzinzi unachoma sana uchumi, ni wanawake tu ndo angalau wanafanikiwa na uzinzi," aliandika Sultan.

Baadhi ya watumiaji wa Twitter walimshambuliaji kwa maneno mengi huku wengine wakimtania kwamba kauli hizo zake ni kama amerubuniwa na nauli na mwanadada ambaye baadaye hakutokea na ndio chanzo cha falsafa kama hizo kwamba wanawake tu ndio hufaidika kutokana na uzinzi.

Licha na kumshambulia, wengi walionekana kukubaliana na kauli yake hiyo hadi kunukuu maandiko matakatifu kwenye Biblia yanayokemea uzinzi.

"Sio uchumi tu unamfanya anayezini awe mpumbavu kwetu, sisi wakristo biblia inatuambia 'azinie na mwanamke hana akili kabisa afanya jambo litakalo angamiza nafsi yake, atapata jeraha na kuvunjiwa heshima, wala fedheha yake haitafutika' Mithali 6:32,33," alindika mmoja wa wachangiaji.

Sultan alijizolea umaarufu ndani na nje ya Tanzania mwaka 2014 aliposhinda tuzo ya Big Brother Africa Hotshots.





# NIFFER AKATAA KUTOKA NA KIBA

Na Mwandishi Wetu

MREMBO na mjasiriamali, Niffer amefunguka kuhusu tetesi za kuwahi kuwa kwenye penzi na nyota wa Bongo Fleva, Ali Kiba.

Katika mahojiano na kipindi kimoja cha redio cha usiku, mrembo huyo alisema kwamba, wengi wanaamini kwamba alikuwa kwenye mahaba na Kiba, lakini si kitu cha kweli.

Niffer alisema; "Sijawahi kuwa kwenye mahusiano na Ali Kiba, walitukuhusisha kwenye mahusiano sababu Ali ni 'handsome' na mimi ni 'beautiful'.

"Naamini yeye ana ladha yake ya wanawake na mimi nina ladha yangu ya wanaume.

"Mimi ni miongoni mwa wanawake anaoweza kutoka nao, asingekuwa maarufu na kwenye ndoa ningetoka naye, nina vigezo vyote vya kutoka naye.

"Kinachonivutia kwa Ali, ni Muislamu, ni mkarimu, akiwa rafiki yako 'utaenjoy' urafiki wenu.

"Ali alikuwa mtu wa kwanza kunifariji nilivyoanza kuonewa mtandaoni baada yeye 'kuni-tag' kwenye siku ya kuazimisha siku ya kuzaliwa, hivyo naheshimiana naye tu na hatujawahi kuwa wapenzi," alisema Niffer.



# Hailey: Sikumuiba Bieber kwa Selena

**LOS ANGELES,** Marekani

MWANAMITINDO, Hailey Bieber amekanusha uvumi kwamba, yeye alichangia kwa kiasi kikubwa kuvunja penzi la Justin Bieber na rafiki yake, Selena Gomez kabla ya yeye kuolewa naye.

Akizungumza katika kipindi cha televisheni cha Call Her Daddy kinachoongozwa na mtangazaji, Alex Cooper, Hailey alidai uvumi huo haukuwa wa kweli na bado watu wanaamini kwamba alimuiba Bieber kutoka kwa Selena.

Mahojiano hayo yalikuwa sehemu ya kusherehekea miaka minne ya ndoa yake na Bieber, lakini akabainisha bado kuna maswali kuhusu yeye kuharibu penzi la Selena.

"Watu walikuwa wakitamani sana (Justin na Selena) kuwa pamoja," alisema na kuongeza kuwa hakuwahi kuwa kwenye mapenzi kwa wakati mmoja.

"Sijawahi kuzungumza juu ya hili kamwe. Chuki nyingi zimekuwa juu yangu kwamba nilimwiba. Lakini inahitaji watu wajue ukweli, kwa sababu upo wazi."

Kabla ya kufunga pingu za maisha na Hailey, Justin alikuwa kwenye uhusiano ya kuachana na kurudiana na Selena kwa takriban miaka nane.

Nyota hao walirejesha uhusiano wao mwishoni mwa 2017 kabla ya kuuacha rasmi mapema mwaka 2018. Na Mei 2018 E!News iliripoti kuwa Selena "amehama kabisa" kutoka kwa Justin.

Juni mwaka huo huo, Justin, alipigwa picha akiwa na Hailey. Na kuanzia wakati huo na kuendelea, Hailey na Justin wakawa wapenzi.

Septemba 2018, Hailey na Justin walifunga rasmi ndoa katika mahakama ya New York City.

# CLASS AJIGAMBA KUTOA KICHAPO KWA MMEXICO

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA nyota wa Tanzania, Ibrahim Class, ametamba kumtembezea kichapo mpinzani wake, Gustavo Pina Melgar kutoka Mexico katika pambano la kimataifa lililopangwa kufanyika kesho katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

**Pambano hilo limeandaliwa na Kampuni ya MO Boxing, ikiwa ni mara ya kwanza kwa kampuni hiyo chini ya Mfanyabiashara maarufu, Mohammed 'Mo' Dewji.**

Class alisema baada ya kukaa nje ya ulingo kwa muda mrefu, ameamua kurejea kwa kasi kwa lengo la kutwaa mikanda mbalimbali ya ngumi za kulipwa nchini."

Alisema amejiandaa vema kwa ajili ya pambano hilo na hatamdharau mpinzani wake kwani anaamini naye amekuja kwa ajili ya ushindi.

"Najua Melgar ni bondia mzuri, lakini si kwa kufikia kwangu, nimejiandaa vema na nitamwonyesha jinsi gani Tanzania ina mabondia wazuri na wenye vipaji vikubwa," alisema Class.

Kwa upande wa Melgar alisema amekuja kusaka ushindi ili kuboresha rekodi yake katika ngumi za kulipwa.

Mratibu wa pambano hilo kutoka MO Promotion, Ahmed Seddiqi, alisema maandalizi yamekamilika na kwamba kutakuwa na mapambano sita ya utangulizi.

Pambano la kwanza la utangulizi litakuwa kati ya bondia nyota wa Ghana, Alfred Lamptey ambaye atapambana na bondia Abraham Ndauendapo kutoka Namibia huku Juma Choki akizichapa na bondia wa kutoka Mexico, Jose Hernandez ambapo bondia kutoka Kenya Nicholas Mwangi atazipiga na Emmanuel Mwakyembe wa Tanzania.

Pambano lingine litakuwa baina ya bondia Sameer Anwar dhidi ya Adam Mrisho huku Mwinyi Mzengela akizichapa na Sabari J na pambano lingine litakuwa baina ya Lulu Kayage dhidi ya Sadra Mohamed.

Mapambano hayo yamedhaminiwa na Kampuni ya Azam TV, Boxer, MO XTRA, Mlimani City, KCB Bank, White Sands Resorts, Bajaj na OTAPP.

Naye Mkuu wa Masoko na Uhusiano wa Benki ya KCB, Christine Mnyenye, alisema wanajisikia fahari kubwa kudhamini mchezo wa ngumi za kulipwa nchini.

"Tunajisikia fahari kubwa kudhamini mchezo wa ngumi za kulipwa hapa nchini ikiwa si mara yetu ya kwanza, tutatumia mchezo huu kutambulisha huduma yetu mpya ya bima na kuwaomba wadau wa ngumi za kulipwa na watu wengine kujiunga nayo ili kujiwekea kinga na majanga mbalimbali,"alisema Mnyenye.




Mratibu wa pambano la kwanza la Kampuni ya Mo Boxing, Ahmed Seddiqi (katikati), akiwatambulisha mabondia, Ibrahim Class wa Tanzania (kushoto) na Gustavo Pina Melgar wa Mexico jana, ambao watapanda ulingoni kesho katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# *Kocha Taifa Stars alia na mwamuzi Libya*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa, Taifa Stars, Honour Janza, amewasifu vijana wake kwa kupambana hadi dakika ya mwisho, wakionyesha kubadilika kwa siku za hivi karibuni licha ya kufungwa mabao 2-1 juzi kwenye Uwanja wa Modern, Benghazi dhidi ya Timu ya Taifa ya Libya, lakini alimshutumu mwamuzi kwa kuwatoa wachezaji wake mchezoni.

Kocha huyo alisema mwamuzi wa mechi hiyo alijaribu mara kwa mara kuwatoa wachezaji wa Taifa Stars mchezoni kwa kutoa maamuzi ambayo hayakuwa sahihi, lakini hilo linatokea kwenye mpira hasa unapocheza ugenini.

"Tumepoteza, lakini kama mnavyojua tulikuwa ugenini, tumepigana, Libya ni timu nzuri ina wachezaji wazuri wanaocheza soka la kasi na tumejifunza kitu na nina imani tukirudi kwenye ubao tunaweza kurekebisha baadhi ya mapungufu, lakini baadhi ya maamuzi hayakuwa mazuri, mwamuzi alijaribu kututoa mchezoni.

"Baadaye tulikaa na vijana tukaongea nao, walitufunga, tukarudisha, wakatufunga la pili, lakini nilichofurahishwa nacho ni upambanaji wa wachezaji, wamefanya kila wanachoweza, ila huu ni mpira, na Libya pamoja na kuwa ni timu nzuri, ilikuwa kwao," alisema kocha huyo raia wa Zambia.

Kwenye mechi hiyo, bao la kufutia machozi la Stars lilifungwa na Said Khamis.

Stars imemaliza ziara yake nchini humo ambapo ilikuwa kwenye mwaliko wa mechi za kimataifa zilizo kwenye Kalenda ya FIFA, ambapo mechi ya kwanza iliyochezwa Septemba 24, mwaka huu Tanzania iliichapa timu ya Taifa ya Uganda 'The Cranes' bao 1-0 lililowekwa nyavuni na Simon Msuva



## Mfungaji bora Cecafa atua Simba Queens

**Na Adam Fungamwango**

MFUNGAJI bora wa michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) ya Wanawake 2019, Jentrix Shikangwa, amesajiliwa na klabu ya soka ya Simba Queens kwa mkataba wa miaka miwili kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi hicho kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika zitazofanyika kuanzia Oktoba 30, mwaka huu nchini Morocco, pamoja na Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajia kuanza hivi karibuni.

Klabu ya Simba ilimtangaza mchezaji huyo raia wa Kenya kwenye mitandao yake ya kijamii, ikisema pamoja na mambo mengine ataisaidia timu hiyo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo Simba Queens inauwakilisha Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Hivi karibuni, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Mkoma alisema timu hiyo itasajili kipa pamoja na straika mmoja kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi hicho.

Starika huyo hatari amesajiliwa kutoka Fatih Karagumruk ya Uturuki, ambapo kabla ya hapo alikuwa akiichezea Vihiga Queens ya Kenya.

## Ndanda yaapa kurejea Ligi Kuu

**Na Baraka Jamali,** Mtwara

LICHA ya kutofanya vizuri katika michezo yao ya mzunguko wa kwanza na pili kwenye Ligi ya Championship, Ndanda FC maarufu kwa jina la 'Wanakuchele' wameeleza mikakati yao ya kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wachezaji hawadai fedha zao za usajili na kulipa mishahara kwa wakati.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Selemani Kachele, alisema wamejitahidi kuhakikisha wachezaji wote 27 wamelipwa stahiki zao na bodi yao ya wakurugenzi mpaka sasa imejitahidi kuhakikisha hawapitii changamoto yoyote.

Kachele alisema msimu huu wametumia zaidi ya Sh. milioni 36 katika usajili tu tofauti na miaka mingine huku bajeti ya siku kwa wachezaji hao ikiwa ni Sh. milioni 1.1 wakiwa nje ya Mtwara.

"Tumejitahidi kulipa kila mchezaji na hatudaiwi kama huko nyuma kwa wachezaji wapya ambao tumewasajili mwaka huu, japokuwa tunakiri kudaiwa madeni ya nyuma ya wachezaji waliopita, lakini tunashukuru kwa kazi kubwa inayofanywa na bodi ya wakurugenzi wa timu yetu," alisema.

## ZISIKUPITE

### MESSI KUONDOKA PSG

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35, anatarajiwa kuondoka Paris St-Germain msimu ujao kwani atakataa ofa yoyote ya mkataba mpya. ***(Beteve, via Star)***

### BAYERN YAKOMAA NA KANE

MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, anabaki kuwa mlengwa namba moja wa Bayern Munich, huku miamba hao wa Ujerumani wakitarajiwa kujadiliana tena uamuzi wa Tottenham. ***(Kicker, via Sun)***

### KUMRUDIA MADDISON

KLABU ya Newcastle United iko tayari kutuma ofa ya tatu kwa kiungo wa kati wa Leicester City na England, James Maddison mwenye umri wa miaka 25, baada ya ile ya pauni milioni 40 na pauni milioni 45 kukataliwa. ***(Times)***

### BELLINGHAM APELEKWA UTD

KIUNGO wa Kati wa England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, anafaa kujiunga na Manchester United atakapoondoka Borussia Dortmund, kwa mujibu wa golikipa wa zamani wa pale Old Trafford, Ben Foster. ***(Metro)***

### FERNANDEZ ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL ambao pia wamehusishwa na Jude Bellingham, wameanza kulenga viungo wa kati mbadala na wanamfuatilia mchezaji wa Benfica na Argentina, Enzo Fernandez mwenye umri wa miaka 21. ***(Fichajes, via Teamtalk)***

### PULISIC BEI HAIPUNGUI

CHELSEA haitapunguza bei wanayohitaji ya pauni milioni 31 kwa winga wa Marekani, Christian Pulisic huku Juventus wakionyesha nia ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Calciomercato, via Express)***

### RONALDO ATAJWA AL HILAL

KLABU ya Al Hilal ya Saudi Arabia imedai mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, alikuwa na nia ya kujiunga nao msimu huu. ***(Mirror)***

### LINDSTROM AJIBU YA ARSENAL

MCHEZAJI wa Eintracht Frankfurt, Jesper Lindstrom mwenye umri wa miaka 22, amejibu ripoti zinazomhusisha na kuhamia Arsenal, akisema ni "klabu kubwa kama wao zinanitazama". ***(Tipsbladet via Express)***


### HARRISON MKATABA MPYA

LEEDS United inatarajia kuanza mazungumzo ya mkataba mpya na winga wa England, Jack Harrison, ambaye aliripotiwa kuwasilisha ombi la pauni milioni 20 kutoka Newcastle United. Mkataba wa sasa wa kiungo huyo wa kati mwenye umri wa miaka 25, utakamilika msimu wa 2024. ***(Football Insider)***

### AHUSISHWA ENGLAND

KOCHA Mkuu wa zamani wa Tottenham Hotspur na Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, ambaye amekuwa akihusishwa na kazi ya ukocha wa timu ya Taifa ya England, alikuwa Wembley kutazama mechi yao na Ujerumani waliyotoka sare ya mabao 3-3. ***(Telegraph)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TITE AIJIA JUU TUNISIA KWA RAFU YA NEYMAR

●●● Ni hatua ya kumtoa mchezaji nje ya Kombe la Dunia kuelekea...

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Tite amelaumu rafu ya Dylan Bronn dhidi ya Neymar wakati wa ushindi wa Brazil dhidi ya Tunisia, akidai ni "hatua ya kumtoa mchezaji kwenye Kombe la Dunia."

**'Selecao' hao walikamilisha maandalizi yao ya kwenda Qatar kwa ushindi mnono wa mabao 5-1 kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Tunisia juzi jijini Paris, huku Neymar akiwa miongoni mwa waliofunga mabao, wakati penalti yake ikimfanya afikishe magoli 75 kwa kikosi hicho.**

Lakini fowadi huyo wa Paris Saint-Germain alikumbana na changamoto nzito katika dakika ya 42 wakati beki wa Tunisia, Bronn alipomfanyia faulo mbaya na kulimwa kadi nyekundu.

Na wakati Tite alizungumzia mchezo huo dhidi ya kikosi cha Kocha, Jalel Kadri kwamba ulikuwa wa ushindani, hakufurahishwa na faulo aliyofanyiwa Neymar.

"Tulikuwa katika mazingira ambayo mashabiki wengi walikuwa kutoka Tunisia," alisema Tite baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Wakati fulani, nilijaribu kutafuta mashabiki wetu, walipungua. Hii imeunda mazingira ya ushindani.

"Mchezo wa uwanjani - tulijua ungekuwa wa ushindani, uaminifu, lakini sikufikiria hatua iliyotokea kwa Neymar. Ni hatua ya kumtoa mchezaji nje ya Kombe la Dunia.

"Tumejaribu kufanya mechi mbili za kirafiki na timu ambazo ziko kwenye Kombe la Dunia, kwa sababu kiwango cha mahitaji ni kikubwa sana, kimwili, kiufundi na kiakili. Tunisia walikuwa na michezo saba bila kufungwa.

"Roho ya ushindani haikuruhusu kucheza mechi ya kirafiki ambayo haina mgongano wa kihisia, kwa hiyo tulitaka kujiandaa, na tungeenda kuchukua hatari hiyo, ndio. Lakini ndio tuliamua."

Mabingwa hao mara tano wa dunia wanakwenda Qatar baadaye mwaka huu wakiwa hawajapoteza mechi 15 mfululizo na wapo Kundi G kwenye Kombe la Dunia pamoja na Serbia, Uswizi na Cameroon.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,034,9

MECHI KALI
RUVU SHOOTING
VERSUS
COASTAL UNION
1 | 2.11
X | 3.04
2 | 3.38

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa airtel money EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# N'GOLO AREJEA MAZOEZINI CHELSEA

**LONDON,** England

KIUNGO wa Kati wa Chelsea, N'Golo Kante, amerejea mazoezini akija kuongeza nguvu kubwa kwa 'The Blues' hao wanaosuasua baada ya kukosa mechi sita zilizopita za klabu hiyo katika michuano yote.

Kante, ambaye pia amekosa kuicheza Ufaransa kwenye mechi za Ligi ya Mataifa ya Uefa Septemba hii, hajashiriki tangu katikati ya Agosti wakati Chelsea ilipotoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Tottenham.

Wameshinda mara mbili pekee akiwa hayupo na wamepata vipigo visivyotarajiwa kutoka kwa Leeds United, Southampton na Dinamo Zagreb.

Mfaransa huyo alijiunga na klabu hiyo mwaka 2017 baada ya hapo awali kubeba Kombe la Ligi Kuu England akiwa na Leicester. Alitajwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa PFA na Ligi Kuu na pia aliisaidia Ufaransa kushinda Kombe la Dunia mwaka 2018.

Mafanikio ya Chelsea katika miaka ya hivi karibuni yamehusiana moja kwa moja na kiwango cha Kante, klabu hiyo pia ikishinda Kombe la FA mwaka 2018, Ligi ya Europa mwaka 2019 na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2021.

Lakini alikosa sehemu kubwa ya msimu wa 2019/20 wakati Chelsea haikushinda chochote na alicheza mechi 21 tu za Ligi Kuu England.

# Mikel Obi astaafu soka rasmi

**LONDON,** England

NAHODHA wa zamani wa Nigeria, John Obi Mikel ametangaza kustaafu kucheza soka la ushindani akiwa na umri wa miaka 35.

Kiungo huyo, ambaye alikuwa ameichezea Kuwait SC hivi majuzi, alitangaza rasmi kustaafu kucheza soka baada ya miaka 20 kuwa uwanjani.

Mikel alitumia muda mwingi wa siku zake za kilele kucheza pale Chelsea, akishinda mataji mawili ya Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi ya Europa.

Pia alinyanyua Kombe la FA mara tatu wakati akiwa na 'The Blues' hao na akashinda Kombe la EFL mwaka 2007.

Aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram: "Kuna msemo kwamba 'mambo yote mazuri lazima yafike mwisho' na kwa maisha yangu ya soka ya kulipwa, siku hiyo ni leo (juzi).

"Ninakumbuka miaka 20 iliyopita wakati nikianza kucheza, lazima niseme kwamba nimeridhishwa sana na yote niliyoweza kuyafikia.

"Yote haya yasingewezekana bila uungwaji mkono usioyumba wa familia yangu, mameneja, klabu, makocha, wachezaji wenzangu na muhimu zaidi mashabiki wangu waaminifu daima.

"Waliniunga mkono katika hali yangu ya juu na chini, hata siku ambazo sikufikia matarajio yako. Nasema asante sana.

"Pia nitapenda kuwatia moyo kila mmoja ambaye labda nilimtia moyo kwa njia moja au nyingine katika kipindi cha maisha yangu ya soka, kwamba kamwe usikate tamaa juu ya ndoto zako, kwani kila unapofikiria kuacha, jikumbushe kwa nini ulianza.

Mikel alicheza mechi 91 akiwa na Super Eagles na kilele cha maisha yake ya kimataifa kilikuwa ni ushindi wa Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2013.

HABARI MICHEZO

905,195/-

# MKAZI WA NJOMBE ALAMBA MAMILIONI JACKPOT BONUS

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Chalole Wilaya ya Njombe mkoani Iringa, Luka Amos Mwenda, ameibuka na kitita cha shilingi milioni sita kwenye Jackpot ya katikati ya wiki baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 zilizochezwa wiki iliyopita.

Akizungumza baada ya hafla fupi ya makabidhiano ya hundi jijini Dar es Salaam jana, Luka alisema alianza kucheza na SportPesa mwaka 2018 baada ya kuwa na Sh. 600 pekee kama chenji iliyobaki katika Tigo Pesa yake.

"Unajua wakati ule mwaka 2018 ulikuwa unaweza kubeti kwa shilingi 500. Hivyo nilijaribu nikaweka 500 na kuchagua nafikiri timu tano au sita ambazo zote zilikuwa timu kubwa tupu kama Juventus na Roma. Baada ya hapo mkeka wangu ulishinda shilingi 7,000 na kuwa mwanzo wa mimi kucheza na SportPesa," alisema.

Luka aliendelea kusema baada ya hapo hakujishughulisha na ubashiri mpaka Oktoba 15, mwaka jana. Akiwa Ilula kwenye mihangaiko yake alipigiwa simu arudi Njombe kuna dharura ya kifamilia. Wakati huo yeye alikuwa na Sh. 10,000 tu.

"Nilimuomba rafiki yangu Benson msaada akanitumia shilingi 2,000 asubuhi ambayo niliweka shilingi 1000 kwa 500, mikeka miwili na yote ilichanika ilipofika majira ya jioni".

"Sikukata tamaa nikaweka tena mkeka wa multibet wa timu 13 kwa shilingi 500. Safari hii mkeka ulishinda nikapata Sh. 35,000 na baada ya makato nilitoa Sh. 29,000 ambayo ilifanikisha dharura iliyonipeleka kijijini," alisema Luka.

Luka anaelezea kuwa alishawishika kucheza SportPesa baada ya rafiki yake Justin Nyago kuwa anashinda kila mara na kumpatia mgao kwenye sehemu ya ushindi wake.

"Alikuwa ananipatia elfu tano hadi 10 kila aliposhinda. Hiyo ilisababisha na mimi kuingia wivu na kuanza kujifunza na kushawishika kucheza mpaka leo".

Akizungumzia mkeka alioshinda, Luka alisema aliziona timu tarehe 20/9/2022 jioni na kuchagua timu za multibet na za Jackpot za Septemba 23 ambazo mechi zote zilichezwa siku moja. "Nilikuwa na Sh. 2,000 siku iliyofuata niliweka Sh. 1,500 kwenye akaunti ya SportPesa na kuweka mikeka mitatu tofauti ambapo miwili ilikuwa ya Multibet na mmoja ulikuwa wa Jackpot ya katikati ya wiki.

"Nakumbuka mkeka wa Multibet wenye Geita Gold ulichanika na pia tarehe 23 mkeka wa pili wa Mutibet nao ulichanika nikabaki na wa Jackpot tu. Mungu si Athumani mkeka huo nilikosa mechi moja na kupata timu 12 kati ya 13, hivyo kushinda shilingi milioni sita na ushehe kama Jackpot Bonus".

AMETUA...




Msanii Ruger kutoka Nigeria akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere Tanzania jana kwa ajili ya shoo kubwa 'Unmasked Edition' itakayo fanyika Ware-House (Zamani Next Door Arena) Masaki, keshokutwa Jumamosi. Wasanii wengine watakaotumbuiza ni Nyashinski kutoka Kenya na Jay-Melody wa hapa nchini. **MPIGAPICHA WETU**

## *Dejan ndiyo kama mlivyosikia*

INATOKA UKURASA 32

klabu ilimtafutia na kumlipia kama ilivyo utaratibu wa Simba ingawa inadaiwa alikuwa akisumbua kuwa hajaipenda hata kidogo.

Kingine akiwa kambini alimwambia meneja kuwa anataka chumba cha kulala cha peke yake na kutimiziwa takwa lake hilo, hivyo madai mengine ya kukiukwa kwa mkataba wake anapaswa kuyaeleza mwenyewe.

***Imeandaliwa na Saada Akida, Shufaa Lyimo na Hadija Mngwai***

## Kamwe aanika njia zake Yanga

INATOKA UKURASA 32

"Unaweza kukuta wewe Yanga, lakini baba na mama yako Simba, au wao mmoja Simba mwingine Yanga, sasa wewe ukiwa upande mmoja ukawa unafanya kazi ya kuidhalilisha taasisi nyingine, kuvunja heshima za wenzako, unaivunjia heshima pia familia yako, mimi binafsi nitasalia kwenye kile ambacho taasisi inaeleza nikifanye, nitaishi bila kuvuka mipaka, nitaheshimu utani uliopo, lakini sitoenda zaidi kwa kuvunja heshima ya watu wengine," alisema.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally alimpongeza Kamwe na kusema anampongeza yeye binafsi kwa kupata nafasi hiyo, lakini Klabu ya Yanga kwa kumpata Mwanayanga mwenzao kuifanya kazi hiyo badala ya kufanywa na mamluki, ingawa hakufafanua zaidi juu ya hilo.

Mbali na Kamwe, Yanga ilimtangaza raia wa Zambia, Andre Mtine kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo na Priva Abiud, maarufu 'Privaldinho', kuwa Msimamizi Mkuu wa Digitali na Maudhui.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/10/22 | 17:00 | Coventry vs Middlesbrough | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 02. 01/10/22 | 17:00 | Fulham vs Newcastle | 3.04 | 3.39 | 2.27 |
| 03. 01/10/22 | 17:00 | Rotherham vs Wigan | 2.33 | 3.19 | 3.09 |
| 04. 01/10/22 | 17:15 | Getafe vs Valladolid | 2.44 | 3.03 | 3.08 |
| 05. 01/10/22 | 18:00 | Strasbourg vs Rennes | 2.92 | 3.36 | 2.32 |
| 06. 01/10/22 | 19:30 | Sevilla FC vs Atletico Madrid | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 07. 01/10/22 | 19:30 | Werder Bremen vs Borussia Monchengladbach | 2.58 | 3.57 | 2.48 |
| 08. 02/10/22 | 14:00 | Lorient vs Lille | 2.92 | 3.42 | 2.30 |
| 09. 02/10/22 | 14:00 | Stoke City vs Watford | 2.38 | 3.18 | 3.03 |
| 10. 02/10/22 | 15:00 | Espanyol vs Valencia | 2.73 | 3.22 | 2.58 |
| 11. 02/10/22 | 16:00 | AJ Auxerre vs Brest | 2.67 | 3.36 | 2.52 |
| 12. 02/10/22 | 16:00 | Troyes vs Reims | 2.47 | 3.36 | 2.72 |
| 13. 02/10/22 | 16:00 | Sampdoria vs AC Monza Brianz | 2.31 | 3.29 | 3.04 |
| 14. 02/10/22 | 16:30 | Hertha BSC vs Hoffenheim | 2.97 | 3.56 | 2.21 |
| 15. 02/10/22 | 17:15 | Celta Vigo vs Betis | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 16. 02/10/22 | 18:30 | Leeds vs Aston Villa | 2.59 | 3.43 | 2.59 |
| 17. 02/10/22 | 19:30 | Girona vs Real Sociedad | 3.19 | 3.14 | 2.31 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 29/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 3370 | Persis Solo vs PSM Makassar | 3.09 | 3.04 | 2.24 |
| 12:30 | 4110 | Shanghai SIPG vs Chengdu Qianbao | 1.84 | 3.34 | 3.89 |
| 14:00 | 5278 | Dodoma FC vs Geita Gold FC | 3.14 | 2.74 | 2.40 |
| 14:30 | 1950 | Dalian Aerbing vs Shanghai Shenhua | 2.49 | 3.27 | 2.54 |
| 14:30 | 4819 | Wuhan Zall vs Shijiazhuang | 4.42 | 3.73 | 1.65 |
| 15:00 | 2547 | Akhmat Grozny vs Rostov | 2.09 | 3.20 | 3.25 |
| 15:00 | 3620 | Derincespor vs Amasyaspor | 1.49 | 4.03 | 5.50 |
| 15:30 | 2658 | AS Roma W vs AC Sparta Prague W | 1.14 | 7.27 | 11.79 |
| 16:00 | 3378 | FK Graficar Beograd vs Sloboda | 1.30 | 4.71 | 8.24 |
| 16:00 | 4737 | FC Brasov Steagul Renaste vs Hermanstadt | 4.03 | 3.25 | 1.84 |
| 16:00 | 5056 | Ruvu Shooting vs Coastal Union | 2.11 | 3.04 | 3.38 |
| 16:00 | 5085 | CA River Plate (Arg) vs Argentinos Juniors Reserve | 2.27 | 3.14 | 2.94 |
| 16:30 | 3353 | PSS Sleman vs Persita Tangerang | 1.67 | 3.49 | 4.63 |
| 16:30 | 3635 | Qizilqum vs Metallurg Bekabad | 1.76 | 3.14 | 4.71 |
| 16:30 | 5000 | FCM Alexandria vs Miercurea Ciuc | 4.32 | 3.63 | 1.69 |
| 17:00 | 1188 | Colon de Santa Fe Reserve vs Estudiantes de LP Reserve | 2.38 | 3.05 | 2.85 |
| 17:00 | 2720 | CA Aldosivi Reserve vs CA Tigre Reserve | 2.55 | 3.24 | 2.50 |
| 17:00 | 3609 | Atletico Tucuman Reserve vs Patronato Reserve | 1.75 | 3.50 | 4.14 |
| 17:00 | 4730 | Menemen Bld vs Bigaspor | 1.12 | 8.02 | 12.72 |
| 17:00 | 5698 | Macva Sabac vs Red Star Belgrade | 34.38 | 13.75 | 1.01 |
| 17:30 | 1466 | Fakel vs Kryliya Sovetov | 3.05 | 3.39 | 2.09 |
| 18:00 | 2375 | Sahab Club vs Shabab Al Ordun | 2.38 | 2.99 | 2.89 |
| 18:00 | 4142 | Honka vs HJK Helsinki | 2.72 | 3.05 | 2.48 |
| 18:30 | 5020 | MS Kiryat Gat W vs Maccabi Bnot Emek Hefer W | 1.36 | 4.94 | 6.12 |
| 18:45 | 3452 | Concordia Chiajna vs Universitatea Cluj | 3.23 | 3.13 | 2.12 |
| 19:00 | 1637 | Hapoel Nir Ramat Hasharon W vs Hapoel Beer Sheva W | 1.19 | 6.30 | 9.84 |
| 19:00 | 4176 | ASEC Mimosas vs Societe Omnisport | 1.35 | 4.71 | 6.68 |
| 20:00 | 2279 | Hobro vs Fremad Amager | 2.02 | 3.33 | 3.28 |
| 20:00 | 3258 | Bayern Munich W vs Real Sociedad W | 1.15 | 6.67 | 12.75 |
| 20:00 | 3739 | FC Giessen 1927 Teutonia 1900 VfB vs TUS Dietkirchen | 1.55 | 4.60 | 4.60 |
| 20:00 | 4718 | Kvarnsvedens IK vs Korsnas IF FK | 1.92 | 3.78 | 3.19 |
| 20:30 | 1839 | Spartak Moscow vs Zenit St Petersburg | 3.77 | 3.77 | 1.75 |
| 20:30 | 2101 | FC Maan vs Jazeera Amman | 3.15 | 3.10 | 2.17 |
| 20:30 | 2417 | VfL Oldenburg vs Luneburger Hansa | 1.50 | 4.44 | 4.83 |
| 20:30 | 4255 | Everton W vs Leicester City FC W | 1.50 | 4.23 | 5.12 |
| 20:30 | 5573 | Hapoel Petach-Tikva W vs Hapoel Katamon Jerusalem | 1.30 | 5.40 | 7.80 |
| 21:00 | 3198 | TUS Bersenbruck vs SC Spelle-Venhaus | 2.39 | 3.68 | 2.44 |
| 21:00 | 3676 | Atletico Grau vs Sport Boys Association | 1.73 | 3.68 | 4.02 |
| 21:00 | 5157 | AE Realidade Jovem SP W vs Pinda Sport Clube SP | 1.95 | 3.49 | 3.34 |
| 21:00 | 5470 | Sporting Cristal vs Asociacion Deportiva Tarma | 1.25 | 5.10 | 9.82 |
| 21:30 | 3034 | ACS Sirineasa vs Dinamo Bucuresti | 3.20 | 3.15 | 2.13 |
| 21:30 | 5184 | Barracas Central vs Gimnasia y Esgrima | 2.61 | 3.00 | 2.61 |
| 23:30 | 4250 | FBC Melgar vs Escuela Municipal Deportivo Binacional | 1.33 | 4.42 | 8.05 |
| 23:30 | 5379 | Cobreloa vs Magallanes | 2.14 | 3.09 | 3.24 |

IJUMAA - 30/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 21:00 | 1394 | Sporting Lisbon vs Gil Vicente | 1.29 | 5.22 | 9.03 |
| 21:30 | 3465 | Bayern Munchen vs Bayer Leverkusen | 1.32 | 5.78 | 6.78 |
| 22:00 | 4707 | Athletic Bilbao vs Almeria | 1.39 | 4.65 | 7.49 |
| 22:00 | 5994 | Angers vs Marseille | 3.92 | 3.71 | 1.82 |
| 23:15 | 1631 | Porto vs Sporting Braga | 1.72 | 3.82 | 4.32 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Septemba 29, 2022

Nipashe




Tite aijia juu Tunisia kwa rafu ya Neymar UKURASA 29

# Dejan ndiyo kama mlivyosikia Simba

## ●●● Mengi yaanikwa, kupanda pipa kurejea kwao kesho, uongozi wafunguka....

**Na Waandishi Wetu**

MENGI yamezidi kuibuka baada ya mshambuliaji mpya wa Simba aliyesajiliwa siku za mwisho kabla ya dirisha la usajili msimu huu kufungwa, Mserbia Dejan Georgijevic, kudaiwa kuposti mtandaoni taarifa ya kuvunjwa kwa mkataba wake kwa kile kilichoelezwa kwamba ni ukiukwaji wa makubaliano na klabu hiyo.

**Katika taarifa iliyosambaa jana mchana ikidaiwa ni akaunti yake ya Instagram, imemnukuu Dejan akieleza: "Ninathibitisha kwamba mkataba wangu wa ajira umevunjwa kwa sababu za msingi za ukiukwaji wa makubaliano na klabu. Asante mashabiki kwa sapoti na upendo mlionipa."**

Hata hivyo, Nipashe lilipomtafuta Dejan kutaka kujua ukweli wa 'posti' hiyo, hakupatikana kuthibitisha, lakini chanzo chetu cha uhakika ndani ya klabu hiyo kilikiri kuwa tayari ameondoka kambini Zanzibar na yupo jijini Dar es Salaam kwa mazungumzo na uongozi wa klabu hiyo.

Kilisema: "Ni kweli amerudi Dar es Salaam na anatarajia kuondoka kesho kwenda kwao, lakini kuna taarifa ameamua kufanya hivyo kwa sababu amepata timu Afrika Kusini."

Hata hivyo, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alipotafutwa hakupokea simu, lakini kwa upande wa Mwenyekiti wa Wanachama wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu alipotafutwa na Nipashe alisema: "Mtafute Dejan mwenyewe."

Alisema kama kaandika huko sawa, lakini siwezi kuzungumzia suala la mtandaoni. Nachojua Dejan Georgjevic ni mchezaji wa Simba na kama kutakuwa na taarifa tofauti kuhusu mkataba wake tutawajuza.

Nipashe lilipobisha hodi kwa Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda kutoka kambini visiwani Zanzibar kutaka kujua kama Dejan yupo kambini ama laa, alisema hawezi kulitolea ufafanuzi suala hilo kwani lipo nje ya uwezo wake.

"Siwezi kulitolea ufafanuzi suala hilo, hata hivyo nimepokea hii simu kwa heshima yako tu, nipo kwenye kikao ninaomba uutafute uongozi, alisema Mgunda.

Alisema hajapata taarifa yoyote ya kuondoka kwa mchezaji huyo na kudai akipata taarifa hizo ataweka wazi ukweli wa jambo hilo.

Aidha, Nipashe lilimtafuta Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, ambaye naye alisema: "Taarifa imetumwa na mchezaji mwenyewe kwa nini msimtafute, mimi siwezi kuzungumzia, mchezaji katuma kitu kwenye ukurasa wake.

"Kama kavunja mkataba kaamua yeye mwenyewe, klabu haijatoa taarifa yoyote, mimi siwezi kuzungumzia chochote na siwezi kusema kama ni kweli ama si kweli".


Kwa mujibu wa chanzo chetu kingine, kilieleza Dejan ni kama amejiwahi mwenyewe maana aliwekewa idadi kadhaa ya mabao ndani ya kipindi cha miezi sita awe tayari ameyafikia kitu ambacho huenda ameona ni kigumu kwake kukitimiza.

Aidha, kilizidi kuanika kwamba mshambuliaji huyo alihitaji kupangiwa 'apartment' ambayo

INAENDELEA UK. 31







Dejan. **Picha ndogo;** akiwasili bandarini Dar jana akitokea Zanzibar.

# Kamwe aanika njia zake Yanga

**Na Adam Fungamwango**

OFISA Habari mpya wa Yanga aliyetangazwa juzi, Ali Kamwe, amesema kuwa ataendeleza utani wa jadi uliopo baina ya klabu yao na Simba, lakini hatovunja heshima ya mtu, kumtusi au kudhihaki taasisi, badala yake atafanya kazi ambayo anatakiwa kufanya chini ya katiba ya klabu hiyo inavyoelekeza.

Akizungumza jana kwa mara ya kwanza baada ya kutangazwa rasmi, Kamwe ambaye hapo awali alikuwa mchambuzi wa masuala ya soka kwenye televisheni, redio na mitandao ya kijamii, alisema kazi yake kubwa ni kuhakikisha anahusika na mawasiliano na kuwajibika kwa Mtendaji Mkuu kama ilivyoainishwa kwenye Katiba ya Yanga ibara ya 39.

"Katiba ya Yanga ibara ya 39 inasema kazi ya Ofisa Habari ni kufanya mawasiliano yote ya klabu na kuwajibika kwa Mtendaji Mkuu, kwa hiyo mimi nahakikisha kuwa nahusika na mawasiliano ya klabu kwenda kwa mashabiki na wanachama kupitia tasnia ya habari, hili suala la kucharurana ni utamaduni uliojengeka, tunaheshimu utani wa jadi ndiyo mpira wetu ulivyo, utani wa hapa na pale unaweza kuwapo, lakini sidhani kama mimi naweza kufika hatua ya kumvunjia mtu heshima, kumdhihaki, kumtusi, mimi nimelelewa kwenye familia yenye kutunza maadili ya Mwafrika," alisema Kamwe.

Alisema kitendo cha kuitusi, au kuidhalilisha taasisi nyingine si ya kiuanamichezo kwani kwenye familia za Kitanzania zimegawana pande mbili za Simba na Yanga, hivyo kufanya hivyo pia ni kuivunjia heshima familia yako pia.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >